# ULINGANISHI NA ULINGANUZI WA TASFIDA ZA MATIBABU KATIKA KISWAHILI NA KIMARACHI

**NA**

**OYINDA PATRICK**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KUKUU CHA NAIROBI**

**OKTOBA, 2016**

## UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo chochote.

____________________________ ____________________________

**Oyinda Patrick** Tarehe

**Mtahiniwa (C50/72359/2014)**

Tasnifu hii imetolewa kwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

____________________________ ____________________________

**Dkt. Ayub Mukhwana** Tarehe

**(Msimamizi)**

____________________________ ____________________________

**Dkt. Jefwa Mweri** Tarehe

**(Msimamizi)**

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia babangu Sylvester Oyinda na mamangu Francisca Nekesa.

// SHUKRANI

Atukuzwe Mola kwa zawadi kuu ya nguvu, afya na maarifa ambayo amenijalia katika safari hii nzito. Kila mwanzo huwa na mwisho wake. Wasimamizi wangu wamekuwa nami kila mara na kunielekeza ipasavyo kando na kunipa moyo wa kutia bidii zaidi. Isitoshe, maarifa yao kweli yameitanua akili yangu zaidi kuelewa vyema jinsi ya kutangamana na kuchanganua maswala mbalimbali kwenye upeo mpana wa elimu, hasa katika lugha ya Kiswahili. Hongera sana wasimamizi wangu Dkt. Ayub Mukhwana na Dkt. Jefwa Mweri kwa kunitengea muda wenu, kuwa tayari kuisoma kazi yangu na kunielekeza ipasavyo. Mola awajalie hekima na ufanisi mkubwa katika kazi zenu.

Shukrani kuu pia ziwaendee wahadhiri wengine waliochangia pakubwa katika usomi wangu ili nikafika nilipo. Hongera prof. John Habwe, Prof, Raya Timammy, prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kinene wa Mutiso, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Amir Swaleh na Dkt. Evans Mbuthia. Mungu awazidishie hekima na nguvu zaidi katika kazi zenu.

Shukrani nyingi ziwaendee wazazi wangu mzee Sylvester Oyinda na mama Francisca Nekesa kwa kunilea na kunipa nafasi ya kutangamana na vitabu hadi kufikia kiwango hiki. Nawashukuru pia ndugu zangu Charles Oyinda, Everlyne Oyinda, Vincent Oyinda na Roselyn Oyinda kwa kunihimiza na kuniombea kila wakati. Namshukuru zaidi kakangu Charles Oyinda kwa kunielekeza ningali mdogo kwenye uwanja wa taaluma na kunihimiza kila wakati kufanya bidii shuleni. Sitamsahau shemeji Chrispinus Bwire kwa msaada wake tangu nilipokuwa kwenye shule ya upili. Pia, Everlyn Nabwire anastahili shukrani zangu kwa kunisaidia katika ukusanyaji wa data hasa kutoka kwa watafitiwa wa kike.

Shukrani kuu pia ziwaendee makasisi wa shirika la Vincentian, Lavington kwa msaada wa maombi niliopata kutoka kwao. Pia, marafiki zangu Maximilla, Evans, Kimathi, Josephat, Sarah, Pius, Emmanuel, Noah, Michael na Hiram wanastahili shukrani zangu. Isitoshe, nawashukuru wenzangu tuliokuwa nao darasani ambao ni Edward, Sarah, Tecla, Catherine, Makori, Kimwea, Mumo, Virginia, Lilian, Aluvitsa, Adoli, Wakesho na wengine wote.

Sina budi kumshukuru mwalimu mkuu wa shule ya upili ya St. Mary's – Nairobi pamoja na walimu wenzangu kwa kunipa nafasi ya kuendeleza kazi hii hadi upeo huu.

# IKISIRI

Tasnifu hii imeangazia ulinganishi na ulinganuzi wa tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi. Tumejikita katika tasfida za tiba, ushauri nasaha, uhamasishaji na uasaji. Tulichagua mada hii kwa sababu ulimwengu hivi leo unakumbwa na janga la ukumwi na magonjwa mengine hatari ambayo huhitaji kuzungumziwa kwa lugha ya upole ili ujumbe uwafikie walengwa kwa njia isiyotisha, kukera au kuzua aibu. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kubainisha tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi, kuangalia mfanano au tofauti za tasfida hizo na mikakati inayotumiwa kuibua tasfida za muktadha wa matibabu katika jamii lugha husika. Data kuhusu tasfida za matibabu katika Kiswahili tumeipata kwa kusoma kamusi za semi, kamusi sanifu ya TUKI na vitabu vingine vya Kiswahili sanifu tulivyopata. Data kuhusu lugha ya Kimarachi nayo tumeipata nyanjani kwa kuwasilisha hojaji kwa baadhi ya watumiaji wa Kimarachi tuliowachagua kwa njia ya kimaksudi ili wajaze. Mtafiti pia ametumia ujuzi wake kama mwanafunzi wa Kiswahili na mzungumzaji wa Kimarachi kutathmini tasfida husika. Tuliwahusisha wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji na wanajamii wengine kujaza hojaji hizo. Pia, tulifanya mahojiano na wazee wachache wanaozungumza Kimarachi ambao hawajaathirika kwa vyovyote na elimu au hata kusafiri ng'ambo. Tumebainisha tasfida zinazotumiwa katika tiba na ushauri nasaha na zile zitumiwazo katika uhamasishaji na uasaji katika Kiswahili na Kimarachi kisha tukazipanga kwenye majedwali. Tumechunguza idadi ya tasfida hizi, mfanano au tofauti zake katika lugha tafitiwa na mikakati inayotumiwa kuibulia tasfida hizo. Tumechanganua data tuliyoipata kwa kutumia nadharia mbili: nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........ ii

**TABARUKU** ........ iii

**SHUKRANI** ........ iv

**IKISIRI** ........ vi

**ISTILAHI MUHIMU** ........ x

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**1.1. Usuli wa mada** ........ 1

**1.2. Tatizo la utafiti** ........ 4

**1.3. Madhumuni ya utafiti** ........ 5

**1.4. Nadharia tete** ........ 5

**1.5. Sababu ya kuchagua mada** ........ 6

**1.6. Upeo na mipaka ya utafiti** ........ 7

**1.7. Msingi wa kinadharia** ........ 8

**1.7.1. Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974)** ........ 9

**1.7.2. Nadharia ya upole kulingana na Brown na Levinson (1987)** ........ 15

**1.8. Yaliyoandikwa kuhusu mada** ........ 19

**1.9. Mbinu za utafiti** ........ 23

**1.9.1. Sampuli na jinsi ya kuipata** ........ 23

**1.9.2. Vifaa vya kutumia** ........ 24

**1.9.3. Njia za kuchanganua data** ........ 25

**SURA YA PILI** ........ 26

**TASFIDA ZA TIBA NA USHAURI NASAHA** ........ 26

**2.1. Utangulizi** ........ 26

**2.2. Tasfida za Tiba na Ushauri Nasaha** ........ 26

**2.2.1. Tasfida za Kutaja Magonjwa** ........ 27

**2.2.2. Tasfida za Kutaja Takamwili** ........ 34

**2.2.3. Tasfida za Kutaja Vitendo vya Kutoa Takamwili** ........ 38

**2.2.4. Tasfida za Kutaja Sehemu za Siri Mwilini** ........ 43

**2.2.5. Tasfida za Kutaja Vitendo vya Kujamiiana** ........ 47

**2.2.6. Tasfida za Kurejelea Tendo la Kutoa Mimba** ........ 51

**2.2.7. Tasfida za Kurejelea Baadhi ya Dawa za Kuwatibu Wagonjwa** ........ 54

2.3. Hitimisho....................56

SURA YA TATU....................58
TASFIDA ZA UHAMASISHAJI NA UASAJI....................58
3.1. Utangulizi....................58
3.2. Tasfida za Uhamasishaji na Uasaji....................58
3.2.1. Tasfida za Tendo la Kuzini....................59
3.2.2. Tasfida za Kifo na Mambo Yanayoingiliana....................62
3.2.3. Tasfida za Kazi za Watu....................67
3.2.4. Tasfida za Hali za Watu....................70
3.2.5. Tasfida za Kurejelea Mwanamke aliye na Mimba....................74
3.2.6. Tasfida za Kurejelea Kitendo cha Mwanamke Kuzaa....................76
3.2.7. Tasfida za Magonjwa....................78
3.2.8. Tasfida za Vitendo vya Kufanya Ngono....................79
3.3. Hitimisho....................80

SURA YA NNE....................82
MIKAKATI YA UIBUAJI WA TASFIDA ZA MUKTADHA WA MATIBABU....................82
4.1. Utangulizi....................82
4.2. Mikakati ya Uibuaji wa Tasfida za Muktadha wa Matibabu....................82
4.2.1. Mkakati wa Kutumia Maelezo Marefu....................83
4.2.2. Mkakati wa Kutumia Tashhisi....................85
4.2.3. Mkakati wa Kutumia Maneno yenye Maana Fiche....................86
4.2.4. Mkakati wa Ujumuishaji....................91
4.2.5. Mkakati wa Kuunda Majina Mapya....................91
4.2.6. Mkakati wa Kutumia Sitiari....................93
4.2.7. Mkakati wa Kutumia Istilahi Zinazohusiana ya Matibabu....................94
4.2.8. Mkakati wa Kutumia Nyimbo....................95
4.2.9. Kubadilisha Mpangilio wa Sauti au Silabi katika Neno....................98
4.2.10. Mkakati wa Kutosema....................99
4.2.11. Mkakati wa Kutumia Ishara za Mikono....................100
4.2.12. Mkakati wa Kubadilisha Kategoria ya Neno....................101
4.2.13. Mkakati wa Kuibua Maana Mpya za Maneno....................101
4.2.14. Mkakati wa Kutumia Kinaya....................102

**4.3. Hitimisho** ..... **103**

**SURA YA TANO** ..... **105**
**MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO** ..... **105**
**5.1. Utangulizi** ..... **105**
**5.2. Muhtasari wa Matokeo** ..... **105**
**5.3. Changamoto** ..... **107**
**5.4. Mapendekezo** ..... **108**

**MAREJELEO** ..... **110**
**VIAMBATISHO** ..... **114**

## ISTILAHI MUHIMU

TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Uso chanya (positive face)

Uso hasi (negative face)

Jumuiya lugha (speech community)

Hali ya lugha (speech situation)

Tendo lugha (speech event)

Matendo ya kimawasiliano (communicative acts)

Mitindo ya kimawasiliano (communicative styles)

Njia za kuzungumza (ways of speaking)

# SURA YA KWANZA

## 1.1. Usuli wa mada

Neno tasfida linamaanisha utumiaji wa maneno ya upole na heshima katika lugha ambayo hayaudhi au kuwakera wasikilizaji lengwa kulingana na utamaduni wa jamii lugha husika. Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo yao kuhusu maana ya tasfida. Mmoja wao ni Leech (1974) ambaye anaeleza kuwa tasfida ni njia ya kurejelea kitu ambacho si kizuri kwa namna ambayo inakifanya kionekane kizuri kuliko jinsi kilivyo. Naye Lyons (1981) anaeleza kwa ufupi kuwa tasfida ni kujiepusha na maneno ambayo ni miiko. Fromkin (1990) anasema kuwa tasfida ni neno au kishazi ambacho huchukua nafasi ya neno ambalo ni mwiko kutaja au hutumiwa ili kuzuia mada ambazo hutisha au huudhi. Rawson (1995) anasema kuwa tasfida ni neno au kishazi ambacho watu hutumia badala ya maneno ambayo hayakubaliki kabisa au ni ya aibu kwao na kwa hadhira.  Kamusi ya Kiswahili sanifu, TUKI (2014) inaeleza tasfida kuwa ni matumizi ya maneno ya adabu au fiche yasiyoibua hisia mbaya kueleza dhana ambazo maneno yanayoziwasilisha hukera watu yasemwapo. Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa, tasfida ni namna au mkakati wa kutumia maneno au vishazi kwa njia inayoonyesha upole na heshima ili kuokoa nyuso za watumiaji lugha kwa kuzingatia utamaduni wa jamii lugha yoyote. Kwa hivyo, tasfida inaweza kuangaliwa kama mbinu inayotumiwa na wazungumzaji katika lugha fulani kuficha hali ambayo inaweza kuwatisha, kuwatia aibu au kuwaudhi watumiaji wa lugha hiyo husika iwapo itatajwa moja kwa moja.

Tasfida ni kipengele muhimu sana katika matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo katika jamii, ukiwemo muktadha wa matibabu ambao tunalenga kuchunguza katika utafiti wetu. Tumechagua muktadha huu wa matibabu kwa sababu watu wengi hasa

wanaotaka kutibiwa hufika hospitalini au zahanatini kueleza hali zao. Maelezo yao hulenga magonjwa mbalimbali, maumivu kwenye sehemu tofauti za siri mwilini, vitendo fulani hasi ambavyo pengine wametenda au kutendewa na hata uchafu mbalimbali kutoka milini mwao ambao wameshuhudia. Pia, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji na waasaji hutumia lugha ili kuwaelimisha au kuwaelekeza wanajamii kuhusu magonjwa hatari kama vile ukimwi. Wao hupaswa kutumia tasfida ili kuonyesha upole na kujiepusha na kuvuruga utamaduni wa jamii husika. Zaidi ya hayo, matumizi ya tasfida hulenga kuondoa kero, tishio na aibu kwa watumiaji lugha husika.

Lugha yoyote huakisi utamaduni na mazingira ya jamii lugha, hususan maadili, mahusiano, siasa, dini, na shughuli za kiuchumi kama vile ukulima na biashara. Utamaduni huu hupokezanwa na wanajamii lugha kupitia kwa lugha wanayozungumza. Khanfar (2012) anasema kuwa tunatumia lugha kujieleza na kuwaelewa watu wengine. Kama njia ya mawasiliano, lugha ni kiakisi cha mtu binafsi, jamii na utamaduni. Kwa hivyo, wanajamii lugha ambao ndio hujenga familia mbalimbali wana nafasi muhimu sana katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wao kupitia kwa lugha, hasa kwa kuzingatia tasfida.

Saussure (1974) anaamini kuwa lugha ni mfumo wa ishara. Kulingana na maelezo ya mwanaisimu huyu, lugha inaweza kufafanuliwa kuwa ni mfumo wa ishara nasibu ambazo hutumiwa na wanajamii lugha walio na utamaduni sawa kuwasiliana. Ni dhahiri kuwa lugha ni chombo muhimu cha kuupitisha utamaduni wa jamii lugha yoyote kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Lugha hubeba utamaduni wa jamii lugha husika. Basi, ili utamaduni huo uhifadhiwe na kupitishwa vyema kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kuathiriwa, wanajamii lugha wanapaswa kutumia lugha yao kwa uangalifu mkubwa ili wasije wakakipokeza kizazi kijacho maneno au msamiati unaoharibu picha ya utamaduni na mazingira yao au uhusiano wao.

Tasfida zina umuhimu mkubwa katika jamii lugha yoyote ile hasa katika kudumisha heshima, kupunguza kero au tisho na kuhifadhi nyuso za watumiaji lugha. Ili mawasiliano kufaulu miongoni mwa watumiaji lugha fulani kama vile Waswahili na Wamarachi, lazima lugha inyotumiwa idhibitiwe na kila mzungumzaji wa jamii lugha hiyo. Hata hivyo, hili litatokea tu ikiwa kila mwanajamii lugha anafahamu bayana tasfida zinazofaa kutumika katika mazingira mbalimbali kutaja hali za watu, vitu, vitendo au mambo fulani na maana za tasfida hizo.

Binadamu huona aibu kuyataja mambo au vitendo fulani, sehemu za siri kwenye mwili, takamwili au ugonjwa hatari ambao anaugua mbele ya muuguzi au watu wengine kwa fikra kuwa atachekwa na hata kutengwa na wanajamii wenzake. Zaidi ya hayo, wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji na hata wagonjwa huogopa kusema maneno kama hayo yanayokera na kuudhi mbele ya hadhira lengwa ili kujiepusha na uvurugaji wa utamaduni wa jamii lugha husika.

Kulingana na Herbert (2016), tasfida ni muhimu na huweza kutumiwa wakati wa kuzungumza na wagonjwa kiasi kwamba wataelekea kuelewa zaidi kuhusu hali ya ugonjwa wao na hata kupunguza uchungu wa kimawazo wanaopitia. Anaongeza kuwa matumizi ya tasfida kueleza ugonjwa fulani au hali ya mgonjwa huweza kumpa matumaini ikilinganishwa na matumizi ya lugha ya moja kwa moja kueleza magonjwa au hali hizo. Kwa hivyo, tasfida ni kipengee muhimu sana ambacho wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji, wagonjwa au wanajamii kwa jumla wanastahili kuelewa na kutumia katika shughuli za matibabu kwa lengo kufaulisha shughuli hizo bila kuwepo na kero, aibu, tishio au hata kuvuruga utamaduni ya watumiaji lugha husika.

## 1.2. Tatizo la utafiti

Ulimwengu leo unakabiliwa na majanga mengi likiwemo janga la ukimwi na janga hili linaweza kuelezeka kupitia kwa lugha hasa katika muktadha wa matibabu. Endapo lugha iliyotumika kulielezea haikusukwa kwa namna ambayo haitishi umma na kudhibiti utamaduni wa jamii lugha husika, huenda ujumbe uliolenga hadhira fulani usiweze kuifikia. Njia mojawapo ya kulisemea jambo zito kama janga la ukimwi kwa mfano, na ambalo huwakumba watu hasa kutokana na ngono ni kupitia kwa tasfida. Hivyo basi, utafiti huu unanuia kuchunguza tasfida za matibabu katika Kiswahili na Kimarachi na utaweza kuelekeza wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji na watumizi wengine wa lugha hizi katika mkondo wa kisawasawa hasa wanapozungumzia maswala ya matibabu kuhusiana na ugonjwa huu.

Ni kutokana na hali hii ya kulenga kutumia lugha isiyotisha, kukera au kuzua aibu kwa umma na ambayo inadhibiti utamaduni wa jamii lugha husika ambapo uchunguzi umefanywa kubaini tasfida zinazotumiwa kutaja magonjwa hatari kama vile ukimwi, vitendo ambavyo watu wamefanya au kufanyiwa, takamwili, sehemu za siri mwilini, vitendo vya kutoa takamwili na hali za watu kisha kuchunguza mikakati inayotumiwa kuunda tasfida hizo. Pia, tumechunguza kama kuna mfanano au tofauti zozote za tasfida hizo katika Kiswahili na Kimarachi kwa sababu lugha zote mbili ni za aina ya Kibantu

## 1.3. Madhumuni ya utafiti

Kulingana na mada niliyochagua, utafiti huu umeongozwa na madhumuni haya:

i. Kubainisha tasfida ambazo zinapatikana kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

ii. Kutambua iwapo kuna mfanano au tofauti zozote za tasfida zinazotumiwa kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

iii. Kuchunguza mikakati inayotumiwa kuibua tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

## 1.4. Nadharia tete

i. Kuna tasfida nyingi ambazo zinapatikana kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

ii. Kunao mfanano na tofauti za tasfida zinazotumiwa kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

iii. Ipo mikakati inayotumiwa katika uibuaji wa tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

## 1.5. Sababu ya kuchagua mada

Uchunguzi kuhusu tasfida zinazotumika katika muktadha wa matibabu, mikakati ya kuziibua tasfida hizo na mfanano au tofauti zilizopo kwenye tasfida zinazotumika katika muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi utawasaidia wauguzi kuwaelewa wagonjwa wao kwa haraka na kuwahudumia ipasavyo bila kuchelewa. Zaidi ya hayo, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji na waasaji wa umma kuhusu magonjwa hasa ugonjwa wa ukimwi pamoja na wanajamii wa lugha hizi tafitiwa wataelewa vizuri tasfida husika. Pia, watafahamu mikakati inayotumiwa kuziunda na kuzitumia tasfida hizo ipasavyo katika mazungumzo yao kwenye muktadha wa matibabu. Kutokana na utafiti huu, tumeweza kupata orodha ya tasfida mbalimbali za matibabu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi. Orodha hii itakuwa na manufaa makubwa kwa wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji, walimu, wanasiasa, wasomi na wazungumzaji wa Kiswahili na Kimarachi kwa jumla. Wao wataweza kujua tasfida zinazotumiwa hasa kurejelea magonjwa kama vile ukimwi, uchafu unaotoka mwilini, matendo mbalimbali ambayo ni ya aibu kutaja hadharani, hali za watu na sehemu zote za siri mwilini pamoja na mikakati inayotumiwa katika uundaji wa tasfida hizo. Watumiaji wa lugha hizi tafitiwa wataweza kutumia tasfida za muktadha wa matibabu ipasavyo bila kuzua tishio, kero au aibu yoyote.

Herbert (2016) anasema kuwa tasfida ni muhimu na huweza kutumiwa wakati wa kuzungumza na wagonjwa kiasi kwamba wataelekea kuelewa zaidi kuhusu hali ya ugonjwa wao na hata kupunguza uchungu wa kimawazo wanaopitia. Anasema kuwa muuguzi lazima apime kiasi cha uwazi katika mawasiliano akizingatia ujuzi wa mgonjwa na kiasi cha uchungu anaopitia. Anaongeza kuwa matumizi ya tasfida kueleza ugonjwa fulani au hali ya mgonjwa huweza kumpa matumaini ikilinganishwa na matumizi ya lugha ya moja kwa moja kueleza magonjwa au

hali hizo. Hii ndio maana tumechunguza tasfida ambazo hutumiwa katika muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi na mikakati inayotumiwa kuziibua.

Swala hili la kulinganisha na kulinganua tasfida za matibabu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi kulingana na uelewa wetu, halijawahi kufanyiwa utafiti na hivyo kuacha mwanya ambao utafiti huu utaziba.

### 1.6. Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu umelinganisha na kulinganua tasfida za matibabu katika Kiswahili na Kimarachi pekee. Tumechunguza mikakati inayotumiwa kuibua tasfida hizo na kubaini ikiwa kuna mfanano au tofauti zozote za tasfida za matibabu katika lugha hizi mbili tafitiwa. Tumejikita katika tasfida zinazohusiana na tiba, uhamasishaji, utoaji wa ushauri nasaha na uasaji wa watu kuhusu magonjwa hatari kama vile ukimwi. Tumeorodhesha tasfida zilizokamaa kimatumizi ambazo wanajamii katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi wanaweza kujifunza na kutumia katika mazungumzo kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole miongoni mwao na hata kudhibiti utamaduni wao. Utafiti huu umejikita katika kulinganisha na kulinganua tasfida ambazo hutumiwa kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi pekee. Hatujashughulikia swala la aina za tasfida zinazotumiwa kwa sababu ya upana wake na uchache wa muda tuliokuwa nao kutekeleza utafiti huu.

Tumechagua *kamusi za semi: methali, misemo na nahau* pamoja na kamusi ya *Kiswahili Sanifu* ya TUKI ambazo tumesoma na kuorodhesha tasfida zinazohusiana na matibabu, tulizopata katika lugha ya Kiswahili. Kamusi za misemo na nahau na ile ya methali zimetumika kwa sababu ndio huonyesha kwa kiasi kikubwa maneno ambayo ni tasfida hasa kwa kutumia lugha fiche. Misemo na nahau hutaja mambo fulani mazito kwa njia fiche isiyo na kero, tishio au aibu kwa watumiaji

lugha. Hata hivyo, tasfida zinazopatikana katika kamusi za semi na kamusi sanifu ya Kiswahili huwa zimesanifishwa. Tumechunguza tasfida hamsini pekee kutokana na muda mchache ambao tumekuwa nao kuutekeleza utafiti huu. Kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI pia huonyesha namna neno fulani linaweza kutumiwa kwa njia ya upole.

Kwa upande mwingine, data kuhusu Kimarachi tumeipata nyanjani kwenye wadi ya Kingandole, katika kaunti ndogo ya Butula kwa kuandaa hojaji na kuwapa watu arobaini wanaojua kusoma na kuandika ili wajaze. Tulichagua wadi ya Kingandole kwa sababu ndiko kuna hospitali kubwa inayoitwa Murumba kando na zahanati zingine ambapo shughuli nyingi za matibabu na utoaji wa ushauri nasaha hutekelezwa. Zaidi ya hayo, watu wengi huonekana kuangamia katika wadi hii kutokana na magonjwa hatari au hali mbalimbali ambazo wengi wao huogopa kusema au kutafuta matibabu kwa sababu ya kukosa maneno ya upole ya kujieleza. Tuliwachagua wazungumzaji wa Kimarachi kwa njia ya kimaksudi kujaza hojaji. Tulilenga wale walio na umri wa miaka 18 na zaidi, wa kiume na kike kwa sababu hawa ndio wanaelewa umuhimu wa tasfida katika mawasiliano na hivyo wanahitajika kutumia tasfida ipasavyo ili wadogo wao wajifunze maadili mema katika jamii lugha. Hii ni kwa sababu lugha katika jamii huhusisha makundi yote ya watu; vijana na wazee, wanaume na wanawake, (Hickey, 2012). Hata hivyo, tuliwahoji wazee wachache wa kiume na kike walio na miaka sitini na zaidi ambao hawajaathirika kwa namna yoyote na elimu ya kigeni au hata kusafiri ng'ambo. Wazee hawa pia tuliwachagua kwa njia ya kimaksudi.

## 1.7. Msingi wa kinadharia

Nadharia mbalimbali zimetolewa na wanaisimu kueleza swala la upole katika jamii. Jamii lugha yoyote huwa na lugha ambayo ndiyo chombo cha mawasiliano. Kwa hivyo, ni lazima mahusiano

yadhibitiwe vizuri kupitia kwenye lugha inayotumiwa ili mwingiliano mwema uwepo miongoni mwa wanajamii lugha husika. Tumetumia nadharia mbili katika utafiti wetu: Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

### 1.7.1. Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974)

Dell Hymes anajulikana na wengi kama mwanzilishi wa uwanja unaoitwa ethnografia ya mawasiliano. Alipendekeza ethnografia ya kuzungumza kama njia ya kusoma namna watu walizungumza. Baadaye, jina hili lilibadilika na kuwa ethnografia ya mawasiliano. Hymes (1962) alipendekeza nadharia hii ili kuwasaidia watafiti wanaochunguza matumizi ya lugha katika miktadha fulani. Alifikiria kuwa kwa kuangalia jinsi watu hutumia lugha, ruwaza fulani zingeonekana ambazo hazingegunduliwa kwa kuangalia tu maneno yanayotumiwa pekee.

Hymes (1974) anasema kuwa msingi ni uchunguzi wa kiethnografia ya mtagusano wa mawasiliano katika jamii. Mtagusano wa mawasiliano ni kile watu hufanya wanapowasiliana na wengine.

Katika harakati za kuchunguza mawasiliano ya utamaduni fulani, Hymes alipendekeza vitengo msingi sita ambavyo hudhihirisha ni kipengele gani cha utamaduni ambacho mtu anataka kuchunguza zaidi. Vitengo hivi ni:

i. Jumuiya lugha

ii. Hali ya lugha

iii. Tendo lugha

iv. Matendo ya kimawasiliano

v. Mitindo ya kimawasiliano

vi. Njia za kuzungumza

**1.7.1.1. Jumuiya lugha**

Jumuiya lugha ni kundi la watu ambao hutumia ishara zinazofanana katika mawasiliano. Ni watu wanaotumia sheria sawa kuhusu lini na namna gani watazungumza, pamoja na uelewa wao wa maana husika. Watu wa jamii lugha moja wataweza kuelewana katika mazungumzo yao kwa sababu wanaongozwa na sheria sawa katika utamaduni wao. Kwa mfano, Wamarachi wanaoishi kwenye wadi ya Kingandole huunda jumuiya lugha. Pia, Waswahili huunda jumuiya lugha yao.

**1.7.1.2. Hali ya lugha**

Kitengo hiki hupatikana kwenye jumuiya lugha. Hymes (1972) anasema kuwa unaweza kupata hali ya lugha kwa kuangalia wakati ambapo watu huzungumza au wasizungumze. Kwa mfano, mazingira ya matibabu kama vile hospitalini au zahanatini na vikao vya kutoa ushauri nasaha, uhamasishaji au kuasa watu ni hali lugha katika jamii lugha yoyote.

**1.7.1.3. Tendo lugha**

Kitengo hiki huwa na mwanzo pamoja na mwisho. Hymes (1974) anaeleza kuwa tendo lugha ni vitendo ambavyo vinaongozwa na sheria au kanuni za lugha. Kwa mfano, mazingira ya zahanatini au vituo vya kutoa ushauri nasaha huwa na tendo lugha. Mazingira haya yatamwongoza mzungumzaji kung'amua na kuteua msamiati au tasfida ambazo anastahili kutumia katika mazingira husika. Mazungumzo yanayoendelea katika mazingira haya ya matibabu kama vile hospitalini au kwenye vikao vya kutoa ushauri nasaha au kuasa wanajamii ndiyo tendo lugha.

#### 1.7.1.4. Matendo ya kimawasiliano

Kitengo hiki hueleza kuwa ni matendo yepi yanayofanywa maneno fulani yanapotumiwa na watu kwenye jumuiya lugha husika. Kwa mfano, mtu anapoambiwa kuwa asiteme mate ovyo ovyo mbele ya watu naye akatii na kutoyatema mate, basi kitendo cha mawasiliano kitadhihirika. Pia, mgonjwa wa kike anapomweleza daktari kuwa ‘hajaona mwezi’ kwa muda fulani kisha daktari akaelewa alichomaanisha na kumtibu au kumshauri ipasavyo basi tendo la mawasiliano litakuwa limetekelezwa. Matumizi ya maneno fulani pia huweza kuwaathiri wasikilizaji lengwa kwa kuwakera au kuwaogofya iwapo mzungumzaji hatateua na kutumia tasfida ipasavyo katika lugha yake.

#### 1.7.1.5. Mitindo ya kimawasiliano

Hurejelea jinsi ambavyo mtu fulani huzungumza. Kila mtu binafsi katika jumuiya lugha huwa na mtindo wa kipekee wa kuzungumza ambao huweza kumtofautisha na watu wengine. Kwa mfano, mitindo hii huweza kutofautiana kulingana na toni, uzito wa sauti na kasi ya kuzungumza kwani wengine huweza kuzungumza kwa toni ya juu ilhali wengine kwa toni ya chini au wengine wakazungumza haraka ilhali wengine polepole.

#### 1.7.1.6. Njia za kuzungumza

Humaanisha mitindo ya lugha ambayo huweza kutumika katika hali na matendo mbalimbali. Hutumiwa kueleza ruwaza ambazo zinahusishwa na utamaduni fulani. Kwa mfano, utamaduni unaomtarajia kila mwanajamii kutumia tasfida katika mazungumzo yake ya ana kwa ana au hata kupitia kwenye njia ya simu.

Baada ya kuchagua mojawapo ya vitengo hivi sita, mtafiti anaweza kuendelea kuchunguza kwa kutumia moja kati ya mbinu ambazo Hymes (1974) alipendekeza. Kitengo cha kutafitia ndicho humsaidia mtafiti kuchagua mbinu itakayotumiwa katika uchunguzi lengwa. Mbinu hizi ni:

i. Hali. Huhusisha mazingira. Hapa ndipo shughuli hutendeka, yaani huwa mazingira yote ambamo shughuli fulani imo. Kwa mfano, shughuli za matibabu hutendeka katika mazingira ya hosptalini au zahanatini, nayo shughuli ya utoaji wa ushauri nasaha huweza kutokea katika kituo cha kutoa ushauri nasaha au hata hospitalini.

ii. Wahusika. Hawa ni watu waliopo na kazi wanazofanya au uhusiano wao na wengine. Kwa mfano, tunapata daktari, wauguzi, wafanyakazi wengine, wagonjwa, wale wanaowatunza na wanajamii lugha wengine katika mazingira ambamo tiba hupatikana. Pia kuna mtoa ushauri nasaha na mshauriwa katika kituo cha utoaji wa ushauri nasaha.

iii. Hatima au malengo ya mawasiliano. Kinachotarajiwa kutokana na mawasiliano miongoni mwa wahusika. Kwa mfano, mzungumzaji hutambua hatima ya ujumbe anaopitisha kwa msikilizaji na lengo kuu la ujumbe huo. Hatima pia huweza kuwa kumpa mgonjwa matumaini au kumtibu ipasavyo baada ya muuguzi kuelewa matatizo yake.

iv. Matendo au matendo lugha. Huhusisha hali na ujumbe. Tendo lolote hutazamwa kama tendo la kimawasiliano ikiwa linapitisha maana kwa wahusika.

v. Toni ya lugha. Namna lugha inavyosikika au inavyowasilishwa. Mzungumzaji anaweza kuwasilisha ujumbe wake kwa toni ya juu, kadri au chini. Kwa mfano, mtu anayetoa ushauri nasaha anapaswa kuzungumza kwa toni ya chini ili asije akazua woga au aibu kwa mshauriwa.

vi. Njia mbazo mawasiliano hupitia pia huweza kuchunguzwa. Njia hizi huweza kuwa za ana kwa ana, njia ya simu au kwenye mtandao. Kwa mfano, wauguzi, wahamasishaji au watoa ushauri nasaha wanastahili kuzungumza ana kwa ana na wagonjwa au washauriwa mtawalia ili wapate nafasi ya kuwaona na kuelewa hali zao vyema.

vii. Sheria za mawasiliano au sheria zinazodhibiti mawasiliano pamoja na kueleweka huweza kudhihirisha maana. Kwa mfano, sheria katika jamii lugha husika ambapo kila mtumiaji lugha anapaswa kutumia lugha kwa njia ya upole.

viii. Vijigao vya lugha kitamaduni kama vile methali, misemo, nahau, maneno ya kuomba msamaha, maombi, mazungumzo yanayohusu shida za watu.

Kwa hivyo, Dell Hymes (1974) anasema kuwa ujuzi wa mawasiliano ni matumizi ya lugha kwa njia ambayo inaafiki lengo la mawasiliano. Ethnografia ya mawasiliano ni mbinu katika isimu ambayo imetokana na uwanja wa anthropolojia katika ethnografia. Ethnografia ya mawasiliano inahusika na mambo yafuatayo:

i. Maswala ya kiisimu yanayotumiwa na watu katika muktadha wa mawasiliano ambayo si tu isimu, lakini matumizi ya maneno ambayo maana yake inalingana na utaratibu wa jamii lugha, uhusiano wa maneno hayo na namna ya kuyatumia. Kila jamii lugha huwa na sheria zake ambazo huwaongoza wanajamii lugha husika jinsi ya kutumia lugha katika mawasiliano.

ii. Njia mbalimbali ambazo hutumika katika mawasiliano kama vile kutuma arafa ikilinganishwa na mazungumzo ya ana kwa ana miongoni mwa wanajamii lugha.

iii. Namna ishara za sauti na ishara zisizo za sauti huonyesha au kudhihirisha jamii lugha fulani, mahusiano, hisia, mahali na mawasiliano yenyewe.

Kulingana na Dell Hymes (1974), utamaduni ni ujuzi ambao wanajamii hugawana au hushiriki kwa pamoja na pia ni msingi wa tabia, ambao huleta maana fulani katika tabia za watu. Kwa hivyo, lugha inapotumiwa, hudhihirisha kipimo au kipeo cha utamaduni ambao ndio msingi wa tabia. Ethnografia ya mawasiliano pia huwasaidia watu kuelewa namna mawasiliano hutofautiana katika jamii lugha zenye utamaduni tofauti.

Nadharia hii imetusaidia kuchanganua data kwa kuangalia tasfida ambazo hutumika katika muktadha wa matibabu. Pia, tumetumia nadharia hii kulinganisha na kulinganua tasfida za muktadha wa matibabu, kwani maneno fulani huweza kuwa tasfida katika utamaduni wa jamii lugha moja lakini yasiwe tasfida katika jamii lugha nyingine kulingana na sheria zinazoongoza utamaduni husika. Pia, imetuwezesha kupima kuwa tasfida hizo huwa na lengo la kupunguza tishio, kero au aibu na kudhibiti utamaduni wa jamii lugha husika.

Tumejikita katika vipengele vya jumuiya lugha, hali ya lugha, tendo lugha na matendo ya kimawasiliano. Katika jumuiya lugha, tumeangazia jumuiya lugha ya watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi navyo vitengo vya hali lugha na tendo lugha vimetusaidia kutambua tasfida ambazo watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi hutumia katika mukatadha wa matibabu. Kitengo cha matendo ya kimawasiliano pia kimetuelekeza katika kufafanua kuwa tasfida zinazotumika kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi husaidia kupunguza kero, wasiwasi na kuficha aibu.

Miongoni mwa mbinu nane ambazo Hymes (1974) alipendekeza, tumechagua mbinu tano katika uanishaji wa data. Mbinu hizi ni : hali au mazingira, wahusika, malengo ya kimawasiliano, sheria

zinazodhibiti mawasiliano na vijigao vya lugha kama vile nahau na methali zitumiwazo. Mazingira tuliyolenga ni ya matibabu ambamo mna wahusika mbalimbali kama vile wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji na wanajamii kwa jumla. Wahusika hawa hulenga kupitisha ujumbe kwa watu wengine kwa lengo la kutimiza matibabu kwa njia ya tiba au uzuiaji wa magonjwa fulani kuenea. Lugha wanayotumia hustahili kuwa na upole na ambayo inazingatia sheria za utamaduni wa jamii lugha husika ili wahusika wasiwe na woga, aibu au kero.

### 1.7.2. Nadharia ya upole kulingana na Brown na Levinson (1987)

Brown na Levinson (1987) walipendekeza nadharia ya upole ambayo inaeleza swala la upole katika mawanda mapana ya utamaduni na lugha. Kulingana na Brown na Levinson, chanzo cha upole katika jamii zote kinatokana na dhana ya uso. Neno 'uso' lilitolewa katika kazi ya mwanasoshiolojia Goffman (1967), kumaanisha kitu kinachodhibitiwa katika maingiliano ya watu kwa kutumia njia au mikakati ya upole.

Uso katika muktadha wa upole hueleza azma au hamu ya kila mwanajamii lugha kuchunga uso wake dhidi ya uharibifu wowote. Kwa hivyo, uso ni hisia za kibinafsi kuhusu picha, sifa au majina mazuri ambayo mtu anayo na hutarajia kila mtu amtambue. Picha hii ya mtu binafsi inaweza kuharibiwa, kuhifadhiwa au kuendelezwa kutokana na kutangamana na wenzake. Kulingana na Brown na Levinson (1987), kuna aina mbili za uso:

i. Uso chanya: Huu ni uso unaotaka au kutamani kusifiwa, kuheshimiwa na kupongezwa na watu wengine. Uso huu unataka kuhusishwa na mambo mazuri pekee.

ii. Uso hasi: Uso ambao hautaki kuingiliwa na watu wengine katika kazi yake. Hutaka uhuru wake wa kutenda mambo bila kuingiliwa na mtu yeyote.

Matendo ambayo hutishia uso wa mtu huitwa matendo yenye tisho kwenye uso. Kwa hivyo, kila mtu katika jamii hujibiidisha kuzuia matendo ambayo yanaweza kuathiri uso wake na ule wa mwenzake katika mazungumzo yao.

Matendo ambayo huweza kuathiri uso wa mtu ni yale yanayohusisha kutaja maneno fulani bila kutumia tasfida kulingana na utamaduni wa jamii husika, malalamiko, matusi, kutoelewana na wengine, kuingilia kazi ya mtu mwingine bila ruhusa na kuomba ruhusa au hata kitu kutoka kwa mtu mwingine.

Brown na Levinson (1987) huona upole kama njia ya kujiepusha na mafarakano. Mzungumzaji anastahili kutathmini hatari za kudhuru uso wa mwenzake kisha achague mikakati ifaayo ili kupunguza hatari zinazoweza kutokea. Wazungumzaji huchagua mikakati inayofaa ya kuwasilisha ujumbe wao katika mawasiliano. Watumiaji lugha yoyote wanapojipata katika hali ambapo tendo la kudhuru uso linaweza kutokea, uamuzi wao hujikita katika mbinu au mikakati mitano ya upole iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Mikakati hii imepangwa kulingana na kiwango cha athari kwa uso kuanzia ule wenye athari kubwa hadi kwenye ule wenye athari ndogo sana:

i. Mkakati bayana usio na upole

ii. Upole chanya

iii. Upole hasi

iv. Mkakati wa nje ya rekodi

v. Kukosa kuwasilisha

#### 1.7.2.1. Mkakati bayana usio na upole

Mkakati huu huwa na kiasi kikubwa cha kutishia uso wa msikilizaji. Msemaji husema maneno ambayo hayana upole wowote.  Kwa mfano, “Musa amekufa.” Maneno haya hayana upole kwa sababu yanatisha na hayana heshima. Maneno hayo yangekuwa na upole ikiwa mzungumzaji angesema ‘Musa ameaga dunia” au “Musa ametuacha”. Mzungumzaji pia anaweza kusema kuwa “Mpando anaugua ukimwi.” Maneno haya yanaweza kuleta aibu, kero au tishio kwa wasikilizaji lengwa. Mzungumzaji anaweza kusema maneno haya kwa njia ya upole kuwa “Mpando ana ugonjwa mkubwa” au “Mpando alipata mdudu mbaya kiajali.”

Brown na Levinson (1987) wanasema mkakati huu hutumiwa na watu ikiwa mazungumzo ni ya dharura na hivyo mzungumzaji hana nafasi ya kutafuta au kuchagua mkakati unaofaa ili kuonyesha upole.

#### 1.7.2.2. Upole chanya

Mkakati huu hulenga kuokoa uso chanya wa msikilizaji kwa kutumia maneno yanayompendeza mzungumzaji katika mawasiliano. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kumsifu msikilizaji, akakubaliana naye, akampongeza, akamwahidi, kuonyesha kuwa anamjali msikilizaji huyo au kutumia maneno ya heshima katika mazungumzo. Mtoa ushauri nasaha au mhamasishaji anaweza kutoa ushauri kwa wanajamii kwa kusema hivi: “Nawapongeza wanajamii wote wa eneo hili kwa kuchukua hatua za kupunguza ugonjwa huu” badala ya kusema kuwa “Kila mwanajamii lazima achukue hatua kali za kupambana na ugonjwa hatari wa ukimwi”. Kauli ya kwanza ina upole kwa sababu mzungumzaji amewasifu kwanza wasikilizaji na baadaye kuonyesha kuwa walikuwa tayari kupunguza ugonjwa huo wa ukimwi. Pia, hajatumia neno kupambana ili kupunguza picha fulani inyohusu mapambano hatari.

#### 1.7.2.3. Upole hasi

Mkakati huu hulenga kuokoa uso hasi wa msikilizaji au wasikilizaji. Mzungumzaji hutumia mikakati ambayo hupunguza athari fulani kwenye uso wa msikilizaji. Kwa mfano, kuomba msamaha kabla ya kusema jambo, kusema jambo kwa njia ya kuuliza swali, kujiepusha na kumlazimisha msikilizaji kufanya unachosema au kuafikiana nawe na kujiepusha na kumtaja au kumrejelea msikilizaji katika maneno unayosema. Kwa mfano, “Samahani Juma kwa kukusumbua. Je, unaweza kunianulia kitambaa changu?” Mkakati huu unajiepusha na kuathiri uso wa msikilizaji kwa kutomlazimisha. Daktari anaweza kuwaelekeza wasikilizaji kwa upole hasi kwa njia hii: “Tunaweza kujiepusha na mapenzi ya kiholela’ badala ya kusema kuwa ‘Vijana wajiepushe na kufanya ngono kiholela”. Kauli ya kwanza ina upole kwani inalenga kuokoa uso hasi wa wasikilizaji kwa sababu haijarejelea mtu yeyote au kundi lolote la watu katika jamii; ni kauli ya kijumla.

#### 1.7.2.4. Mkakati wa nje ya rekodi

Mkakati huu unahusu kusema mambo kwa njia fiche. Msikilizaji huachiwa nafasi ya kuamua maana ya ujumbe uliowasilishwa na msemaji. Mkakati huu wa nje ya rekodi huonekana kwenda kinyume na mikakati ya Grice (1975) ya kusema mambo kwa uwazi na yanayoeleweka kwa urahisi.

Mkakati huu hulenga kunusuru uso hasi wa msikilizaji ili usiathirike. Kwa mfano, mzungumzaji anapomwambia rafikiye, “Nimetumia hela nyingi leo”au hata aangalie kwenye mifuko ambayo haina hela huenda akawa anapitisha ujumbe kwa rafikiye kuwa amsaidie hela fulani. Mzungmzaji pia anaweza kutumia nahau kwa kusema kuwa “Amina amepata au amejifungua” badala ya kusema kuwa “Amina amezaa.”

#### 1.7.2.5. Kukosa kuwasilisha

Mkakati huu unahusu kutotoa ishara zozote za kimawasiliano. Hii huweza kuwa na maana kuwa hakuna mawasiliano yoyote ambayo yanaendelea. Kwa mfano, watumiaji lugha katika jamii lugha fulani wanaweza kunyamaza au kujiepusha na kuzungumza kuhusu mambo yanayohusiana na ugonjwa fulani kama vile ukimwi katika jamii lugha kama njia ya kuzuia kuwepo na aibu au tishio kwa waathiriwa au jamii lugha nzima kwa jumla. Hii ni kutokana na uzito wa swala hili hasa kwa kuegemea njia ambazo ugonjwa kama ukimwi husambazwa, sehemu za mwili zinazohusika, uchafu unaotoka mwilini mwa mgonjwa, hali za wagonjwa mbalimbali na matokeo ya ugonjwa huu kwa mwathiriwa, familia na hata jamii lugha nzima.

Nadharia hii imetumika katika uchanganuzi wa data ili kubaini kuwa tasfida zinazotumiwa huonyesha upole wa lugha kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi. Pia, nadharia hii imetumika kuweka wazi mikakati inayotumika katika kuibua tasfida za kimatibabu katika lugha tafitiwa, Kiswahili na Kimarachi. Tumejikita zaidi katika mkakati wa nje ya rekodi au mkakati wa maana fiche, upole hasi, upole chanya na kukosa kuwasilisha.

## 1.8. Yaliyoandikwa kuhusu mada

Herbert (2016) anasema kuwa tasfida ni muhimu na huweza kutumiwa wakati wa kuzungumza na wagonjwa kiasi kwamba wataelekea kuelewa zaidi kuhusu hali ya ugonjwa wao na hata kupunguza uchungu wa kimawazo wanaopitia. Anasema kuwa muuguzi lazima apime kiasi cha uwazi katika mawasiliano akizingatia ujuzi wa mgonjwa na kiasi cha uchungu anaopitia. Anaongeza kuwa matumizi ya tasfida kueleza ugonjwa fulani au hali ya mgonjwa huweza kumpa matumaini ikilinganishwa na matumizi ya lugha ya moja kwa moja kueleza magonjwa au

hali hizo. Kazi hii itatufaa sana kwa sababu inadokeza nafasi ya tasfida katika muktadha wa matibabu kwenye jamii lugha.

Omosa (2015) ameshughulikia tasfida kama mkakati wa upole, uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Amechanganua hali zinazozua matumizi ya tasfida na namna mikakati ya tasfida huendeleza upole katika lugha hizi mbili. Katika uchanganuzi wa kazi yake ameangazia baadhi ya tasfida kuhusu ugonjwa, takamwili, vitendo vya kujamiiana, vifo na hali za watu. Kazi hii itatufaa katika utafiti wetu kwa sababu tunalenga kuangalia tasfida zinazorejelea magonjwa hasa ukimwi, takamwili, hali za watu, sehemu za siri za binadamu na vitendo mbalimbali kama vile kujamiiana. Yaani, tasfida ambazo hutumika katika muktadha wa matibabu kwa kurejelea tiba, utoaji wa ushauri nasaha na uhamasishaji. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu tunalenga kulinganisha na kulinganua tasfida zinazotumika katika muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi na mikakati inayotumiwa kuibua tasfida hizo.

Njoroge (2014) amechunguza tasfida na maneno ambayo ni mwiko katika jamii ya Wakikuyu akizingatia lahaja ya eneo la Kabete. Aliangazia tasfida zinazotumika kutaja takamwili, vifo, maswala yanayohusiana na ngono na magonjwa yanayoenezwa kupitia kwa ngono kama vile ukimwi katika jamii ya Wakikuyu. Kazi hii ni muhimu katika kazi yetu kwa sababu imebainisha tasfida zinazohusiana na magonjwa kama vile ukimwi, takamwili na maswala ya ngono ambayo ni njia mojawapo inayosababisha ugonjwa wa ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu ambao unalenga kulinganisha na kulinganua tasfida za matibabu katika Kiswahili na Kimarachi kwa kuangazia tiba, utoaji wa ushauri nasaha, kuasa na kutahadharisha watu katika maziko kuhusu ugonjwa hatari kama vile ukimwi. Zaidi ya hayo, tunalenga kutumia nadharia mbili katika utafiti wetu kuchanganua data: Nadharia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

Nguti (2013) alitafiti kuhusu ulinganishi wa matumizi ya tasfida za muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili. Katika utafiti wake aliweza kubaini tasfida mbalimbali zinazotumika katika muktadha wa nyumbani. Pia, aliainisha namna umri, jinsia, kazi na hadhi huathiri matumizi ya tasfida katika muktadha wa nyumbani. Utafiti huu ni tofauti na wetu ambao tunalenga kufanya kwa sababu ulilenga ulinganishi wa tasfida za muktadha wa nyumbani katika lugha ya Kikamba na Kiswahili kwa kutumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Nao utafiti wetu unalenga ulinganishi na ulinganuzi wa matumizi ya tasfida katika muktadha wa matibabu katika Kimarachi na Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia mbili; nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Hata hivyo, tasnifu hii itatufaa kwa sababu imeshughulikia swala la tasfida ambalo pia tunalenga kushughulikia katika utafiti wetu hasa kwa kujikita kwenye muktadha wa matibabu.

Njoroge na Mukhwana (2015) wameshughulikia tasfida zinazohusu uchafu unaotoka kwenye mwili wa binadamu katika jamii ya Kikuyu katika jarida lao. Kazi hii itatufaa kwani imeeleza aina mbalimbali za tasfida kuhusu uchafu unaotoka kwenye mwili wa binadamu katika jamii ya Kikuyu, nao utafiti wetu unalenga tasfida za muktadha wa matibabu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi.

Khanfar (2012) ameeleza maana ya tasfida na kuainisha aina za tasfida kama vile tasfida za siasa, dini, ngono na zile zinazohusu utoaji wa uchafu mwilini. Kazi hii itatufaa katika utafiti wetu kwani imegusia aina za tasfida na mifano yake, nao utafiti wetu unahusu ulinganishi na ulinganuzi wa tasfida katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi kwa kujikita katika muktadha wa matibabu.

Tengku na Sepideh (2012) wameandika kuhusu lugha na utamaduni. Wanaeleza kuwa kila mtu anatoka kwenye kundi mahsusi la watu. Yeye huakisi utamaduni wake na ni rahisi kumweka kwenye kikundi fulani na kumtofautisha na watu wengine kulingana na jinsi anavyotumia lugha kimuktadha. Utamaduni hueleweka na mtu kutokana na na maingiliano yake na wengine. Wanamnukuu Rool-Amini (1989) anayesema kuwa mavazi, sayansi, imani na maaadili huunganisha watu wa jamii moja pamoja. Kazi hii ni muhimu katika utafiti wetu kwani inaeleza jinsi lugha huhusiana na utamaduni wa jamii lugha fulani, kipengele ambacho utafiti huu utachunguza hasa tukijikita kwenye tasfida za matibabu ambazo hutumika na watumiaji lugha wa jamii ya Waswahili na Wamarachi ili kudhibiti utamaduni wao.

Wambua (2009) katika utafiti wake kuhusu tofauti ya matumizi ya kilahaja na mitazamo ya kileksia za miiko na tasfida katika jamii ya Kikamba, alitofautisha namna mitazamo tofauti inajitokeza katika matumizi na maana ya kileksika za miiko na tasfida kwa kulinganisha lahaja mbili za Kikamba ambazo ni lahaja ya Kimasaku na ile ya Kitui Kati. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani unarejelea lugha tofauti na zile tunalenga. Hata hivyo, utafiti huu utatufaa kwa sababu umegusia tasfida zinazoambatana na kifo, sehemu za mwili na magonjwa.

Mashiri, P. et al (2002) wanasema kuwa mambo kuhusu kifo, ngono na sehemu za siri za mwili ni mwiko kutaja hadharani katika jamii ya Shona kulingana na dhana kuwa ukimwi ni ugonjwa hatari na huenezwa kupitia kwa ngono na sio swala la kuzungumzia hadharani. Wazungumzaji wa Kishona hubuni kila mara majina yanayokubaliwa na jamii kurejelea ugonjwa huo. Wao hutumia mbinu mbalimbali kama vile istiari na kukopa kutoka kwa lugha zingine kubuni majina hayo. Kazi hii ni muhimu katika uchunguzi wetu kwa sababu imeangazia baadhi ya mikakati ambayo wazungumzaji wa Kishona, kule Zimbabwe hutumia ili kurejelea ugonjwa wa ukimwi kwa njia ya upole. Nao utafiti wetu unanuia kulinganisha na kulinganua tasfida zinazotumika

katika muktadha wa matibabu na mikakati inayotumiwa kuziibua katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi.

## 1.9. Mbinu za utafiti

Utafiti huu umehusu ulinganishi na ulinganuzi wa tasfida za matibabu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi kwa mujibu wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) kwa kujikita katika muktadha wa matibabu.

### 1.9.1. Sampuli na jinsi ya kuipata

Data tuliyokusanya katika utafiti wetu ni kuhusu tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi. Data kuhusu tasfida za matibabu katika lugha ya Kiswahili tumeipata kwa kusoma Kamusi za semi: methali, misemo na nahau na kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI. Tumeshughulikia tasfida ambazo zinahusu magonjwa, sehemu za siri mwilini, matendo ya kutoa taka mwilini, matendo mengine yanayozua aibu, hali za watu, kifo na uchafu unaotoka mwilini mwa binadamu. Tumesoma kamusi za semi: methali, misemo na nahau, kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI na vitabu vingine vilivyoandikwa katika lugha ya Kiswahili huku tukiorodhesha tasfida tulizozipata. Tumechagua vitabu hivi ili kupata tasfida zilizosanifishwa katika lugha ya Kiswahili ambazo tumeorodhesha. Mtafiti pia ametumia ujuzi wake kama mwanafunzi wa Kiswahili kutathmini tasfida husika.

Kwa upande mwingine, data kuhusu tasfida za matibabu katika Kimarachi tumeipata nyanjani kwa kuandaa hojaji na kuwapa watu arobaini tuliowachagua kwa njia ya kimaksudi ambao wanajua kusoma na kuandika kuzijaza. Tumehusisha wazungumzaji wa Kimarachi walio na umri wa miaka kumi na minane na zaidi wakiwemo pia wauguzi, watoaji wa ushauri nasaha,

wahamasishaji na waasaji wa umma kuhusu magonjwa mbalimbali hasa ukimwi kujaza hojaji hizo. Pia, tuliwahoji wazee wachache walio na umri wa miaka sitini na zaidi ambao wanaelewa utamaduni wa Wamarachi na hawajaathirika kwa vyovyote vile na tamaduni za kigeni katika elimu au hata kwenda ng'ambo. Wazee walio na umri kama huo wanaelewa utamaduni wa jamii lugha ya Wamarachi pamoja na tasfida zinazotumiwa kwa wingi kutaja magonjwa, hali za watu, sehemu za siri mwilini, matendo ya kutoa taka mwilini na uchafu unaotoka kwenye mili ya binadamu. Zaidi ya hayo, mahojiano yalitusaidia kupata jumbe zaidi kutoka kwa wahojiwa. Tuliamua kuchunguza data kuhusu tasfida za Kimarachi nyanjani kwa sababu hakuna tasfida zozote katika lugha hii ambazo zimetambuliwa, kusanifishwa na kuorodheshwa kwenye vitabu vya kusoma.

Kutokana na utamaduni wa Wamarachi kuwa mwanaume hafai kuwauliza wanawake maswali yanayohusu hasa sehemu za siri mwilini au mambo yanayowahusu wanawake kwa jumla, mtafiti msaidizi alichaguliwa na kuelekezwa jinsi ya kuuliza maswali watafitiwa wa kike. Hata hivyo, mtafiti mwenyewe aliwahoji wazee wa kiume kwani anaelewa vyema lugha ya Kimarachi.

Kulikuwa na maswali ya ziada pale ambapo wahojiwa walitoa majibu kwenye mahojiano lakini majibu hayo hayakumtosheleza mtafiti. Pia, mtafiti alitumia ujuzi wake kama mzawa wa Kimarachi na mwanafunzi wa Kiswahili kutathmini tasfida zilizotolewa na wahojiwa.

### 1.9.2. Vifaa vya kutumia

Tuliandaa hojaji ambazo tuliwapa watafitiwa wanaojua kusoma na kuandika kujaza. Hojaji hizo zilikuwa na maswali funge na yale ambayo ni wazi.  Maswali wazi humsaidia mtafiti kupata ujumbe zaidi kutoka kwa watafitiwa (Mugenda na Mugenda, 1999). Tuliandaa pia mwongozo

wa maswali ambayo tuliwauliza wazee katika mahojiano hasa wale wenye umri wa mika sitini na zaidi. Tulitumia kalamu na karatasi kunakili chini maoni ya watafitiwa wasiojua kusoma na kuandika, hasa wazee ambao tuliwahoji.

### 1.9.3. Njia za kuchanganua data

Data ambayo tuliipata tumeichanganua kwa njia ya kimaelezo. Tumeipanga data hiyo kwenye majedwali katika makundi mbalimbali ya tasfida za matibabu ambazo zinarejelea magonjwa, uchafu unaotoka katika mwili wa binadamu, hali za watu, sehemu za siri mwilini, matendo yanayohusu utoaji wa taka mwilini, kitendo cha ngono, kitendo cha kuzini na kifo. Tumezipanga tasfida hizo kwa kuzingatia tasfida zinazotumiwa katika tiba na utoaji wa ushauri nasaha kisha zile tasfida ambazo hutumiwa katika uhamasishaji na uasaji wa umma kutokana na shughuli za matibabu ya magonjwa kama vile ukimwi katika Kiswahili na Kimarachi. Pia, tumechunguza mfanano na tofauti zilizopo katika tasfida hizo na mikakati inayotumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili na Kimarachi kuziibua. Hii ni kwa sababu maneno fulani huweza kuwa tasfida katika lugha moja lakini yasiwe tasfida katika lugha nyingine kutokana na kuwepo kwa sheria tofauti za utamaduni katika jamii lugha husika. Data hii imechanganuliwa kwa misingi ya nadharia mbili ambazo ni, nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

# SURA YA PILI

# TASFIDA ZA TIBA NA USHAURI NASAHA

## 2.1. Utangulizi

Matumizi ya tasfida katika tiba na utoaji wa ushauri nasaha ni jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa sana na wahusika kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi. Wengi wa wahusika katika muktadha huu wa matibabu hukosa tasfida mwafaka za kutumia kutajia magonjwa, uchafu na vitendo mablimbali ilhali wengine wakiwemo wauguzi au watoa ushauri nasaha huchelea kutumia tasfida katika muktadha wa matibabu kwa madai kuwa kufanya hivyo kutasababisha ukosefu wa maelewano miongoni mwa wahusika. Hata hivyo, Herbert (2016) anaunga mkono matumizi ya tasfida katika muktadha wa tiba kwani matumizi yake husaidia kupunguza wasiwasi kwa mgonjwa na kumpa matumaini. Jambo la muhimu ni kuwa tasfida hizo zitumiwe kwa njia itakayoleta uwazi na uelewano katika mazungumzo. Dai la Herbert, ambaye ni muuguzi, lina nguvu kwani matumizi ya tasfida katika tiba na ushauri nasaha huweza kuwa kitulizo kikubwa kwa mgonjwa au mwathiriwa kwa kujenga picha chanya kuhusu shida anayopitia.

## 2.2. Tasfida za Tiba na Ushauri Nasaha

Wauguzi na watoa ushauri nasaha wanapaswa kuteua na kutumia lugha ambayo haina makali kwa wagonjwa na washauriwa. Kwa upande mwingine, wagonjwa au watafutaji wa ushauri kuhusu maswala ya kiafya wanastahili kutumia lugha ambayo haizui aibu, kero au kuvunja kanuni za utamaduni wa jamii lugha husika. Herbert (2016) anaeleza kuwa tasfida ni muhimu na huweza kutumiwa wakati wa kuzungumza na wagonjwa kiasi kwamba wataelekea kuelewa zaidi

kuhusu hali ya ugonjwa wao na hata kupunguza uchungu wa kimawazo wanaopitia. Anaongeza kuwa matumizi ya tasfida kueleza ugonjwa fulani au hali ya mgonjwa huweza kumpa matumaini ikilinganishwa na matumizi ya lugha ya moja kwa moja kueleza magonjwa au hali fulani.

Watoa ushauri nasaha pia huhitajika kutumia lugha ya upole ili kuteka hisia za washauriwa. Hali hii itaibua mawasiliano bila woga au kero na kumpa mtoaji wa ushauri nasaha nafasi bora ya kumwelekeza mteja wake vyema. Aghalabu wauguzi au watoa ushauri nasaha hutangamana na wagonjwa au waathiriwa wa magonjwa fulani hatari ili kuwapa tiba au ushauri kwa lengo la kupunguza maumivu mwilini, kuwapa matumaini au kuwaelekeza namna ya kuishi na kukabiliana na changamoto zinazowasonga katika jamii lugha wanamoishi.

Wajnryb (2005) anasema kuwa kuna mada za mazungumzo ambazo husheheni lugha chafu ambayo haifai kutumiwa au kutajwa mbele ya watu. Mada hizi zinahusu kazi za viungo fulani mwilini na takamwili. Mifano ya maneno yanayohusisha lugha mbaya ni *mavi*, *kujamiiana*, *manii* na *damu.*

Tasfida zifuatazo hutumika sana katika tiba na ushauri nasaha:

### 2.2.1. Tasfida za Kutaja Magonjwa

Binadamu wengi huogopa kutaja au kusikia magonjwa fulani yakitajwa. Hii ni kwa sababu majina ya magonjwa hayo huwafanya watu kuanza kufikiria kuhusu kifo, hali ambayo huwatia hofu kuwa wao hasa waathiriwa huenda wakaaga dunia punde. Zaidi ya hayo, kutaja magonjwa hatari moja kwa moja bila kutumia tasfida huweza kuwaongezea wagonjwa uchungu na kufanya hata hali zao kuwa mbaya zaidi kulingana na (Herbert, 2016). Ili kujiepusha na matatizo kama hayo, wauguzi na hata watoaji wa ushauri nasaha wanastahili kutumia msamiati wa upole ili kutaja au kueleza kuhusu magonjwa ambayo huzua tishio kwa wagonjwa wao. Kwa mfano,

ugonjwa wa ukimwi huwa tishio kubwa sana katika jamii lugha yoyote mara tu unapotajwa mbele ya watu. Hii ni kwa sababu ugonjwa huo hutazamwa kama janga kubwa linaloweza kuwaangamiza watu wengi katika familia au jamii kwa upana kwani mtu yeyote anayepatikana na ugonjwa wa ukimwi huhusishwa na kifo ambacho wengi huogopa. Baadhi ya watu wanaougua ugonjwa wa ukimwi huona aibu kujitambulisha hadharani kutokana na aibu inayoweza kuwaandama na hata kwa jamii lugha nzima. Kutokana na hali hii, maneno ya upole yaliyokamaa kimatumizi hutumiwa na watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi kurejelea ugonjwa huo na baadhi ya magonjwa mengine.  Tumetambua katika utafiti wetu kuwa tasfida zifuatazo hutumiwa kutajia magonjwa mbalimbali katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu.

**Mifano :** **KISWAHILI**

**Jedwali la 1A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 1 | Ukimwi | Ugonjwa mkubwa<br>Mdudu |
| 2 | Kaswende/ Tego | Maumivu kwenye tupu ya mbele<br>Ugonjwa wa wanawake<br>Matatizo ya kwenda haja ndogo<br>Kuungua |
| 3 | Kisonono | Maumivu kwenye tupu ya mbele<br>Matatizo ya kwenda haja ndogo<br>Kuungua |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Kansa/ Saratani | Ugonjwa wa uvimbe<br><br>Uvimbe |
| 5 | Bawasiri | Ugonjwa wa tupu ya nyuma |
| 6 | Kuhara | Kuendesha<br><br>Kutoa haja kubwa nyepesi |
| 7 | Kifua kikuu | Shida ya kupumua<br><br>Matatizo ya kifua |
| 8 | Shinikizo la damu | Ugonjwa wa mawazo<br><br>Tatizo la damu kwenda haraka mwilini |
| 9 | Ugonjwa wa moyo | Ugonjwa wa mawazo |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 1B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Obulwaye** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 10 | Vukimu | Obulwaye bukhongo<br><br>Bulwaye bwefwe<br><br>Siranda<br><br>Lubukha | Ukimwi | Ugonjwa mkubwa<br><br>Ugonjwa wetu<br><br>Mtu aliyekonda sana<br><br>Mdudu |
| 11 | Kaswende | Bulwaye bwa imberi | Kaswende | Ugonjwa wa tupu ya mbele |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Bulwaye bwa abakhasi<br>Idakanyi | | Ugonjwa wa wanawake<br>Ugonjwa wa zinaa |
| 12 | Gonoria | Bulwaye bwa bakhasi<br>Bulwaye bwa imberi<br>Idakanyi | Kisonono | Ugonjwa wa wanawake<br>Ugonjwa wa tupu ya mbele<br>Ugonjwa wa zinaa |
| 13 | Saratani/ Kansa | Obufwimbe | Kansa | Uvimbe |
| 14 | Bulwaye bwa munie | Mkongo khuvula | Bawasiri | Shida kwenye tupu ya nyuma |
| 15 | Khunyalala | Khwetsira<br>Khurusia ihaja ikhongo inyangu<br>Khudatsa<br>Khwechuka | Kuhara | Kujiendea/ Kuendesha<br>Kutoa haja kubwa nyepesi<br>Kuvuja<br>Kujiendea haja kubwa nyepesi |
| 16 | Bulwaye bwa esirifu | Siyera | Kifua kikuu | Shida ya kupumua |
| 17 | Bulwaye bwa ipresha | Bulwaye bwa maparo | Shinikizo la damu | Ugonjwa wa mawazo |
| 18 | Bulwaye bwa omwoyo | Bulwaye bwa amaparo | Ugonjwa wa moyo | Ugonjwa wa mawazo |

Tumebaini katika utafiti huu kuwa magonjwa fulani yanapotajwa mbele ya hadhira lengwa katika muktadha wa matibabu hasa tiba na utoaji wa ushauri nasaha bila kutumia tasfida

ipasavyo huzua tishio, wasiwasi na aibu kwa wahusika. Huenda hata mgonjwa akapoteza matumaini. Kwa mfano, wanajamii wengi Afrika wanaposikia neno *ukimwi* wao hulihusisha na kifo. Kwa hivyo, mtu yeyote anayetajwa kuwa na ukimwi huonwa kama mfu tayari ambapo hali hii huwafanya watu wengine katika jamii kujitenga naye.

Watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi huibua maneno ya upole ambayo hutumiwa kurejelea magonjwa yenye kutisha au kuleta aibu mbele ya watu hasa katika muktadha wa matibabu. Hali hii ya kutumia tasfida kutajia ugonjwa wa ukimwi husaidia kupunguza tishio, aibu au fikra mbaya hasa miongoni mwa waathiriwa na hata kuwapa matumaini fulani. Kwa mfano, ugonjwa wa ukimwi hurejelewa kwa upole *ugonjwa mkubwa* na *mdudu* katika Kiswahili na *bulwaye bukhongo* (ugonjwa mkubwa), *bulwaye bwefwe* (ugonjwa wetu), *siranda* (mtu aliyekonda) na *lubukha* (mdudu) katika Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuondoa hofu kuwa mtu fulani ana ugonjwa huo. Kuepuka kutaja neno *ukimwi* humfanya mwathiriwa yeyote kuwa na matumaini kwamba ugonjwa alionao ni mkubwa au wa kawaida tu na unaweza kuisha. Hatua hii husaidia kwa kiasi fulani kufanikisha lengo la muuguzi au mtoa ushauri nasaha ambalo ni kutoa matibabu kwani mwathiriwa ataweza kumsikiliza na kutekeleza maagizo ya kimatibabu anayopewa.

Kaswende na kisonono ni magonjwa ambayo mtu hupata kutokana na kujihusisha kimapenzi na mtu anayeugua magonjwa hayo. Mara nyingi waathiriwa huona aibu kutaja mbele ya muuguzi au mshauri kuwa wanaugua ugonjwa wa kaswende au kisonono hasa kutokana na njia ambayo magonjwa hayo husambazwa. Kwa hivyo, watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi hutumia maelezo yenye maana fiche kurejelea ugonjwa wa kaswende na kisonono ili kupunguza aibu. Kwa mfano, maelezo *ugonjwa wa wanawake*, *matatizo kwenye tupu ya mbele*, *matatizo ya kwenda haja ndogo au kuungua* hutumiwa kama njia ya upole kurejelea ugonjwa wa kaswende

na kisonono katika Kiswahili. Kwa upande mwingine, magonjwa haya hurejelewa kwa upole *bulwaye bwa bakhasi* (ugonjwa wa wanawake), *bulwaye bwa imberi* (ugonjwa wa tupu ya mbele) au *idakanyi* (ugonjwa wa zinaa) katika Kimarachi. Ugonjwa wa kaswende na kisonono hurejelewa kwa njia ya upole kama *ugonjwa wa wanawake* katika Kiswahili na *bulwaye bwa bakhasi* (ugonjwa wa wanawake) katika Kimarachi kwa sababu aghalabu mtu huupata kwa kufanya mapenzi kiholela na wanawake wanaougua ugonjwa huo. Isitoshe, huitwa *bulwaye bwa imberi* (ugonjwa wa tupu ya mbele) kutokana na hali kuwa kaswende na kisonono huathiri sana tupu ya mbele ya mwanamume au mwanamke.

*Saratani au kansa* ni ugonjwa ambao pia huwaogofya watu wengi hasa unapotajwa. Mgonjwa yeyote anayeugua saratani husongwa na mawazo mengi pamoja na uchungu zaidi anapoambiwa mara ya kwanza na daktari kuwa anaugua ugonjwa huo. Kama njia ya kuondoa au kupunguza woga na wasiwasi, daktari huweza kumweleza mgonjwa wake kuwa *ana uvimbe* mwilini katika Kiswahili au *ali nende obufwimbe* (ana uvimbe) katika Kimarachi ili kuonyesha upole. Hii ni kwa sababu ugonjwa wa saratani husababisha uvimbe kwenye sehemu au seli fulani mwilini.

Ugonjwa wa bawasiri huathiri tupu ya nyuma ya binadamu. Ugonjwa huu husababisha kufura kwa tupu ya nyuma ya binadamu na hata kutokwa na damu. Kulingana na aibu ambayo mwathiriwa huona, yeye hujiepusha na kuutaja ugonjwa huo moja kwa moja mbele ya muuguzi au mshauri anapotafuta matibabu. Tasfida *shida kwenye tupu* ya nyuma hutumiwa ili kuonyesha upole katika Kiswahili ambayo ni sawa na *omukongo khuvula* (matatizo kwenye tupu ya nyuma) katika Kimarachi. Mtumiaji wa Kiswahili au Kimarachi atakuwa amezingatia na kuheshimu utamaduni unaomhitaji kutumia lugha kwa njia ya upole isiyozua aibu hasa katika muktadha wa matibabu.

Ugonjwa wa *kuhara* hutajwa kwa upole kwa kutumia tasfida *kuendesha* au *kutoa haja kubwa nyepesi* ili kupunguza aibu na kero kwa msikilizaji katika Kiswahili. Watumiaji wa Kimarachi pia husema *khwetsira* (kujiendea) au *khurusia ihaja ikhongo inyangu* (kutoa haja kubwa nyepesi) badala ya kutumia neno *khunyalala* (kuhara). Kuendesha ni hali inayofahamika na kila mtu kuwa ni kuchukua usukani kwenye gari, pikipiki au baiskeli. Vyombo hivi pia hutoa sauti fulani hasa vinapokimbia. Kwa hivyo, tendo la kuhara hulinganishwa na hali hii ya kuendesha gari kama njia ya kuonyesha upole. Ugonjwa wa kifua kikuu, shinikizo la damu na ugonjwa wa moyo pia hurejelewa kwa tasfida tulizoorodhesha kwenye jedwali la **1A** na **1B** ili kuonyesha upole.

Tasfida zinazorejelea hasa magonjwa hatari kama vile ukimwi huteuliwa na kutumiwa ili kumzuia mgonjwa kupokea habari mbaya inayoweza kumwongezea kiwango cha maumivu na hata kumfanya apoteze matumaini. Harbert (2016) anasema kuwa utamaduni husika huweza kuwa na athari katika aina ya lugha inayotumiwa kueleza ugonjwa fulani hatari. Kwa mfano, utafiti huu umebaini kuwa ingawa kuna tasfida zinazofanana za kutajia ugonjwa wa ukimwi katika Kiswahili na Kimarachi, kuna tasfida *bulwaye bwefwe (ugonjwa wetu)* na *siranda (mtu aliyekonda sana)* ambazo hutumiwa na kueleweka katika Kimarachi lakini hazitumiki katika Kiswahili. Hii huenda ikawa kwa sababu watumiaji wa Kimarachi wanaweza kuelewa vyema tasfida hizo zinapotajwa kwani zinakubaliwa na utamaduni wao. Kulingana na Hymes (1974) maneno fulani huweza kuwa tasfida katika jamii lugha moja lakini yasiwe tasfida katika jamii lugha nyingine.

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, ni idhahiri kuwa tasfida zinazotumiwa kutajia magonjwa mengi kama vile ukimwi, kaswende, kisonono, saratani, bawasiri, ugonjwa wa kuhara, kifua kikuu, shinikizo la damu na ugonjwa wa moyo katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu zinafanana pakubwa.

### 2.2.2. Tasfida za Kutaja Takamwili

Mtu yeyote katika jamii lugha husika hapendi kusikia au kutaja hadharani baadhi ya taka ambazo hutoka katika mwili wa binadamu. Hii ni kwa sababu taka hizo zikitajwa moja kwa moja huweza kuwaudhi, kuzua aibu au hata kuvunja kanuni za jamii zinazomtarajia kila mwanajamii kutumia lugha ya upole katika mazungumzo. Hymes (1974) anasema kuwa kila jamii huwa na sheria za lugha ambazo hufuatwa na watumiaji lugha katika jamii lugha hiyo.

Takamwili kama vile matapishi, damu, kamasi, usaha na zile zinazohusiana na maswala ya kingono huhusika pakubwa katika usambazaji wa magonjwa mbalimbali kutoka kwenye mwili wa mtu mmoja hadi mwingine (Njoroge na Mukhwana, 2015). Kwa mfano, damu na taka zinazohusiana na maswala ya kingono huweza husababisha uenezaji wa magonjwa kama vile ukimwi na homa ya manjano aina ya B na C.  Pia, homa ya manjano aina ya A na E huweza kusambazwa na kinyesi cha mtu anayeugua ugonjwa huo. Kwa hivyo, iwapo mtumiaji lugha husika atataja taka hizi moja kwa moja bila kutumia tasfida au lugha ya upole, huenda akawakasirisha, akawatisha au kuwaudhi wasikilizaji na hata kuonyesha kutokuwepo kwa heshima.

Allan na Burridge (2006) wanaeleza kuwa iwapo takamwili zitatajwa moja kwa moja huwa chanzo cha aibu na wale wanaosikiliza huweza kuona kama matusi kwao. Mgonjwa au mshauriwa huweza kuogopa kutaja baadhi ya taka hizi hasa zile zinazohusika na maswala ya kingono mbele ya muuguzi au mshauri, hali ambayo huenda ikatatiza matibabu mwafaka kutolewa. Hata hivyo, matibabu yafaayo yatatolewa na muuguzi au mtoa ushauri nasaha ikiwa waathiriwa wanaelewa vyema tasfida hasa zile komavu ambazo hutumika kurejelea takamwili kwa njia ya upole.

**Mifano :** **KISWAHILI**

**Jedwali la 2A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 19 | Mavi | Haja kubwa<br>Haja ndefu<br>Kinyesi |
| 20 | Mkojo | Haja ndogo<br>Haja fupi |
| 21 | Manii | Mbegu za uzazi<br>Nguvu za uume<br>Maji ya uzazi<br>Mbegu za mwanamume<br>Nguvu za mwanamume |
| 22 | Damu | Ngeu |
| 23 | Usaha | Uchafu wa kidonda |
| 24 | Kamasi | Uchafu unaotoka puani |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 2B**

| | | | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| **Likhuwa** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 25 | Mafwi | Ihaja ikhongo<br>Ihaja indambi<br>Obunyaka | Mafi | Haja kubwa<br>Haja ndefu<br>Kinyesi |
| 26 | Manyi | Ihaja indidi<br>Amatsi<br>Ihaja inyimbikiri | Mkojo | Haja ndogo<br>Maji<br>Haja fupi |
| 27 | Spamu | Imbegu ya ubwibusi<br>Obusatsa<br>Lwibulo lusatsa<br>Lwibulo lwa omusatsa<br>Amani ka omusatsa | Manii | Mbegu ya uzazi<br>Uume<br>Uzazi uume<br>Uzazi wa mwanamume<br>Nguvu za mwanamume |
| 28 | Mavanga | Malasire<br>Matsai | Damu | Damu<br>Damu |
| 29 | Mafiria | Masera<br>Obuchafu bwa esikonzo | Usaha | Uchafu unaotoka kwenye kidonda<br>Uchafu wa kidonda |
| 30 | Mamira | Sivove | Kamasi | Uchafu wa puani |

Utafiti huu umebaini kuwa uchafu utokao mwilini kama vile *mavi* na *mkojo* haufai kutajwa ovyo ovyo katika muktadha wa matibabu. Watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi wanazo tasfida amabazo hutumia kutajia uchafu huo. Tasfida *haja kubwa*, *haja ndefu* na *kinyesi* hutumiwa sana katika Kiswahili ili kuonyesha upole badala ya kusema *mavi*. Kwa upande mwingine, tasfida *ikhaja ikhongo* (haja kubwa) na *bunyaka* (kinyesi) hutumiwa katika Kimarachi badala ya kusema *mafwi* (mavi). Kwa mfano, mgonjwa anapomweleza muuguzi kuwa *"haja kubwa yangu ni ngumu'* huonyesha upole kuliko kusema *'mavi yangu ni ngumu'* katika Kiswahili au *'mafwi kanje ni momu'* (mavi yangu ni ngumu) katika Kimarachi.

Neno *mkojo* nalo hurejelewa kwa tasfida *haja fupi* au *haja ndogo* katika Kiswahili na *ikhaja inyimbikiri* (haja fupi) au a*matsi* (maji) katika Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu. Tasfida *haja fupi* hutumiwa katika Kiswahili na Kimarachi kwa sababu uchafu huu aghalabu huchukua muda mfupi kutolewa mwilini. Katika Kimarachi, neno *amatsi* (maji) hutumiwa kurejelea mkojo kwa sababu takamwili hii hufanana na maji. Neno *amatsi (maji)* haliwezi kuzua aibu au kero hasa linapotajwa mbele ya watu. Sababu kuu ya kutumia tasfida hizi huwa kuonyesha upole au heshima miongoni mwa wahusika kulingana na sheria za utamaduni wa jamii lugha husika. Tasfida zinazotumiwa kurejelea mavi na mkojo katika Kiswahili na Kimarachi katika muktadha wa matibabu hasa tiba na ushauri nasaha zinafanana pakubwa kulingana na mifano tuliyopata na kuorodhesha. Hata hivyo, neno *matsi* (maji) ambalo hutumiwa kama tasfida ya kurejelea *manyi* (mkojo) katika Kimarachi halitambuliki kama tasfida ya kurejelea mkojo katika Kiswahili kwani huchukuliwa tu kama neno la kawaida. Hii ni kutokana na tofauti zilizoko katika sheria zinazodhibiti utamaduni wa watumiaji lugha husika; kwani neno fulani huweza kutumiwa kama tasfida katika lugha moja lakini lisiwe tasfida katika lugha nyingine kulingana na nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Hymes (1974).

Sheria za kitamaduni haziruhusu kutaja kiholela uchafu unaotokana na kitendo cha ngono. Hili hupelekea wanajamii hasa wauguzi, watoa ushauri nasaha na watumiaji wengine wa lugha husika kubuni tasfida nyingi ambazo huwawawezesha kuzungumzia mambo haya katika muktadha wa matibabu bila kuzua kero au aibu miongoni mwa walengwa. Kwa hivyo, tasfida *mbegu za uzazi, nguvu za uume, maji ya uzazi, mbegu za mwanamume* na *nguvu za mwanamume* hutumiwa badala ya *manii* katika Kiswahili kwenye muktadha wa matibabu hasa tiba na ushauri nasaha. Kwa upande mwingine, tasfida *imbegu ya obwibusi* (mbegu ya uzazi), *obusatsa* (uume), *olwibulo lusatsa* (uzazi uume), *lwibulo lwa omusatsa* (uzazi wa mwanamume) na *amani ka omusatsa* (nguvu za mwanamume) hutumiwa katika Kimarachi kuonyesha upole.

Tumebaini katika utafiti wetu kuwa *usaha* na *kamasi* pia huwa na tasfida za kutajia katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole katika lugha. Tasfida nyingi ambazo hutumiwa kutajia takamwili kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi zinafanana. Kwa mfano, tasfida za kutajia *mavi, mkojo* na *manii, usaha* na *kamasi* katika Kiswahili na Kimarachi zinafanana pakubwa jinsi inavyojitokeza katika data tuliopata na kuorodhesha.

### 2.2.3. Tasfida za Kutaja Vitendo vya Kutoa Takamwili

Vitendo vya kutoa taka mwilini mara nyingi havistahili kutajwa moja kwa moja hadharani. Taka mwili mbalimbali ambazo tumekwisha kuzitaja na kueleza hutolewa mwilini kupitia kwa vitendo hivi. Vitendo mbalimbali vinavyohusu utoaji wa takamwili huleta picha hasi kwa wasikilizaji ambayo huwaudhi, huwachafua roho au kuwakera. Baadhi ya wagonjwa au washauriwa wanaotafuta matibabu zahanatini au hospitalini huweza kuwa na shida kuhusu utoaji wa taka fulani mwilini au kutoa taka ambazo si za kawaida kulingana na hali za miili yao au magonjwa

wanayougua. Kwa hivyo, ili kudumisha mawasiliano kati yao na wauguzi na kuonyesha upole, lazima tasfida zitumike kwa makini ili kila mhusika asiwe na haya au kukerwa.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 3A**

| Neno | | Tasfida |
|---|---|---|
| 31 | Kunya | Kutoa haja kubwa<br>Kwenda haja ndefu<br>Kujisaidia<br>Kwenda msalani |
| 32 | Kuhara | Kuendesha<br>Kutoa haja kubwa yenye maji maji<br>Kwenda haja ndefu yenye maji maji |
| 33 | Kukojoa | Kutoa haja ndogo<br>Kwenda haja fupi<br>Kujisaidia<br>Kwenda pembeni<br>Kwenda msalani |
| 34 | Kutoa manii | Kutoa mbegu za uzazi<br>Kutoa uume<br>Kutoa nguvu za uume<br>Kutoa maji ya uzazi uume<br>Kushusha |
| 35 | Kutokwa na damu<br>(mwanamke) | Kupata hedhi<br>Kuona mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kuingia mwezini<br>Kutembelewa na mgeni |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 3B**

| Likhuwa | | Injira ya ovupole | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **Neno** | **Tafsida** |
| 36 | Khunia | Khurusia ihaja ikhongo<br>Khwekhonya kukhongo<br>Khutsia rwanyi | Kunia | Kutoa haja kubwa<br>Kujisaidia kukubwa<br>Kwenda nje |
| 37 | Khunyalala | Khubisia<br>Khwetsira | Kuhara | Kupitisha<br>Kujiendea |
| 38 | Khwinyala | Khutsia kando<br>Khutsukha amatsi<br>Khwekhonya khutiti | Kukojoa | Kwenda kando/ pembeni<br>Kumwaga maji<br>Kujisaidia kudogo |
| 39 | Khurusia<br>spamu | Khurusia obusatsa<br>Khurusia amani ka olusatsa<br>Khurusia imbegu ya obwibusi | Kutoa manii | Kutoa uume<br>Kutoa nguvu za uume<br>Kutoa mbegu ya uzazi |
| 40 | Kudatsa mavanga (mukhasi) | Khulola omwosi<br>Khuba khumwosi<br>Khukenderwa nende omukeni | Mwanamke kutokwa na damu | Kuona mwezi<br>Kuwa kwenye mwezi<br>Kutembelewa na mgeni |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Khudatsa | | Kuvuja |

Kitendo cha *kunya* hurejelewa kwa upole katika Kiswahili kama *kutoa haja kubwa*, *kwenda haja ndefu* au *kwenda msalani* ilhali tasfida *khurusia ihaja ikhongo* (kutoa haja kubwa), *khwekhonya khukhongo* (kujisaidia kukubwa) na *khutsia rwanyi* (kwenda nje) hutumiwa sana kutajia kitendo *khunia* (kunya) katika Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole katika lugha. Ni kutokana na muda ambao mhusika huchukua kutoa taka hizi pamoja na kiasi cha taka anayotoa mwilini ndipo tasfida *kwenda haja ndefu* na *kutoa haja kubwa* katika Kiswahili na *khutsia ikhaja indambi* (kwenda haja ndefu) *na khurusia ikhaja ikhongo* (kutoa haja kubwa) katika Kimarachi hutumiwa ili kuficha aibu au kero miongoni mwa wahusika katika muktadha wa matibabu. Tasfida *khutsia rwanyi* (kwenda nje) hutumiwa katika Kimarachi kwa sababu mtu huhitajika kutoka mahali ambapo watu wapo na kujificha hasa msalani ambamo tendo hilo hutekelezwa. Kwa mfano, mgonjwa anaposema kuwa *'ndolanga ishida ninzia rwanyi'* kwa maana ya *'mimi huona shida nikienda nje'* atakuwa amezingatia lugha ya upole kulingana na sheira za utamaduni wa jamii lugha ya Wamarachi badala ya kusema *'ndolanga ishida ninzia khunia'* kwa maana ya *'mimi huona shida nikienda kunya'*.

Mgonjwa fulani hasa yule anayeugua ukimwi au aliye na matatizo ya tumbo huwa na dalili kama vile kutoa haja kubwa yenye maji maji. Kuhara huzua aibu hasa kwa mgonjwa mwenyewe na huenda asiwe na ukakamavu wa kutaja mbele ya muuguzi iwapo hatapata tasfida ya kusemea. Kulingana na juhudi za kila mwanajamii yeyote kudumisha utamaduni wao, ni lazima kila mtumizi wa lugha husika ateue kwa makini msamiati unaotumia kusemea jambo fulani. Badala

ya mtu kusema kuwa *'anahara'* yeye anastahili kusema kuwa *'anaendesha'* au *'anatoa haja kubwa yenye maji maji'* katika lugha ya Kiswahili. Neno *kuendesha* hutumika kutokana na kasi ambayo taka husika hutoka mwilini pamoja na sauti kama ya mngurumo wa gari inayosikika wakati wa kutoa taka ya aina hii. Kwa upande mwingine, mgonjwa aliye na shida ya kuhara husema kuwa *yetsira* (anajiendea) au *avisia* (anapitisha) katika Kimarachi. Neno *yetsira* (anajiendea) au *avisia* (anapitisha) hutumika kutokana na hali kuwa mgonjwa aliye na shida ya aina hii wakati mwingine huweza kujichafua bila kutarajia au kupitisha uchafu husika bila kujua. Mgonjwa pia huweza kushindwa kuzuia kutoa taka hiyo hata akiwa kwenye umati wa watu. Kwa hivyo, maneno *kuhara* katika Kiswahili na *khunyalala* (kuhara) katika Kimarachi hayastahili kutumika katika muktadha wa matibabu mbele ya muuguzi au mshauri ili kupunguza aibu na kero kwa wahusika.

Kitendo cha kutoa manii huhusisha hali ya uzazi ambayo kulingana na tamaduni za jamii lugha nyingi hakifai kuzungumziwa hadharani. Hata hivyo, iwapo kitasemwa, lazima tasfida ziteuliwe na kutumika ili kupunguza aibu na chukizo miongoni mwa watumiaji wa lugha husika. Mazungumzo kati ya muuguzi au mtoa ushauri nasaha na mteja wake huweza kutatizika iwapo wahusika hawana msamiati wa upole wa kutumia kutajia kitendo kama hiki. Zaidi ya hayo, mgonjwa au mshauriwa huweza kukosa matibabu kikamilifu kulingana na ukosefu wa maelewano kutokana na kuogopa kutaja kitendo cha kutoa manii au mzungumzaji mmoja kutaja msamiati wa upole ambao mwenzake haelewi maana. Kwa mfano, badala ya muuguzi au mgonjwa kusema *kutoa manii* anaweza kusema *kutoa mbegu za uzazi, kutoa nguvu za mwanamume* au *kushusha* katika Kiswahili ili kuonyesha upole. Watumiaji wa Kimarachi hutumia tasfida *khurusia obusatsa* (kutoa uume) au *khurusia imbegu ya obwibusi* (kutoa mbegu ya uzazi) ili kuonyesha upole katika muktadha wa matibabu. Ni bayana kuwa tasfida

zinazotumika kutajia kitendo cha mwanamume kutoa manii katika Kiswahili na Kimarachi zinaelekeana pakubwa.

Tendo la mwanamke kuona damu hurejelewa kwa njia ya upole kama *kuona mwezi, kupata hedhi, kuwa katika mwezi* au *kutembelewa na mgeni* katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, kitendo hiki pia hurejelewa kwa upole kama *khulola mwosi* (kuona mwezi), *khuba khumwosi* (kuwa katika mwezi), *khukenderwa nende omukeni* (kutembelewa na mgeni) na *khudatsa* (kuvuja) katika lugha ya Kimarachi. Mwezi huonekana kwa wakati fulani na kisha kutoweka sawa na mgeni ambaye huja wakati fulani kwa kutarajiwa au bila kutarajiwa na hatimaye akaondoka. Kwa hivyo, kitendo hiki cha mwanamke kutokwa na damu kwenye sehemu yake ya uzazi hufananishwa na hali ya mwezi kuonekana au mgeni kumtembelea mwenyeji katika Kiswahili na Kimarachi kutokana na dhana kuwa kitendo hicho huonekana tu kwa wakati fulani na kisha kutoweka tena. Kitendo cha mwanamke kuona damu hurejelewa kwa tasfida mbalimbali ambazo tumetaja ili kuondoa aibu inayoweza kumwandama mwanamke hasa inapojulikana kuwa anakishuhudia au amekishuhudia. Tasfida zinazotumiwa kutajia kitendo cha msichana kuona damu pia zinafanana pakubwa katika Kiswahili na Kimarachi.

### 2.2.4. Tasfida za Kutaja Sehemu za Siri Mwilini

Sehemu fulani katika mwili wa binadamu hazistahili kutajwa ovyo ovyo mbele ya watu kulingana na tamaduni za jamii lugha nyingi zikiwemo jamii lugha za Waswahili na Wamarachi. Sehemu hizi hujulikana kama sehemu za siri kwa sababu kila mara zinastahili kufunikwa au kusitiriwa kwa mavazi ifaavyo hasa kulingana na utamaduni wa jamii lugha nyingi za Kiafrika. Mara nyingi sehemu zinazorejelewa kuwa za siri kwenye mwili wa binadamu ni zile zinazohusika katika utoaji wa taka mwilini na zile za uzazi. Hata hivyo, sehemu hizi za siri ndio

hukumbwa na magonjwa ya zinaa kama vile ukimwi, kaswende, kisonono na mengine yasiyo ya zinaa kama vile bawasiri. Mtu yeyote aliye na matatizo katika sehemu yake ya siri atakuwa na ujasiri wa kuelezea hali yake ikiwa anajua neno au maneno mwafaka ya upole ambayo atatumia. Hali hii husaidia katika kutimiza matibabu kwani muuguzi au mtoa ushauri nasaha huweza kutoa matibabu kikamilifu na yaliyo bora.

**Mifano : KISWAHILI**

**Jedwali la 4A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 41 | Mboo/ Mboro | Tupu ya mbele ya mwanamume<br>Uume |
| 42 | Makende | Stoo ya uume |
| 43 | Kuma | Tupu ya mbele ya mwanamke<br>Uuke |
| 44 | Mkundu | Tupu ya nyuma<br>Kinyeo |
| 45 | Matako | Makalio |
| 46 | Matiti | Chuchu |
| 47 | Mavuzi | Nywele zinazomea kwenye sehemu za siri |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 4B**

| | | | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Ingira ya vupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 48 | Imbolo | Imberi wa omusasta<br>Lusatsa | Mboro | Mbele ya mwanamume<br>Uume |
| 49 | Maneke | Maladiro<br>Mangu'su<br>Bubishiro bwa amani ka omusatsa | Makende | Sehemu ya uume<br>Sehemu ya uume<br>Hifadhi ya nguvu za mwanamume |
| 50 | Lwena | Imberi ya umukhasi | Kuma | Mbele ya mwanamke |
| 51 | Munie | Inyuma<br>Siniero | Mkundu | Nyuma<br>Kinyeo |
| 52 | Madakho | Bwikhaliro | Matako | Makalio |
| 53 | Tsimbere | Tsinuniro<br>Amakina<br>Ichapati | Matiti | Chuchu<br>Mawe<br>Chapati |
| 54 | Vwoya | Bunabwori<br>Liswiri lya emwalo | Mavusi | Aina ya nyasi<br>Nywele za chini |

Kulingana na utafiti huu, tasfida nyingi zimebuniwa ili kutumiwa kutajia sehemu za siri mwilini katika muktadha wa matibabu. Kwa mfano, sehemu ya uzazi ya mwanamume huitwa *tupu ya mbele ya mwanamume* au *uume* badala ya *mboo* ilhali ile ya mwanamke hurejelewa kama *tupu*

*ya mbele ya mwanamke* au *uuke* katika Kiswahili badala ya neno *kuma* ili kuonyesha upole katika muktadha wa matibabu. Tasfida *imberi ya musatsa* (mbele ya mwanamume) nayo hutumiwa katika Kimarachi kurejelea sehemu ya uzazi ya mwanamume ilhali sehemu ya siri ya mwanamke huitwa *imberi ya omukhasi* (mbele ya mwanamke) ili kuonyesha upole. Majina haya yanatokana na dhana kuwa sehemu hizi zinapatikana kwenye sehemu ya mbele ya binadamu na ndio humtambulisha mwanamume na mwanamke kibiolojia kando na kuhusika sana katika maswala ya uzazi. Imebainika kuwa tasfida zinazotumiwa kurejelea sehemu za uzazi katika Kiswahili na Kimarachi zinafanana pakubwa.

Neno *makende* linapotumiwa kurejelea sehemu ya siri ya mwanamume huzua aibu na kero miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi. Neno hili hurejelewa kama *stoo ya uume* katika Kiswahili na *bubishiro bwa amani ka omusatsa* (hifadhi ya nguvu za uume) katika Kimarachi. Maneno *stoo* katika Kiswahili na *bubishiro* (hifadhi) katika Kimarachi hayawezi kuzua aibu na hutumiwa kurejelea mahali maalum pa kuweka au kuhifadhi vitu fulani. Kwa hivyo, neno *makende* hurejelewa kwa upole *stoo ya uume* katika Kiswahili au *bubishiro bwa amani ka omusatsa* katika Kimarachi kutokana na hali kwamba sehemu hiyo ndiyo huweka au huhifadhi mbegu za uzazi wa mwanamume. Sehemu hiyo hurejelewa jinsi tulivyoeleza katika muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole na kuondoa aibu kati ya muuguzi na mgonjwa au mshauriwa na mshauri. Jambo hili husaidia kufanikisha matibabu kwa wahusika.

Sehemu inayotumika kutoa kinyesi kwenye mwili wa binadamu huitwa *tupu ya nyuma* au *kinyeo* badala ya *mkundu* katika Kiswahili na *inyuma* (nyuma) au *siniero* (kinyeo) badala ya *munie* (mkundu) katika Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole. Watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi hutumia tasfida hizi kwani huonyesha kazi ya sehemu husika lakini kwa njia ya upole kuliko kutaja neno lenyewe moja kwa moja kulingana na sheria za utamaduni

husika. Utamaduni wa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi huthamini sana matumizi ya lugha yenye heshima au upole katika muktadha wowote wa mawasiliano ukiwemo muktadha wa matibabu ambao tumechunguza. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni bayana kuwa tasfida zinazotumiwa kutajia neno mkundu katika Kiswahili na Kimarachi pia zinafanana pakubwa.

Maneno *matako* na *matiti* pia huleta aibu hasa yakitumiwa bila kuzingatia tasfida miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi. Kama njia ya kuonyesha upole, neno *chuchu* hutumiwa katika Kiswahili kurejelea matiti na *makalio* kurejelea *matako* katika muktadha wa matibabu ilhali *tsinuniro* (chuchu) au *makina* (mawe) hutumiwa kurejelea *tsimbere* (matiti) na *mekhaliro* kurejelea *madakho* (matako) katika Kimarachi. Mtumiaji yeyote wa Kiswahili na Kimarachi hana budi kukumbatia tasfida hizo tulizotaja ili kuonyesha kuwa amezingatia sheria za lugha husika kulingana na utamaduni wa jamii lugha. Tulibaini katika utafiti huu kuwa baadhi ya vijana wengi katika Kimarachi hurejelea matiti ya mwanamke hasa yale yaliyosimama tisti kifuani kwa tasfida *mawe* kutokana na dhana kuwa matiti ya aina hiyo hufanana na aina ya jiwe fulani lenye umbo la duara au bapa. Pia, wao hurejelea matiti ya mwanamke yaliyolala kwenye kifua kwa neno *ichapati* (chapati) badala ya kusema moja kwa moja kuwa matiti hayo yamelala kifuani. Ni dhahiri kuwa tasfida nyingi zinazotumiwa kutajia sehemu za siri kwenye mwili wa binadamu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi zinafanana pakubwa.

### 2.2.5. Tasfida za Kutaja Vitendo vya Kujamiiana

Vitendo vyote vinavyohusisha hali ya kujamiiana huzua aibu au kero iwapo wazungumzaji wa lugha fulani watavitaja bila kutumia tasfida. Kulingana na Giddens (1992) maswala kuhusu ngono huwa siri kubwa, hali ambayo husababisha uundaji wa tasfida nyingi mpya za kutajia maswala hayo.  Kitendo cha kufanya ngono kinapaswa kuhusisha watu wa jinsia tofauti, yaani

mwanamume na mwanamke ambao wamefunga pingu za maisha. Hata hivyo, kunao watu katika jamii mbalimbali wanaoweza kwenda kinyume na matarajio ya wengi na kushiriki kwenye mapenzi yanayohusisha watu wa jinsia moja. Hali kama hii huwa kinyume na tamaduni za Kiafrika. Kulingana na aibu kubwa inayoambatana na kitendo kama hicho, mwathiriwa huogopa kukitaja anapotafuta matibabu kwa namna ya tiba au ushauri kutoka kwa daktari. Kwa upande mwingine, daktari au mshauri pia huweza kuona aibu kutaja vitendo vya aina hiyo moja kwa moja bila kutumia tasfida mwafaka.

Gura (2005) asema vitendo vya ngono ni dhambi na haviruhusiwi kulingana na mafundisho ya dini kama vile ile ya Kikristo. Vitendo hivi vinapotendwa, havifai kuonekana au kuzungumziwa hadharani kwani huleta aibu. Kwa hivyo, iwapo muuguzi, mtoa ushauri nasaha, mgonjwa au mshauriwa analazimika kutaja vitendo kama hivi katika mazingira ya tiba au ushauri nasaha, anastahili kutumia tasfida zifaazo. Ni dhahiri kuwa maneno yanayorejelea vitendo vya kingono huleta aibu na kero kubwa sana hasa yanapotajwa mbele ya watu bila kuzingatia tasfida. Hali kama hii inapotendeka katika mazingira ya kimatibabu hasa kwenye tiba na ushauri nasaha huenda mawasiliano yakavurugika.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 5A**

| | **Neno** | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 55 | Tomba | Fanya mapenzi<br>Lala na mtu<br>Lala pamoja<br>Kula uroda |

| | | |
|---|---|---|
| | | Chuna ngozi<br><br>Jamii<br><br>Ingilia |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 5B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Heshima** | **Neno** | **Tasfida** |
| 56 | Soda | Khukona nende omundu<br><br>Khukhola mapenzi nende omundu<br><br>Khwirana<br><br>Kukhola madia<br><br>Khuribana alala<br><br>Khubanana mubulili<br><br>Khukhola obwitsa bwa omukhasi nende omusatsa<br><br>Khuba alala | Tomba | Kulala na mtu<br><br>Kufanya mapenzi na mtu<br><br>Kupelekana<br><br>Kufanya mapenzi<br><br>Kusukumana pamoja<br><br>Kubanana kwenye malazi<br><br>Kufanya urafiki wa mwanamume na mwanamke<br><br>Kuwa pamoja |

Ni mwiko kutaja tendo la ngono hadharani bila kutumia tasfida katika jamii lugha nyingi, zikiwemo jamii lugha za watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi. Utafiti wetu umebaini kuwa kuna tasfida nyingi ambazo hutumiwa kutajia tendo la ngono katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole katika lugha. Tasfida kama vile *fanya mapenzi, lala na mtu, lala pamoja, kula uroda, chuna ngozi* na *ingilia* hutumia badala neno

*tomba* ambalo linapotumiwa huleta aibu na kero kubwa miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili. Kutokana na hali kuwa kitendo cha ngono hufanywa kati ya watu wanaopendana, basi tendo hili hurejelewa kwa njia ya upole kuwa wanaohusika nalo huwa wanafanya mapenzi au kuonyeshana mapenzi. Zaidi ya hayo, wanaohusika hasa mwanamume na mwanamke huja pamoja au hulala pamoja dhana ambayo inakifanya kitendo hiki kurejelewa kwa nahau *lala na mtu* au *lala pamoja* katika Kiswahili. Tasfida *kona nende mundu* (lala na mtu), *khola mapenzi nende mundu* (fanya mapenzi na mtu), *khwirana* (pelekana), *khukhola madia* (fanya mapenzi), *khuribana alala* (kusukumana pamoja) na *khubanana alala* (kubanana pamoja) hutumika katika Kimarachi kama njia ya kuonyesha upole katika muktadha wa matibabu.

Utafiti huu umebaini kuwa baadhi ya tasfida za kutajia kitendo cha kufanya ngono kama vile *fanya mapenzi, lala pamoja* katika Kiswahili na *khola mapenzi* (fanya mapenzi), *kona nende mundu* (lala na mtu) katika Kimarachi zinafanana. Hata hivyo, tasfida nyingi zinazorejelea kitendo cha ngono katika lugha hizi mbili tafitiwa zinatofautiana. Kwa mfano, katika Kiswahili tasfida *kula uroda, chuna ngozi, jamii, ingilia* hutumiwa ilhali katika Kimarachi, tasfida *khwirana* (kupelekana) *khuribana alala* (kusukumana pamoja) na *khubanana mubulili* (kubanana kwenye malazi) hutumiwa. Hii ni kutokana na tofauti za sheria za kitamaduni baina ya watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi. Hymes (1974) anasema kuwa kila jamii huwa na sheria zake bainifu ambazo huwaongoza watumiaji lugha kwenye jamii lugha hiyo katika utumiaji wa lugha. Hivyo basi, neno fulani huweza kuwa tasfida katika jamii lugha moja lakini lisiwe tasfida katika jamii lugha nyingine kutokana na mifano ambayo tumeorodhesha. Kwa mfano, neno *ingilia mtu* ni tasfida yenye maana ya kufanya ngono katika Kiswahili lakini si tasfida katika Kimarachi kwani ni neno la kawaida tu ambalo lina maana ya mtu au watu kuvamia nyumba ya mtu na kuiba mali yake au hata kumwangamiza.

Ni bayana kuwa kuna tasfida nyingi ambazo hutumiwa kutajia kitendo cha kufanya ngono kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi. Kulingana na mafundisho ya dini nyingi, hasa ile ya Kikristo, tendo la ngono huonekana kama dhambi kubwa kwa wanaojihusisha nalo kabla ya ndoa au nje ya ndoa. Wale wanaohusika nalo mara nyingi hutazamwa kama wachafu na hivyo wanastahili kutakaswa. Hii huenda ikawa sababu kubwa ambayo huwafanya watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi kuibua tasfida nyingi za kutajia kitendo hicho hasa katika mazingira ya tiba na utoaji wa ushauri nasaha ili wasije wakapoteza heshima au kuvuruga utamaduni wao. Zaidi ya hayo, tendo la ngono hasa linapotajwa kiholela bila kutumia tasfida ipasavyo huweza kuwakumbusha wanajamii kuhusu chanzo cha usambazaji wa magonjwa hatari kama vile ukimwi.

### 2.2.6. Tasfida za Kurejelea Tendo la Kutoa Mimba

Baadhi ya wanawake ambao ni wajawazito huenda wakakumbwa na matatizo fulani ya kiafya na kijamii yanayoweza kusababisha mimba yao kuharibika bila wao kutaka au kutarajia. Pia, hali ya kisaikolojia au shinikizo fulani huweza kuwalazimu baadhi ya wasichana wajawazito kutoa au kuharibu mimba yao kimaksudi. Hali kama hii mara nyingi huwa mbaya sana kwa waathiriwa kulingana na uchungu, matatizo zaidi ya kiafya na matatizo ya kisaikolijia ambayo huwaandama baadaye. Kwa hivyo, maumivu yanapozidi, waathiriwa hulazimika kutafuta matibabu kutoka kwa wauguzi au ushauri nasaha kutoka kwa washauri. Matumizi ya tasfida huwa muhimu sana katika hali hii kwa sababu wengi huogopa kutaja moja kwa moja kitendo hiki chenye uchungu, aibu na ambacho pia huwa kinyume na matarajio ya tamaduni za jamii lugha nyingi hasa Afrika zikiwemo tamaduni za watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwalila 6A**

| Neno | | Tasfida |
|---|---|---|
| 57 | Kutoa mimba<br>(bila kutarajia) | Kutungua mimba<br>Mimba kuharibika<br>Ujauzito kuharibika |
| 58 | Kutoa mimba<br>(kimaksudi) | Kuharibu mimba<br>Kuavya mimba<br>Kutungua mimba |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 6B**

| | | | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| Lira | | Injira ya ovupole | Neno | Tasfida |
| 59 | Okhurusia omwana<br>(bila maksudi) | Khurekukha omwana<br>Inda khunyasika<br>Khurulutsa<br>Khuusia | Kutoa mtoto<br>(bila kutarajia) | Mtoto kutoka<br>Mimba kuharibika<br>Mimba kutoka<br>Mimba kutoka |
| 60 | Okhurusia omwana<br>(maksudi) | Khurusia mabanga<br>Khururutsa<br>Khurutsulula omwana<br>Khufubula<br>Khubwogia | Kutoa mtoto<br>(kimaksudi) | Kutoa damu<br>Kutoa mimba<br>Kutoa mtoto<br>Kutoa mimba<br>Kushtukiza |

Kutoa mimba bila kutarajia au kwa utashi wa mhusika ni jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya wanajamii wengi hasa katika jamii za Kiafrika. Tendo hili hulinganishwa na kifo ambacho huhusishwa na laana kubwa kwenye jamii lugha hasa katika familia husika. Kulingana na aibu kubwa inayoletwa na kitendo cha kutoa mimba katika jamii, utafiti huu umebaini kuwa kuna tasfida nyingi za kutajia kitendo hicho kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi ili kuonyesha upole. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa tasfida zinazorejelea kitendo cha kutoa mimba kimaksudi ni nyingi kulingana na metokeo tuliyoorodhesha kwenye jedwali la **6A** na **6B.**

Japo tendo la mimba kuharibika yenyewe halina uzito sana ikilinganishwa na lile la mimba kuharibiwa kimaksudi, baadhi ya wanajamii huliona kama laana kwa familia husika. Kwa hivyo, tasfida *kutungua mimba*, *ujauzito kuharibika* au *mimba kutoka* hutumika kama njia ya kuonyesha upole katika Kiswahili kwenye muktadha wa matibabu. Nazo tasfida *khurekukha omwana* (mtoto kutoka), *inda khunyasikha* (mimba kuharibika), *khurulutsa* (mimba kutoka) na *khuusia* (mimba kutoka) hutumika katika Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole. Matumizi ya tasfida hizi huonyesha kuwa watumiaji lugha katika Kiswahili na Kimarachi wamezingatia sheria za lugha kulingana na utamaduni husika zinazomhitaji kila mtumiaji lugha kuficha ukali wa maneno fulani kwa kutumia lugha ya upole.

Kitendo cha kutoa mimba kimaksudi hulinganishwa na kile cha kuua. Kwa hivyo, msichana au mwanamke yeyote anayejihusisha na kitendo kama hicho hufananishwa na muuaji, jambo ambalo ni mwiko katika jamii. Kutokana na changamoto ambazo huweza kumwandama mhusika baada ya kujihusisha kwenye kitendo cha kutoa mimba kimaksudi, yeye huenda akahitaji matibabu kwa njia ya tiba au ushauri nasaha. Hali hiyo hulazimu kuwepo kwa matumizi ya tasfida katika mazungumzo kati ya mwathiriwa na muuguzi au mtoa ushauri nasaha ili

kuonyesha upole. Kwa mfano, *kuavya mimba* au *kuharibu mimba* katika Kiswahili na *khurusia mabanga* (kutoa damu), *khurutsulula omwana* (kutoa mtoto kimaksudi) au *khufubula* (kutoa mimba) katika lugha ya Kimarachi hutumiwa ili kupunguza ukali fulani. Kwa hivyo, muuguzi au mtoa ushauri nasaha atakayemhoji mwathiriwa kwa kutumia tasfida husika ipasavyo ataweza kujenga mwamana na mgonjwa au mshauriwa huyo pamoja na kumpa matumaini. Hali hii itamwondolea mwathiriwa wasiwasi na kufaulisha utoaji wa matibabu bora kwa njia ya tiba au ushauri nasaha. Kwa kufanya hivyo, lengo la utoaji wa matibabu kikamilifu litaweza kuafikiwa vyema.

### 2.2.7. Tasfida za Kurejelea Baadhi ya Dawa za Kuwatibu Wagonjwa

Tiba fulani huweza kuwaogopesha wagonjwa au washauriwa hasa wanaposikia muuguzi au mtoa ushauri nasaha akitaja tiba hizo. Baadhi ya watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi huogopa matibabu ambapo wanastahili kudungwa sindano, kumeza au kunywa dawa. Kutokana na hali kama hii, huwa muhimu kuwepo kwa tasfida maalum ambazo zinaweza kutumiwa na wahusika ili kupunguza athari hasi kwa walengwa. Mifano ifuatayo itasadifu:

**KISWAHILI**

**Jedwali la 7A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 61 | Dawa | Tiba |
| 62 | Dawa ya ukimwi | Tiba ya ugonjwa mkubwa<br>Tiba ya kupunguza makali |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 7B**

| | | | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| Lira | | Heshima | Neno | Tasfida |
| 63 | Musala | Malesi | Dawa | Tiba |
| 64 | Musala kwa vukimu | Malesi ka obulwaye bukhongo<br>Malesi ka obulwaye bwefwe<br>Musala kwa lubukha | Dawa ya ukimwi | Tiba ya ugonjwa mkubwa<br>Tiba ya ugonjwa wetu<br>Tiba ya mdudu |

Tulibaini kuwa watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi wanao msamiati wa kutajia tiba ili kupunguza tishio fulani kwa walengwa. Kwa mfano, neno *'dawa'* katika Kiswahili na neno *musala (dawa)* katika Kimarachi huwaogopesha wagonjwa wanapotajiwa na muuguzi. Hii ni kwa sababu maneno haya huhusishwa na ukali au harufu mbaya ambayo baadhi ya dawa huwa nayo, hali inayowafanya wagonjwa wengi kuogopa. Hata hivyo, neno *tiba* katika Kiswahili na *malesi (tiba)* katika Kimarachi hutumiwa na wauguzi wengi kurejelea dawa ili kupunguza woga fulani kwa walengwa. Kiulinganishi, *musala* (mti) ni mkubwa kuliko *malesi* (mizizi ya mti) katika Kimarachi.

Dawa fulani mahsusi ambayo hulenga ugonjwa hatari kama vile ukimwi ambao huwatisha watu wengi unapotajwa pia hupewa tasfida ili kupunguza tishio au aibu. Utafiti huu ulibaini kuwa badala ya kusema *dawa ya ukimwi* wauguzi na wanajamii huweza kusema *tiba ya ugonjwa mkubwa* katika Kiswahili. Kwa upande mwingine, wauguzi na watoa ushauri nasaha katika

Kimarachi husema *malesi ka obulwaye bukhongo* (tiba ya ugonjwa mkubwa) badala ya kusema *musala kwa vukimu* (dawa ya ukimwi) katika mazingira ya tiba na ushauri nasaha. Matumizi ya tasfida ambazo tumetaja katika Kiswahili na Kimarachi huwasaidia wauguzi na watoa ushauri nasaha kutimiza malengo yao ambayo ni kuwatibu au kuwahudumia waathiriwa bila kuwepo na woga.

## 2.3. Hitimisho

Tumeshughulikia tasfida za tiba na ushauri nasaha katika sura hii. Tumeangazia tasfida zinazotumika kutaja magonjwa mbalimbali, takamwili, vitendo vya kutoa takamwili, vitendo vya kujamiiana, tendo la kutoa mimba na baadhi ya dawa za kuwatibu wagonjwa. Tumebaini, katika utafiti huu, kwamba kuna tasfida mbalimbali zinazotumiwa kutajia ugonjwa hatari kama vile ukimwi, taka zinazotoka mwilini, vitendo vya kutoa taka mwilini, kitendo cha kujamiiana na kitendo cha kutoa mimba kwenye muktadha wa matibabu (tiba na ushauri nasaha) katika Kiswahili na Kimarachi. Pia, tumegundua kuwa kunao mfanano mkubwa wa tasfida zinazotumiwa kutaja magonjwa, takamwili na vitendo mbalimbali kwenye maswala ya tiba na ushauri nasaha katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu.

Tumetambua katika utafiti huu kuwa maswala ya elimu na lugha anazojua mtu pamoja na umri huathiri tasfida zinazotumika katika jamii lugha kwenye muktadha matibabu. Kwa mfano, kuna wale wanaofahamu Kimarachi pekee katika jamii lugha ya Wamarachi ambao tasfida zao ni za asilia kwa sababu zinatokana na mazingira ya Kimarachi kitamaduni na kijamii. Mifano ya tasfida hizi ni *bunyaka* (kinyesi) na *khutsukha amatsi* (kumwaga maji) kwa maana ya *kukojoa*. Wale wanaofahamu Kiswahili na vile vile Kimarachi hujitokeza na tasfiri za tasfida za Kiswahili na kuzitumbukiza katika Kimarachi kama tasfida. Kwa mfano, *ikhaja indindi- haja fupi* (mkojo).

Isitoshe, wale ambao wamekwenda skuli na kufahamu Kiingereza, Kiswahili na Kimarachi hujitokeza kama walio tofauti katika miundo yao ya tasfida za Kimarachi. Wao hutumia ujuzi wao katika lugha hizi kujitokeza na tasfida nyingi na ambazo zikihakikiwa zinaonyesha kuhusiana na zile za Kiingereza, Kiswahili na Kimarachi kama vile *khutsia ihaja inyimbikiri* (kwenda haja fupi) *na khutsia ihaja indambi* (kwenda haja ndefu). Kulingana na swala la umri, tumebaini pia katika utafiti huu kuwa vijana hutumia tasfida wao kwa wao kwa kuwa watu wa makamu na wazee katika jamii lugha ya Kimarachi hawawezi kuwaelewa. Hili linadhihirisha hali ya usisi inayowatofautisha na wao kwa kuwa ni kundi la nje. Mifano ya tasfida ambazo hutumiwa sana na vijana hasa katika Kimarachi ni *makina- mawe* (matiti ya mwanamke yaliyosimama kifuani) na i*chapati* (matiti ya mwanamke yaliyolala kifuani). Kwa upande mwingine, tasfida zinazotumiwa na wazee zimejengeka katika historia na utamaduni wa Wamarachi kama jamii lugha. Mifano ya tasfida hizo ni *bunyaka* (kinyesi) na *khurusia amabanga – kutoa damu* (mwanamke kutoa mtoto tumboni kimaksudi).

# SURA YA TATU

# TASFIDA ZA UHAMASISHAJI NA UASAJI

## 3.1. Utangulizi

Uhamasishaji na uasaji wa wanajamii kuhusu maswala ya matibabu ni muhimu sana kwa afya ya wahusika. Hii ni njia mojawapo ya matibabu kwa namna ya uzuiaji wa magonjwa fulani kuenea au kuzuka miongoni mwa wanajamii lugha husika. Aghalabu ujumbe unaowasilishwa hubeba msamiati unaohusu kifo, hali za watu, matendo fulani na magonjwa mbalimbali. Lugha inayotumiwa kupitisha ujumbe wowote kwa walengwa, na hasa kwa lengo la uhamasishaji na uasaji huwa na athari kubwa sana kwa wapokezi. Kwa mfano, iwapo msamiati unaotumiwa unazua hofu, kero au aibu kwa wasikilizaji, basi huenda ujumbe husika ukose kupokelewa ilivyokusudiwa na mzungumzaji. Kwa hivyo, ni jukumu la wahamasishaji na waasaji katika Kiswahili na Kimarachi kuteua kwa uangalifu na kutumia tasfida ipasavyo ili kuonyesha upole wanapotekeleza shughuli zao.

## 3.2. Tasfida za Uhamasishaji na Uasaji

Maswala ya matibabu kwa njia ya uhamasishaji na uasaji kwa wanajamii ni muhimu na huweza kuzuia usambazaji au ueneaji wa magonjwa hatari kama vile ukimwi katika jamii. Wahamasishaji na waasaji ambao huchukua jukumu la kuwaelimisha na kuwatahadharisha wanajamii kuhusu ugonjwa fulani hatari, namna ugonjwa huo husambazwa, athari za ugonjwa huo kwa jamii lugha na jinsi ya kujiepusha na ugonjwa husika hubiidishwa kuteua na kutumia tasfida ifaavyo. Jumbe ambazo hutolewa na wahamasishaji au waasaji hawa hustahili kuwafikia walengwa kikamilifu. Hata hivyo, jambo hili litafanyika iwapo lugha ya upole ambayo haizui

aibu, kukera wasikilizaji au kutia doa kwenye utamaduni wa jamii lugha inayohusika itateuliwa na kutumika. Kwa misingi hii, hebu tuchunguze tasfida zifuatazo ambazo hutumiwa ili kuonyesha upole kwa kurejelea Kiswahili na Kimarachi hasa kwenye muktadha wa matibabu.

### 3.2.1. Tasfida za Tendo la Kuzini

Kuzini ni jambo ambalo halistahili kutajwa kiholela katika jamii nyingi ulimwenguni hapa. Kitendo hiki hudhihirisha ukosefu wa uaminifu katika ndoa kati ya mume na mke. Pia, huweza kuvuruga na kusababisha talaka au ndoa husika kuvunjika. Kwa hivyo, kutokana na uzito wa swala kama hili la mapenzi nje ya ndoa katika jamii zikiwemo jamii za watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi, mzungumzaji yeyote anayetoa hotuba kuhusu matibabu kwa lengo la kuwahamasisha au kuwaasa wanajamii anastahili kutumia tasfida ili kupunguza aibu na kero miongoni mwa wasikilizaji.

**Mifano : KISWAHILI**

**Jedwali la 8A**

| Neno | | Tasfida |
|---|---|---|
| 65 | Kuzini | Kuwa na mpango wa kando<br>Kutembea nje ya ndoa<br>Kukosa uaminifu katika ndoa<br>Kuwa na jicho la nje katika ndoa<br>Kufanya mapenzi nje ya ndoa |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 8B**

| Likhuwa | | Injira ya ovupole | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **Neno** | **Tasfida** |
| 66 | Khukhola ovudamba | Khuba nende mpango kwa kando<br>Khukenda erwanyi wa indoa<br>Khukosa buaminifu mu indoa<br>Khukhola butseke<br>Khuba nende tsimoni tsindambi | Kuzini | Kuwa na mpango wa kando<br>Kutembea nje ya ndoa<br>Kukosa uaminifu katika ndoa<br>Kufanya ukahaba<br>Kuwa na macho marefu |

Swala la kufanya mapenzi nje ya ndoa huzua aibu na kero miongoni mwa wanajamii katika jamii lugha mbalimbali zikiwemo jamii lugha za watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi. Hii ni kwa sababu tabia hii hudhihirisha ukosefu wa uaminifu baina ya wanandoa na husababisha uharibifu wa ndoa nyingi hasa ikiwa mmoja wa wanandoa atagundua hilo. Zaidi ya hayo, tendo la kuzini huwa chanzo cha uenezaji wa magonjwa ya zinaa kama vile kaswende na ugonjwa hatari wa ukimwi. Ili kujiepusha na aibu husika, wahamasishaji pamoja na waasaji katika jamii lugha ya Waswahili na Wamarachi huwasilisha hali hii kwa kuchagua na kutumia maneno ya upole namna tulivyobaini katika utafiti wetu na kuorodhesha kwenye jedwali la **8A** na **8B.**

Mhamasishaji au muasaji husema katika Kiswahili kuwa '*tuache kuwa na mpango wa kando, kutembea nje ya ndoa, kukosa uaminifu katika ndoa, kuwa na jicho la nje katika ndoa* au *kufanya mapenzi nje ya ndoa* ili kuonyesha upole badala ya kusema kuwa '*watu waache kuzini.'* Katika Kimarachi, tasfida *khuba nende mpango kwa kando* (kuwa na mpango wa kando), *khukenda*

*erwanyi wa indoa* (kutembea nje ya ndoa), *khukosa buaminifu mu indoa* (kukosa uaminifu katika ndoa), *khukhola butseke* (kufanya ukahaba) na *khuba nende tsimoni tsindambi* (kuwa na macho marefu) hutumika kurejelea kitendo cha kuzini ili kuonyesha upole katika lugha.

Utafiti huu umebaini kuwa tasfida zinazotumiwa kutajia kitendo cha kuzini katika Kiswahili na Kimarachi ni nyingi na zinafanana pakubwa. Tasfida *kutembea nje ya ndoa* katika Kiswahili na *khukenda rwanyi wa indoa* (kutembea nje ya ndoa) katika Kimarachi hutumiwa kutokana na ile hali ya mwanamume au mwanamke kumwacha mwenzake wa ndoa na kwenda kujihusisha kimapenzi na mtu au watu wengine. Zaidi ya hayo, mhusika hufanya hivyo kwa sababu ya kuangalia angalia watu wengine anaofikiria kuwa wana sura bora kuliko mwenzake halisi wa ndoa, kitendo ambacho hurejelewa kama *kuwa na jicho la nje* katika Kiswahili na *khuba nende tsimoni tsindambi* (kuwa na macho marefu) katika Kimarachi. Mtu yeyote afanyapo hivyo basi huwa amepoteza uaminifu katika ndoa hiyo hali ambayo husababisha kubuniwa kwa tasfida *kukosa uaminifu kwenye ndoa* katika Kiswahili na *khukosa buaminifu mu indoa* (kukosa uaminifu kwenye ndoa) katika Kimarachi. Anayejulikana kujihusisha na tendo kama hili pia husemwa kwa njia ya upole kuwa *ana mpango wa kando* katika Kiswahili ilhali katika Kimarachi hurejelewa kama *khuba nende mpango kwa kando* (kuwa na mpando wa kando).

Tasfida zinazorejelea neno *kuzini* husaidia kudumisha heshima kwa kupunguza aibu au kero. Hii ni kwa sababu tasfida hizo huhusisha maneno ya kawaida ambayo yakitajwa hayana madhara yoyote hasi kwa wasikilizaji. Upole hujitokeza hapa kwa kuzingatia mkakati wa nje ya rekodi, jambo ambalo pia husaidia sana kutimiza malengo ya kimawasiliano katika muktadha wa matibabu kwenye vikao vya uhamasishaji na uasaji. Isitoshe, utamaduni wa jamii husika unaomhitaji kila mtumiaji lugha kuzingatia upole katika matumizi ya lugha ili kupunguza aibu na kero huwa umezingatiwa kikamilifu.

### 3.2.2. Tasfida za Kifo na Mambo Yanayoingiliana

Kifo hutazamwa kama kitendo ambacho huwanyang'anya wanajamii wapendwa wao. Alembi (2002) anasema kuwa picha inayoletwa na kifo ni ya kuondoa au kutenganisha watu. Kifo huogopwa sana na watu katika jamii lugha nyingi hasa za Kiafrika. Kwa hivyo, ni vyema kwa wanajamii kupunguza uzito wa maneno yanayoingiliana na kifo kwa kutumia maneno ya upole, ambayo kisaikolojia hupunguza tisho kwa walengwa hasa wagonjwa. Wahamasishaji na waasaji wa wanajamii fulani hasa katika Kiswahili na Kimarachi hupaswa kutumia maneno ya upole wanapotaja au kurejelea kifo katika hotuba zao ili wasije wakawaogopesha na kuwatishia wasikilizaji.

Gumaa, A na Shi, A (2012) wanasema kuwa katika jamii zote na takriban lugha zote, kifo ni mada inayozua hisia na yenye kuogofya ambayo watu hujaribu kujiepusha kuitaja au kuzungumzia. Binadamu kitamaduni waliogopa kukabiliana na mada kuhusu kifo wakitumia maneno moja kwa moja. Tulibaini kuwa tasfida zifuatazo hutumiwa kutajia kifo na mambo yanayoingiliana na kifo katika jamii lugha ya Waswahili na Wamarachi kwenye muktadha wa matibabu.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 9A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 67 | Kufa | Kuaga dunia<br>Kulala<br>Kuacha watu<br>Kuchukuliwa na Mungu<br>Kwenda ahera<br>Kwenda jongomeo<br>Kukatika roho<br>Kushika njia ya binadamu<br>Kutoka watu<br>Kutokwa na roho<br>Kufariki dunia<br>Kukoma moyo<br>Kufuata njia ya marahaba<br>Kupumzika |
| 68 | Jeneza | Sanduku la marehemu |
| 69 | Kaburi | Nyumba ya marehemu |
| 70 | Kuzika | Kumpa marehemu kwaheri<br>Kumsindikiza marehemu |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 9B**

| | | | Tafsiri (Kiswahili) | |
|---|---|---|---|---|
| **Likhuwa** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 71 | Khufwa | Khubulukha<br>Khutsia<br>Khukona<br>Khulekha abandu<br>Khulangwa nende Nyasae<br>Khubukulwa nende Nyasaye<br>Khutsia emagombe<br>Kukhalikha omwoyo<br>Khudira injira ya buli omundu | Kufa | Kupumzika<br>Kwenda<br>Kulala<br>Kuacha watu<br>Kuitwa na Mungu<br>Kuchukuliwa na Mungu<br>Kwenda emagombe<br>Kukatika roho<br>Kushika njia ya kila mtu |
| 72 | Lisanduku lya omulambo | Lisanduku lya marehemu | Sanduku la maiti | Sanduku la marehemu |
| 73 | Ing'ani | Inyumba ya marehemu<br>Elina | Kaburi | Nyumba ya marehemu<br>Shimo |
| 74 | Khuyavira | Khuvikha<br>Khukova | Kuzika | Kuweka<br>Kusindikiza |

Kutokana na woga unaosababishwa na kutaja kifo katika mazungumzo, utafiti huu emebainisha kuwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi wanazo tasfida nyingi za kutajia hali hii katika muktadha wa matibabu hasa kwenye uhamasishaji na uasaji.

Katika Kiswahili, tasfida *kulala, kuacha watu, kukatika roho* na *kuchukuliwa na Mungu* hutumika katika muktadha wa matibabu ambazo ni sawa na tasfida *khukona* (kulala), *khulekha abandu* (kuacha watu), *khukhalikha omwoyo* (kukatika moyo) na *khubukulwa nende Nyasaye* (kuchukuliwa ma Mungu) katika Kimarachi. Maneno *kulala* au *kuacha watu* ni ya kawaida na yanapotumiwa hayazui wasiwasi miongoni mwa wasikilizaji. Basi, kutumiwa kwa maneno hayo kurejelea kifo huonyesha upole katika mazungumzo. *Kuchukuliwa na Mungu* huleta dhana kuwa aliyekufa ameondoka tu kwenda kumwona Mungu. Hali hii huwapa wazungumziwa matumaini fulani kuwa watakutana na aliyechukuliwa na Mungu tena siku moja. Kwa hivyo, mhamasishaji au muasaji anapohutubia wanajamii lugha husika kwenye kikao fulani husema kwa upole *'ukijihusisha katika mapenzi kiholela utatuacha haraka'* badala ya kusema kuwa *'ukifanya ngono kiholela utakufa haraka.'* Tasfida zingine kama vile *kuaga dunia, kwenda ahera, kwenda jongomeo, fariki dunia na koma moyo hutumiwa* katika Kiswahili kwenye muktadha wa matibabu kurejelea kifo kwa njia ya upole ilhali tasfida *khutsia emagombe* (kwenda emagombe) hutumiwa katika Kimarachi kama njia ya kuonyesha pia upole. Kuwepo kwa tofauti kwenye baadhi ya tasfida tulizotaja za kurejelea kifo katika Kiswahili na Kimarachi kunatokana na sheria tofauti za utamaduni wa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi ambazo hutawala uibuaji wa tasfida na matumizi yake ili kuonyesha upole.

Tulibaini kuwa watumiaji wengi wa Kiswahili na Kimarachi huogopa kusikia neno *kaburi* likitajwa katika muktadha wa matibabu hasa kwenye vikao vya uhamasishaji na uasaji. Ili kupunguza woga huo na kuonyesha upole, tasfida *nyumba ya marehemu* hutumika katika Kiswahili ambayo ni sawa na *inyumba ya marehemu* (nyumba ya marehemu) katika Kimarachi. Neno *nyumba* humaanisha mahali ambamo binadamu huishi ilhali *marehemu* ni jina la kiheshima linalotumiwa kurejelea mtu aliyekufa. Kwa mfano, mhamasishaji au muasaji

anayetumia Kiswahili anaweza kusema kwa upole kuwa *'vijana wasiojichunga wataingia kwenye nyumba ya marehemu wangali wadogo'* badala ya kusema kuwa *'vijana wanaofanya usherati watamezwa na kaburi wangali wadogo.'* Pia, mtumiaji wa Kimarachi husema kwa upole kuwa *'varaga varechunga walenjira mu inyumba ya marehemu nibasiri baere'* (vijana wasiojichunga wataingia kwenye nyumba ya marehemu wangali wadogo) badala ya kusema kuwa '*varaga vakholanga ovudamba valamirwa nende ing'ani nibasiri baere'* (vijana wanaofanya usherati watamezwa na kaburi wangali wadogo). Kitendo cha kuzika maiti pia hurejelewa kwa tasfida katika Kiswahili na Kimarachi namna tulivyobaini na kuorodhesha katika data yetu ili kuonyesha upole.

Ni wazi kuwa tasfida zinazotumiwa hulenga kupunguza makali ya neno *kifo* na kuleta matumaini kuwa mhusika ameondoka tu au amelala na huenda akarudi au wakakutana naye siku moja. Kwa hivyo, wahamasishaji na waasaji wanapotumia tasfida hizo tulizopata na kuorodhesha, hupunguza tishio kwa wasikilizaji na kuwafanya kupokea ujumbe husika bila woga. Gumaa na Shi (2012) wanaeleza kuwa binadamu hukwepa kutumia maneno yanayotisha kuhusu kifo na badala yake kuyafunika kwa kutumia yale yenye upole.

Hata hivyo, Herbert (2016) anaonya kuwa tasfida zinazorejelea kifo lazima zitumiwe kwa makini hasa mbele ya watoto ili wasije wakachanganyikiwa na kuwa na hofu. Kwa mfano, mtoto anayeambiwa kuwa mwenzake *amelala* ilhali *amekufa* huenda akaogopa kulala akiona kwamba yule anayesemwa kuwa amelala haamki kamwe. Basi, lazima tasfida za kifo ziteuliwe kwa makini kwa kuzingatia umri wa wahusika na hata viwango vyao vya uelewa.

### 3.2.3. Tasfida za Kazi za Watu

Kunazo kazi zinazofanywa na baadhi ya watu katika jamii mbalimbali zikiwemo jamii lugha za Waswahili na Wamarachi hasa katika muktadha wa matibabu ambazo zinapotajwa hadharani bila kuzingatia lugha ya upole huweza kuwaaibisha au kuwakera baadhi ya wahusika. Mtumiaji wa lugha yoyote katika jamii lugha zinazohusika anapowahamasisha au kuwaasa wanajamii lugha husika lazima azingatie na kuteua tasfida za kutumia katika hotuba yake hasa anaporejelea watu wanaofanya kazi fulani kwenye muktadha wa matibabu. Baadhi ya kazi hizi ni kuosha vyoo, kuzalisha wanawake na kutahiri. Kazi hizi hurejelewa na wahamasishaji pamoja na waasaji katika jamii kwani huweza kuwa njia mojawapo ambazo magonjwa hatari husambazwa. Kwa mfano, kuwapasha wavulana tohara huweza kusababisha maambukizo ya ugonjwa wa ukimwi iwapo vifaa vinavyotumiwa kama vile visu havitatumiwa kwa makini. Pia, mtu anayeosha vyoo asipovaa glovu inavyofaa huenda akaandamwa na maradhi ya kipindupindu. Hebu tuangalie mifano ya tasfida tulizopata.

**KISWAHILI**

**Jedwali 10A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 75 | Mkunga | Muuguzi anayewasaidia akina mama kujifungua |
| 76 | Ngariba | Daktari wa kuwapasha wavulana tohara |
| 77 | Chura | Mtu anayesimamia usafi msalani |
| 78 | Mfanyakazi kwenye | Msimamizi wa usafi katika hifadhi ya wafu |

| | | |
|---|---|---|
| | nyumba ya maiti | |
| 79 | Daktari wa wanawake | Mtaalamu wa mambo kuhusu wanawake |

**KIMARACHI**

**Jedwali 10B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 80 | Mwivusi | Mnasi ukhonyanga abakhasi bali asiro khwebolola | Mkunga | Muuguzi anayewasaidia akina mama wajawazito kujifungua |
| 81 | Mukhebi | Daktari ukasianga abasiani | Ngariba | Daktari anayewatengeza wavulana |
| 82 | Mwosi wa tsichoo | Mundu wemeranga obusafi bwa tsichoo | Chura | Mtu anayesimamia usafi wa choo |
| 83 | Mwosi wa milambo | Wemeranga busafi mu inyumba ya vafu | Anayeosha Maiti | Anayesimamia usafi kwenye chumba cha wafu |
| 84 | Daktari wa Abakhasi | Mtalamu usirikhanga vamama | Daktari wa wanawake | Mtaalamu anayewatibu kina mama |

Utafiti wetu ulibaini kuwa kazi fulani za watu katika muktdha wa matibabu hasa zile zisizofaa kutajwa ovyo ovyo hurejelewa kwa namna ya maelezo ili kuonyesha upole. Njia ya kipekee ya kuifanya hadhira ielewe haraka kwa namna ya upole jambo ambalo wahamasishaji au waasaji wanasema ni matumizi ya maelezo ambayo yanaonyesha upole.  Maelezo haya hufafanua picha halisi ya kazi inayorejelewa kwa njia ya kuonyesha kiasi fulani cha heshima.

Tulibaini katika utafiti huu kuwa neno *mkunga* halionyeshi heshima hasa linapotumiwa kurejelea mtu au muuguzi anayewazalisha wanawake. Maelezo '*muuguzi anayewasaidia wanawake wajawazito kujifungua'* hutumiwa ili kuonyesha upole katika mazungumzo kwenye muktadha wa matibabu badala ya kutumia neno *mkunga* katika Kiswahili. Maneno haya ya heshima pia hutumiwa na wahamasishaji na waasaji katika Kimarachi ili kuonyesha upole. Kwa mfano, badala ya kusema *mwivusi* (mkunga) maelezo '*mnasi ukhonyanga vamama khwebolola'* (muuguzi anayewasaidia akina mama kujifungua) hutumiwa kwa lengo la kuonyesha upole.

Mtu anayefanya kazi ya kuwatahiri wavulana hurejelewa kama *ngariba* katika lugha ya Kiswahili na *mukhebi* katika Kimarachi. Hata hivyo, majina haya hukosa heshima kwa wahusika hasa yanapotajwa kwenye vikao vya uhamasishaji au uasaji wa umma. Kama juhudi za kujenga mwamano mzuri na kufikia malengo husika ya matibabu kwa njia ya uhamasishaji na uasaji, wazungumzaji hawana budi kuteua na kutumia maneno ya heshima kurejelea watu wanaofanya kazi hii ya kutahiri. Kwa mfano, '*daktari wa kuwapasha vijana tohara'* hutumiwa katika Kiswahili ilhali '*daktari ukasianga basiani'* (daktari anayewatengeneza wavulana) hutumiwa katika Kimarachi ili kuonyesha upole.

Matokeo ya utafiti wetu pia yanaonyesha kuwa mtu anayeosha vyoo, anayefanya kazi kwenye chumba cha kuhifadhi maiti na daktari anayewahudumia wanawake hurejelewa kwa kutumia tasfida ili kudhihirisha upole katika lugha.

### 3.2.4. Tasfida za Hali za Watu

Binadamu katika jamii lugha yoyote huwa katika hali tofauti kulingana na maumbile yao, hali zinazowakumba kutokana na magonjwa fulani au maswala ya uzazi. Wahamasishaji au waasaji katika jamii lugha kama vile jamii lugha za watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi wanapowahutubia wanajamii kuhusu maswala ya matibabu hasa kwa kurejelea mbinu za kupunguza uenezaji wa magonjwa hatari, hawana budi kutumia msamiati wa upole wanaporejelea watu wenye hali mbalimbali kama vile watu walemavu, wendawazimu, walevi na malaya. Matumizi ya tasfida kurejelea watu wenye hali kama hizo husaidia kupunguza makali kwenye lugha na kuondoa aibu na kero hasa kwa wale ambao wana hali kama hizo na wamo miongoni mwa wasikilizaji. Pia, matumizi ya lugha ya upole husaidia kufanikisha mawasiliano na kufanya walengwa kupokea ujumbe kikamilifu bila kuwepo na vizuizi vyovyote.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali 11A**

| Neno | | Tasfida |
|---|---|---|
| 85 | Mlemavu | Mtu aliye na upungufu fulani mwilini<br>Mtu aliye na upungufu wa kimwili |
| 86 | Mwendawazimu | Mtu aliyepungukiwa akili<br>Mtu aliyechanganyikiwa akili |
| 87 | Mlevi | Mtu anayeonja mvinyo kupindukia |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mtu aliyepiga maji |
| 88 | Malaya | Kiruka njia (mwanamke)<br>Kuwa jamvi la wageni (mwanamke)<br>Kiruka mito (mwanamume)<br>Anayependa kufanya mapenzi ovyo |
| 89 | Basha/ Shoga | Mwanamume anayevutiwa na watu wa jinsia yake ya kiume |
| 90 | Msagaji | Mwanamke anayevutiwa na watu wa jinsia yake ya kike |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 11B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 91 | Mulema | Weindieku<br>Welikara<br>Uli nende bulemu khu mubiri | Kilema | Mwenye upungufu<br>Aliyepungukiwa kimwili<br>Aliye na upungufu mwilini |
| 92 | Mulalu | Mulwaye wa bwongo | Mwenda wazimu | Mgonjwa wa akili |
| 93 | Mumesi | Mundu ukhombangakho amatsi | Mlevi | Mtu anayeonja maji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 94 | Omudamba/ malaya | Mundu wetsimoni tsindambi<br><br>Omuyeyi<br><br>Mutseke | Malaya | Mtu mwenye macho marefu<br><br>Anayependa kufanya mapenzi<br><br>Anayependa kufanya mapenzi |
| 95 | Musatsa ukholanga mapenzi nende musatsa | Musatsa ukholanga mapenzi kesifwabi | Basha | Mwanamume anayefanya mapenzi chafu sana |
| 96 | Mukhasi ukholanga mapenzi nende mukhasi | Musatsa ukholanga mapenzi kesifwabi | Msagaji | Mwanamke anayefanya mapenzi chafu sana |

Kunazo tasfida tofauti zinazotumiwa kurejelea watu walio na upungufu fulani wa kimwili au tabia fulani hasi katika jamii lugha za watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi katika muktadha wa matibabu. Kwa mfano, badala ya kutaja neno *mlemavu* mhamasishaji au muasaji husema *mtu aliye na upungufu mwilini* ili kuonyesha upole. Katika Kimarachi, tasfida *weindieku* (mwenye upungufu), *welikara* (aliyepungukiwa kimwili) na *uli nende bulemu khumubiri* (aliye na upungufu mwilini) hutumiwa ili kuonyesha upole katika lugha. Neno *upungufu* katika Kiswahili na Kimarachi linapotumiwa kurejelea mtu mlemavu katika muktadha wa matibabu aghalabu huondoa aibu au kero ambayo huweza kuwaandama wahusika walio na shida hiyo.

Mhamasishaji au muasaji anapohutubia kundi fulani la watu kwa nia ya kuwaelekeza jinsi ya kuzuia magonjwa fulani hupaswa kuteua tasfida mwafaka za kutajia mtu ambaye ni mwendawazimu ili kuonyesha upole. Kwa mfano, tasfida *mtu aliyepungukiwa akili* au *mtu aliyechanganyikiwa akili* hutumiwa katika Kiswahili badala ya neno *mwendawazimu*. Kwa upande mwingine, tasfida *mulwaye wa bwongo* (mgonjwa wa kili) hutumiwa katika Kimarachi badala ya neno *mulalu* (mwendawazimu) kuonyesha upole na heshima.

Neno *mlevi* huzua kero hasa miongoni mwa wahusika wa kitendo hiki. Kwa hivyo, wahamasishaji au waasaji wanaporejelea watu wenye tabia ya ulevi katika muktadha wa matibabu hupaswa kutumia tasfida ili wanaolengwa wasikasirike. Kwa mfano, maelezo *mtu anayeonja mvinyo kupindukia* hutumiwa katika Kiswahili badala ya neno *mlevi* ili kuonyesha upole. Kwa upande mwingine, tasfida *mundu ukhombangakho amatsi* (mtu anayeonja maji) hutumiwa katika Kimarachi. Mhamasishaji au muasaji anaweza kusema kuwa *'tujaribu kujiepusha na kuonja mvinyo kupindukia kwa sababu hali kama hii huweza kudhuru afya sana'* badala ya kusema kuwa '*walevi waache tabia hiyo kwa sababu itawaletea magonjwa hatari.'* Kauli ya kwanza ina upole umbao utawafanya waathiriwa kusikiliza na hata kujaribu kufuata maagizo ya kimatibabu. Mhamasishaji katika Kimarachi pia anaweza kusema kuwa *'khupungusie khukhomba amatsi ili khulinde afya yefwe'* (tupunguze kuonja maji ili tulinde afya yetu) badala ya kusema kuwa *'khupungusie khumera ili khuzuie obulwaye hatari'* (tupuguze kulewa ili tuzuie ugonjwa hatari).

Tumetambua katika utafiti huu kuwa neno *malaya* katika Kiswahili na *mudamba* katika Kimarachi huzua aibu na kero miongoni mwa wahusika hasa yanapotajwa kwenye muktadha wa matibabu. Wazungumzaji wa Kiswahili hutumia nahau *kiruka njia (mwanamke)*, *kuwa jamvi la wageni (mwanamke)*, *kiruka mito (mwanamume)* na *anayependa kufanya mapenzi ovyo* kurejelea mtu malaya ili kudumisha upole katika lugha. Nahau *kuwa jamvi la wageni* huwa na maana ya mwanamke kuruhusu kila mwanamume anayemjia kulala naye namna kila mgeni anayefika nyumbani huweza kukaa au kulala juu ya jamvi. Katika Kimarachi, tasfida *mundu wetsimoni tsindambi* (mtu mwenye macho marefu), *omuyeyi* (mtu anayependa kufanya mapenzi) na *mutseke* (mtu anayependa kufanya mapenzi) hutumiwa ili kuonyesha upole katika lugha. Tasfida *mundu wetsimoni tsindambi* (mtu mwenye macho marefu) hutumiwa kutokana na hali kuwa mtu

yeyote anayependa kufanya mapenzi au usherati kila mara hutazama tazama mtu wa kuzini naye popote alipo. Tasfida hizi zinapotumiwa huonyesha upole na kupunguza aibu miomgoni mwa wahusika.

Kutaja maneno *basha* au *msagaji* huleta aibu mbele ya watu kwenye muktadha wa matibabu kulingana na matokeo ya utafiti wetu. Wahamasishaji na waasaji wanaotumia Kiswahili hutumia maelezo yanayoonyesha upole kurejelea watu wenye tabia kama hizo. Kwa mfano, maelezo *mtu anayevutiwa kimapenzi na mtu mwingine wa jinsia yake* ya *kiume au kike* hutumiwa kurejelea maneno *basha* na *msagaji* mtawalia kwa njia ya upole. Utafiti wetu ulibani kuwa hakuna tasfida mahsusi za kutajia watu wenye tabia kama hizi katika Kimarachi kwani tabia hizi haziaminiki kuwepo katika jamii lugha ya wazungumzaji wa Kimarachi. Hata hivyo, watafitiwa walieleza kuwa mtu mwenye tabia kama hizo huweza kurejelewa kama *mundu ukholanga mapenzi kesifwabi* (mtu anayefanya mapenzi chafu sana) ili kuonyesha upole katika mazungumzo.

### 3.2.5. Tasfida za Kurejelea Mwanamke aliye na Mimba

Hali ya mwanamke kuwa na mimba haifai kutajwa ovyo ovyo moja kwa moja mbele ya watu kwani kufanya hivyo ni kukosa heshima kulingana na jamii lugha nyingi zikiwemo jamii lugha za Waswahili na Wamarachi. Ili kujiepusha na aibu au kero yoyote, wajamii lugha husika hutarajiwa kutumia tasfida komavu ili kurejelea hali kama hii. Tengku na Sepideh (2012) wanasema kuwa maneno ni vielelezo muhimu vya ishara za kitamaduni. Hii ina maana kuwa maneno fulani yakitumiwa kwa njia ya heshima huashiria kuwa jamii lugha husika huthamini sana heshima. Kwa hivyo, wahamasishaji na waasaji katika jamii lugha ya Kiswahili na Kimarachi lazima watumie maneno ya heshima ili ujumbe wao kuhusu matibabu uifikie hadhira lengwa bila athari yoyote hasi.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 12A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 97 | Mwanamke aliye na mimba | Mama mjamzito<br>Mama anayetarajia<br>Mama aliyelemewa |

**KIMARACHI**

**Jedwali 12B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tafsida** |
| 98 | Omukhasi uli inda | Mama uli asiro<br>Mama utarajia | Mwanamke aliye na mimba | Mwanamke mjamzito<br>Mama anayetarajia |

Tasfida hutumiwa sana kutajia hali ya mwanamke kuwa na mimba ili kudumisha heshima kulingana utamaduni wa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi katika muktadha wa matibabu. Neno *mimba* halitajwi kamwe katika jamii lugha husika na badala yake kufananishwa na uzito fulani ambao mwanamke huwa amebeba. Kwa mfano, wahamasishaji na waasaji katika jamii lugha za watumiaji wa Kiswahili husema kuwa *'wanawake wajawazito wawaone wauguzi kila mara ili kudumisha afya bora'* kuliko kusema kuwa *'wanawake walio na mimba waende hospitalini kila mara kupimwa afya yao.'* Katika Kimarachi, mhamasishaji au muasaji husema

‘*abakhasi bali asiro vavalole basirishi buli sikha ili vavacheke afya yavwe’* (wanawake wajawazito wawaone wauguzi kila wakati ili kuchunguzwa afya yao). Tasfida hii hutumiwa kuonyesha upole badala ya kusema kuwa ‘*abakhasi bali inda batsie musivitali ili vapimwe afya yavwe’* (wanawake walio na mimba wawaone wauguzi ili wapimwe afya yao). Watumiaji wa Kiswahiili na Kimarachi watakuwa wamezingatia sheria za utamaduni husika ambapo kila mtumiaji wa lugha anapaswa kutumia lugha ya heshima, yaani tasfida. Utafiti huu unadhihirisha kuwa tasfida zinazotumiwa kutajia hali ya mwanamke kuwa na mimba katika Kiswahili na Kimarachi zinaelekeana pakubwa.

### 3.2.6. Tasfida za Kurejelea Kitendo cha Mwanamke Kuzaa

Kulingana na Kamusi Sanifu ya TUKI (2014) neno kuzaa lina maana ya kutoa mtoto tumboni au mimea kutoa matunda. Neno mwafaka linalojitokeza katika kamusi hii sanifu kurejelea kitendo *kuzaa* hasa binadamu kwa njia ya upole ni *kujifungua.* Kitendo hiki ndicho hupelekea kuwepo kwa viumbe vipya duniani. Tamaduni za jamii lugha nyingi za Kiafrika zikiwemo jamii lugha za Waswahili na Wamarachi hazikubali mtumiaji lugha kutaja kitendo hiki hadharani bila kutumia tasfida hasa anaporejelea binadamu. Hata hivyo, kitendo hiki huwa na changamoto zake kama vile uchungu kwa akina mama pamoja na uchafu unaoshuhudiwa, hali ambayo huweza kuwatisha, kuwachukiza au kuzua aibu miongoni mwa watumiaji lugha. Wahamasishaji na waasaji wa umma hawana budi kutumia tasfida teule hasa zile komavu kurejelea kitendo hiki hasa wanapoihutubia hadhira lengwa kuhusu matibabu hususan namna magonjwa fulani huweza kusambazwa katika jamii lugha za wazungumzaji wa Kiswahili na Kimarachi ili kuonyesha upole. Ifuatayo ni mifano ya tasfida ambazo hutumiwa kutajia kitendo cha mwanamke kuzaa katika Kiswahili na Kimarachi.

**KISWAHILI**

**Jedwali 13A**

| **Neno** | | **Tasfida** |
|---|---|---|
| 99 | Kuzaa | Kujifungua<br>Kupata salama<br>Kujitua mzigo<br>Kujaliwa |

**KIMARACHI**

**Jedwali 13B**

| | | | **Tafsiri (Kiswahili)** | |
|---|---|---|---|---|
| **Lira** | | **Injira ya ovupole** | **Neno** | **Tasfida** |
| 100 | Khwivula | Khwebolola<br>Khwerusiakho<br>Khwekhonya | Kuzaa | Kujifungua<br>Kujitoamo<br>Kujisaidia |

Watumiaji wa lugha ya Kiswahili na Kimarachi hutaja tendo la kuzaa mtoto kwa kutumia tasfida katika muktadha wa matibabu. Utafiti huu umebaini kuwa wahamasishaji na waasaji wengi hutumia tasfida ipasavyo kurejelea tendo la mama kupata mtoto. Kutaja neno *kuzaa* katika Kiswahili na *khwivula* (kuzaa) katika Kimarachi huonyesha ukosefu wa heshima mbele ya watu. Kwa hivyo, ili kudumisha heshima miongoni mwa watumiaji lugha katika muktadha wa

matibabu hasa katika uhamasishaji na uasaji, wahusika hawana budi kuteua na kutumia tasfida zinazoeleza kitendo hiki lakini kwa njia ya upole.

Tasfida *kujifungua* hutumiwa katika Kiswahili kurejelea kitendo cha kuzaa kutokana na hali kuwa mwanamke huwa amelegeza tumbo lake au amepata uhuru fulani wa kufanya kazi ambazo hakuwa anazifanya. Tasfida hiyo katika Kiswahili inalingana na tasfida *khwebolola* (kujifungua) katika Kimarachi. K*upata salama* na *kujaliwa* ni tasfida zaidi ambazo hutumiwa katika Kiswahili kumaanisha kuwa mwanamke amejaliwa mtoto ili kuficha neno lenye la aibu *kuzaa*. Pia, tasfida *kujitua mzigo* hutumiwa katika Kiswahili kwa lengo la kuficha aibu kwenye muktadha wa matibabu kutokana na hali kuwa mwanamke huwa amejitua mzito, yaani mtoto ambaye alikuwa amembeba tumboni. Kwa upande mwingine, wahamasishaji na waasaji wanaotumia Kimarachi husema kwa upole kuwa *omukhasi werusiekho* (mwanamke ambaye amejitoamo) badala ya kusema *omukhasi wivule* (mwanamke ambaye amezaa). Neno *khwerusiakho* (kujitoamo) hutokana na dhana kuwa mhusika huwa amejitoa katika uzito au kazi fulani ngumu ya kumbeba mtoto tumboni. Tasfida hiyo hutumiwa badala ya neno *kuzaa* ili kuondoa kero au aibu miongoni mwa wahusika katika muktadha wa matibabu. Zaidi ya hayo, tasfida *yekhonyere* (amejisaidia) pia hutumika na watumiaji wa Kimarachi katika muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole katika lugha.

### 3.2.7. Tasfida za Magonjwa

Wahamasishaji na waasaji kuhusu swala la matibabu hutaja baadhi ya magonjwa hasa yale hatari kama vile ukimwi na saratani wanapoihamasisha hadhira lengwa. Kutokana na maelezo tuliyotoa hapo awali kwenye sura ya pili kuhusu tasfida za tiba na ushauri nasaha, wahamasishaji na waasaji pia hawana budi kuzingatia lugha yenye upole wanapotaja magonjwa mbalimbali hasa

yale hatari kama vile ukimwi. Hii ni kwa sababu kutaja magonjwa hatari kama vile ukimwi kila mara mbele ya watu huwakumbusha kuhusu kifo. Kwa hivyo, wahamasishaji na waasaji katika Kiswahili na Kimarachi hutumia tasfida kama vile *ugonjwa mkubwa* katika Kiswahili na *bulwaye bukhongo* (ugonjwa mkubwa) katika Kimarachi kurejelea ukimwi kama njia ya kupunguza tishio kwa walengwa. Tumekwisha kuorodhesha tasfida za magonjwa mbalimbali kwenye sura ya pili katika jedwali la **1A** na **1B.**

### 3.2.8. Tasfida za Vitendo vya Kufanya Ngono

Vitendo vya kujamiiana huzua aibu na kero vinapotajwa mbele ya watu kulingana na tamaduni nyingi hasa za jamii lugha za Kiafrika. Giddens (1992) anasema kuwa maswala ya ngono yamekuwa siri kubwa sana katika jamii lugha yoyote. Tendo la kujamiiana kati ya mwanamume na mwanamke linaruhusiwa tu kwa mume na mke ambao wamefunga pingu za maisha kulingana na mafundisho ya dini husika. Hata hivyo, tendo hili linapaswa kutekelezwa mahali maalum pa siri na halipaswi kutajwa hadharani na kihohela. Kutokana na sababu fulani za kisaikolojia, kisosholojia na shinikizo la rika hasa miongoni mwa vijana, kuna baadhi ya wanajamii ambao huweza kwenda kinyume kitabia na kujihusisha katika mapenzi na wenzao wa jinsia moja. Hali kama hii huleta aibu au kero kubwa sana inapotajwa mbele ya watu hasa katika muktadha wa matibabu. Zaidi ya hayo, wanajamii husika huwa na aibu na kuona kwamba huenda vizazi vijavyo vikaambukizwa hulka hasi na chafu kama hizo. Kwa hivyo, ili kuzungumzia swala kama hilo katika muktadha wa matibabu kwenye jamii lugha nyingi zikiwemo hizi za Waswahili na Wamarachi, lazima tasfida ziteuliwe kwa uangalifu na kutumiwa ili kuonyesha upole. Rejelea mifano ya tasfida hizi kwenye sura ya pili chini ya tasfida za tiba na ushauri nasaha.

### 3.3. Hitimisho

Uhamasishaji na uasaji wa wanajamii kuhusu maswala ya afya ni muhimu sana. Hii ni njia mojawapo ya matibabu hasa kwa namna ya uzuiaji wa magonjwa fulani kuenea au kuzuka miongoni mwa wanajamii lugha husika kama vile jamii za watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi. Lugha inayotumiwa kupitisha ujumbe wowote kwa walengwa, hasa kwa lengo la uhamasishaji au uasaji huwa na athari kubwa kwa wapokezi. Iwapo msamiati unaotumiwa unazua aibu, kero au tishio kwa wasikilizaji basi huenda ujumbe ukose kupokelewa na walengwa ilivyokusudiwa na mzungumzaji. Kwa hivyo, wahamasishaji na waasaji katika Kiswahili na Kimarachi hawana budi kukumbatia tasfida ipasavyo wanapotekeleza majukumu yao ya kuwahamasisha na kuwaasa wanajamii kuhusu maswala ya matibabu.

Kama tulivyoona katika tasfida za tiba na utoaji wa ushauri nasaha, pia kuna mfanano au mwelekeano mkubwa katika tasfida za uhamasishaji na uasaji katika Kiswahili na Kimarachi. Kwa mfano, tasfida zinazotumiwa kutajia tendo la kuzini, kazi za watu, mwanamke aliye na mimba na tendo la mwanamke kuzaa zinaelekeana pakubwa katika lugha hizi mbili. Hili linaonyesha kuwa lugha hizi mbili zina mame lugha moja; Kibantu.

Tumetambua katika utafiti huu kuwa Wamarachi wanaoishi mashambani hutumia tasfida za asilia zinazotokana na mazingira ya Kimarachi kitamaduni kwani wengi wao hawajaingiliana sana na watu wanaozungumza Kiswahili au lugha nyingine. Mifano ya tasfida hizi ni *mutseke* au *khuba nende tsimoni tsindambi* kumaanisha *malaya.* Kwa upande mwingine, Wamarachi wanaoishi kwenye miji midogo midogo kama vile Murumba mara nyingi hutumia tasfida ambazo zimetafsiriwa hasa kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Mfano wa tasfida hizi ni *khuba nende mpango kwa kando* (kuwa na mpango wa kando) kumaanisha *kuzini* au *kushiriki mapenzi*

*nje ya ndoa*. Tulibaini vile vile katika utafiti huu kuwa wanawake ambao ni wahamasishaji, waasaji, wauguzi, washauri na wale wengine katika jamii lugha ya Wamarachi huwa makini sana katika uibuaji na utumiaji wa tasfida katika mazungumzo kwenye muktadha wa matibabu ikilinganishwa na wanaume. Hii hutokana na hali kuwa wanawake huonwa kama watu wapole sana.

Tasfida hizi ambazo tumepata katika sura hii ya tatu na ile ya pili zitakuwa msingi bora kwenye sura ya nne kwani zitatusaidia kubaini mikakati mbalimbali ambayo watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi hutumia ili kuibua tasfida katika muktadha wa matibabu.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA UIBUAJI WA TASFIDA ZA MUKTADHA WA MATIBABU

## 4.1. Utangulizi

Mikakati au njia mbalimbali hutumiwa na wanajamii katika jamii lugha husika ili kuibua tasfida zinazotumika kutajia maswala ambayo yanahusiana na matibabu. Wanajamii lugha hawa wakiwemo wale wa jamii za Waswahili na Wamarachi hutumia mikakati hiyo kuunda tasfida ambazo huzoeleka na kutumiwa katika muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole. Warren (1992) anapendekeza mikakati minne ambayo kwake huweza kutumiwa kuibua au kuunda tasfida. Mikakati hii ni kama vile kufanya mabadiliko ya kisauti katika maneno, kukopa maneno kutoka katika lugha nyingine, kubuni maana mpya za maneno na kuunda majina mapya. Katika mikakati hii minne, kuna ndani yake mikakati midogo midogo inayotumiwa. Maoni haya yanatoa mwanga kuhusu namna tasfida huweza kuundwa katika jamii lugha yoyote ile. Hata hivyo, wanajamii lugha tofauti hasa wanaotumia Kiswahili na Kimarachi huweza kuwa na mikakati mingine zaidi ya ile iliyopendekezwa na Warren (1992) katika uibuaji wa tasfida hasa kwenye muktadha wa matibabu. Warren (ibid) mwenyewe anasema kuwa mikakati mingine midogo midogo kando na ile aliyopendekeza huweza kutumiwa katika uibuaji wa tasfida. Hili ndilo hasa lengo kuu la sura hii.

## 4.2. Mikakati ya Uibuaji wa Tasfida za Muktadha wa Matibabu

Kulingana na maelezo ambayo tumetoa katika utangulizi, ni bayana kuwa ipo mikakati mbalimbali ambayo watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimamarachi hutumia kuibua tasfida

zinazotumiwa katika muktadha wa matibabu ili kuonyesha upole. Bila shaka, mikakati tofauti tofauti hutumiwa ili kupata maneno ambayo yanaonyesha heshima kutajia magonjwa, uchafu unaotoka mwilini, sehemu za siri mwilini, hali za watu, vitendo vya kutoa uchafu mwilini, vitendo vingine vya aibu na kazi fulani fulani za watu katika muktadha wa matibabu. Nichol (2011) anaeleza njia saba zinazoweza kutumiwa katika uundaji wa tasfida katika jamii lugha mbalimbali. Njia hizi ni matumizi ya lugha fiche, kutumia maelezo yasioyo ya moja kwa moja, kutumia maneno hasi ili kupunguza ukali au uzito wa neno fulani, kutamka neno vibaya kimaksudi, kubadilisha kategoria ya neno, kutumia tashhisi na matumizi ya misimu. Ni dhahiri kuwa si watumiaji wa lugha katika jamii lugha zote huzingatia au hutumia mikakati hiyo yote. Utafiti wetu ulibaini kuwa kila jamii lugha au kundi fulani la watumiaji lugha huwa na mikakati yao ya kuibulia tasfida hasa kulingana na sheria zinazoongoza utamaduni wao. Tulibaini kuwa si mikakati yote iliyopendekezwa na Warren (1992) na ile inayoelezwa na Nichol (2011) hutumika katika uibuaji wa tasfida katika Kiswahili na Kimarachi.

Kulingana na matokeo ya utafiti wetu, mikakati ifuatayo hutumiwa kuibua tasfida katika Kiswahili na Kimarachi:

### 4.2.1. Mkakati wa Kutumia Maelezo Marefu

Watumiaji wa lugha katika jamii lugha yoyote zikiwemo jamii lugha za Waswahili na Wamarachi mara nyingi hutumia maelezo marefu kueleza kitendo, hali au ugonjwa fulani ili kupunguza makali ya jambo hilo iwapo lingetajwa kwa kutumia neno fulani moja kwa moja. Mkakati wa kutumia maelezo marefu yasiyo ya moja kwa moja ulipendekezwa na Nichol (2011). Mkakati huu wa kutumia maelezo marefu huwasaidia wauguzi, watoa ushauri nasaha,

wahamasishaji na waasaji kurejelea neno fulani katika Kiswahili na Kimarachi kwa njia isiyozua aibu, kero au kutisha. Kuna baadhi ya maneno ambayo yakitajwa jinsi yalivyo hukosa heshima.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 15A**

| Neno | | Tasfida |
|---|---|---|
| i | Ukimwi | Ugonjwa mkubwa |
| ii | Bawasiri | Ugonjwa wa tupu ya nyuma |
| iii | Mkunga | Muuguzi anayewasaidia kina mama kujifungua |
| iv | Chura | Mtu anayesimamia usafi wa vyoo |
| v | Usaha | Uchafu unaotoka kwenye kidonda |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 15B**

| Lira | | Injira ya ovupole | Tasfiri (Kiswahili) |
|---|---|---|---|
| i | Vukimu | Bulwaye bukhongo<br>Bulwaye bwefwe | Ugonjwa mkubwa<br>Ugonjwa wetu |
| ii | Mkunga | Mnasi ukhonyanga vamama khwebolola | Muuguzi anyewasaidia kina mama kuifungua |
| iii | Mafiria | Buchafu bwa esikonzo | Uchafu wa kidonda |

Maneno haya ambayo tumeorodhesha katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi yanapotajwa moja kwa moja huzua kero na aibu miongoni mwa wahusika au wanajamii lugha. Kwa hivyo, ili

kudumisha upole miongoni mwa wazungumzaji katika muktadha wa matibabu, hasa kwenye tiba, utoaji wa ushauri nasaha, uhamasishaji na uasaji, watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi hawana budi kutumia maelezo marefu ambayo yatapunguza aibu au kero fulani.

### 4.2.2. Mkakati wa Kutumia Tashhisi

Kulingana na kamusi sanifu ya TUKI (2014) tashhisi ni usemi wa kukipa kitu kisicho na uhai sifa ya kitu chenye uhai. Mkakati wa kutumia tashhisi huhusisha watumiaji wa lugha katika jamii lugha husika kubuni majina ya viumbe fulani ambayo hutumiwa kurejelea baadhi ya magonjwa ili kuonyesha upole katika mazungumzo. Aghalabu majina hayo ya viumbe huchukua sifa za kirejelewa lakini kwa namna ambayo inadhihirisha upole. Warren (1992) alipendekeza matumizi ya mkakati huo ili kuibua tasfida kwa lengo la kuonyesha upole katika lugha.

Kwa mfano, ugonjwa wa ukimwi hurejelewa na baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili na Kimarachi ifuatavyo:

**KISWAHILI**

*Mdudu*

**KIMARACHI**

*Lubukha/ Lumoli (Mdudu mharibifu)*

Mdudu huwa na uhai na aghalabu wadudu wengi huwa waharibifu kwa mimea, wanyama na hata kwenye miili ya binadamu. Kwa hivyo, ugonjwa huu wa ukimwi hulinganishwa na mdudu fulani hasa mharibifu katika lugha ya Kiswahili na Kimarachi kutokana na uharibifu au hatari ambayo unasababisha kwenye mwili au afya ya mwathiriwa. Hali hii ya uhuishaji inapotumiwa, mbali na kutahadharisha, kuna vile vile kutisha kunakotokana na ugonjwa huu wa ukimwi.

### 4.2.3. Mkakati wa Kutumia Maneno yenye Maana Fiche

Brown na Levinson (1987) walipendekeza matumizi ya maneno yenye maana fiche kama njia mojawapo ya kudumisha upole miongoni mwa wazungumzaji wa lugha fulani.

Mkakati huu aghalabu huhusisha matumizi ya semi hasa nahau na methali ili kusema maneno au vitendo fulani kwa njia isiyo wazi kama hali ya kuonyesha upole au heshima. Matei (2011) akifafanua zaidi kuhusu semi anaeleza kuwa semi ni kauli fupi za kisanaa zenye maana na mafunzo yaliyofichika. Hata hivyo, kutokana na utafiti wetu, mkakati huu hufaulu sana miongoni mwa watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi ikiwa wahusika wanaelewa au wana ujuzi wa kutosha kufasiri maana ya semi husika. Wahamasishaji au waasaji katika Kiswahili na Kimarachi huweza kutumia semi katika hotuba zao kwenye vikao vya uhamashishaji na uasaji ili kupitisha ujumbe kwa lengo la uzuiaji wa magonjwa fulani kuenea katika jamii lugha husika.

Hebu hapa chini tutoe fafanuzi za haya tunayoyasema:

#### 4.2.3.1. Mkakati wa Kutumia Nahau

Nahau ni fungu la maneno ambayo huwa na maana tofauti na maana halisia ya maneno yaliyounda fungu hilo. Maneno fulani yanapotumiwa pamoja huibua maana mpya. Watumiaji lugha ya Kiswahili na Kimarachi hutumia mkakati huu kuibua tasfida katika muktadha wa matibabu hasa kwenye ushauri nasaha, uhamasishaji na uasaji. Mara nyingi nahau hutumiwa katika Kiswahili na Kimarachi ili kurejelea kitendo cha kufanya ngono, vitendo vya kutoa taka mwilini na hali ya kufa.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 16A**

| Neno | | Tasfida (Nahau) |
|---|---|---|
| i | Kunya | Kwenda haja kubwa<br>Kwenda haja ndefu |
| ii | Kukojoa | Kwenda haja ndogo<br>Kwenda haja fupi |
| iii | Mwanamke kuona damu | Kupata hedhi<br>Kuona mwezi<br>Kuingia katika mwezi |
| iv | Kufa | Kuaga dunia<br>Kwenda ahera<br>Kwenda jongomeo<br>Kata roho<br>Kukata kamba<br>Kushika njia ya binadamu<br>Kutoka watu<br>Kufariki dunia<br>Koma moyo<br>Kufuata njia ya marahaba |

**KIMARACHI**

**Jedwali 16B**

| | Lira | Injira ya ovupole | Tafsiri |
|---|---|---|---|
| i | Khunia | Khurusia ikhaja ikhongo<br>Khwekhonya khuhongo | Kutoa haja kubwa<br>Kujisaidia kukubwa |
| ii | Khwinyala | Khwekhonya khutiti | Kujisaidia kudogo |
| iii | Mukhasi khulola amabanga | Khuba khumwosi<br>Khulola omwosi | Kuwa katika mwezi<br>Kuona mwezi |
| iv | Khufwa | Khulekha abandu<br>Khutsia emagombe<br>Khukhalikha omwoyo | Kuacha watu<br>Kwenda emagombe<br>Kukatika moyo |

Tumepata katika utafiti huu kwamba wanajamii lugha ya Kiswahili na Kimarachi hupenda kutumia nahau kusemea mambo mazito kama vile kifo au yale ya aibu kama vile vitendo vya kufanya ngono na kutoa taka mwilini hasa katika muktadha wa matibabu. Tasfida tulizoorodhesha kwenye jedwali la **16A** na **16B** hutumiwa ili kuonyesha upole katika lugha. Hata hivyo, lazima kila mwanajamii lugha husika awe na uelewa au umilisi wa maneno hayo fiche ili aweze kutambua bayana jambo ambalo linasemwa.

#### 4.2.3.2. Mkakati wa Kutumia Methali

Methali ni semi fupi ambazo hueleza jambo au mafunzo fulani kwa kutumia mafumbo. Methali hutumiwa katika jamii lugha yoyote ile kueleza au kuwasilisha jambo fulani kwa njia fiche ili kudumisha upole katika mazungumzo. Hymes (1974) anasema kuwa kuna vijigao vya

kitamaduni kama vile methali ambazo hutumiwa katika lugha ili kuonyesha heshima. Jambo au funzo fulani lenye uzito katika muktadha wa matibabu hasa uhamasishaji na uasaji hupitishwa kwa kutumia methali ili kupunguza aibu na kero. Mifano:

**KISWAHILI**

*i. Akunyimaye tonge kakuepushia mashuzi. / Akunyimaye mbaazi kakuepushia mashuzi.*

Methali hii ina maana kuwa anayekunyima mbaazi au tonge atakuwa amekuepusha na kuchafuliwa tumbo na kuanza kujamba au kushuta. Neno *mashuzi* hutumiwa badala ya *kujamba* au *kushuta* ili kuonyesha upole katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, maana ya ndani ya methali hii ni kuwa mtu akunyimapo kitu usilalamike kwani huenda amekwepusha na taabu kubwa baadaye. Hutumika katika muktadha wa uhamasishaji au uasaji hasa kuwakumbusha vijana ambao hulalamika hasa wanaponyimwa nafasi na wazazi wao kuhudhuria sherehe fulani kiholela ambazo hatima yake huweza kuwaletea shida kubwa.

*ii. Mkware hajiingilii mwenyewe.*

Mkware ni mtu anayependa kufanya ngono ovyo ovyo ilhali kuingilia mtu ni kufanya naye ngono. Kwa hivyo, methali hii ina maana kuwa mtu malaya hawezi kufanya ngono akiwa pekee, lazima awe na mwingine. Neno *hajiingilii* hutumiwa badala ya *hafanyi ngono* ili kuonyesha upole katika lugha. Basi, mhamasishaji au muasaji katika Kiswahili anaweza kusema '*Tujiepushe na vitendo vya kuingiliana kiholela'* badala ya kusema '*Mjiepushe na ngono za kiholela.'*

**KIMARACHI**

*i. Nandaulira kalikuhira emagombe. (Asiyesikia masikio yalifungukia kuzimuni.)*

Methali hii ina maana kuwa asiyesikia mawaidha hasa ya wazee masikio yake yatafungukia kuzimuni (emagombe). Neno *emagombe* limetumiwa katika methali hii badala ya *sialo sya abafuu (nchi ya wafu)* ili kupunguza makali fulani katika lugha na hata tishio kwa hadhira katika Kimarachi. Methali hii pia hutumiwa katika uhamasishaji na uasaji kuwakumbusha Wamarachi hasa vijana kuwa wasipofuata maagizo au mawaidha ya wazee au wakubwa wao wataangamia.

*ii. Nziyukhana khayia meno. (Aliyeharakisha aliungua meno.)*

Methali hii ina maana kuwa anayekimbilia kufanya mambo kiholela au kujiingiza katika tabia mbaya bila kufikiria mwishowe aliungua meno. Maneno *'kuungua meno'* yametumiwa badala ya kutaja *kifo* au *kuambukizwa maradhi hatari kama vile ukimwi* kwa lengo la kuonyesha upole ili ujumbe uifikie hadhira lengwa bila tishio.

Mhamasishaji au muasaji katika Kimarachi husema: '*Abaraga mumanye mbu nziyukhana khayia meno'* (Vijana mjue kwamba aliyekimbilia kufanya mambo kiholela au kujiingiza katika tabia mbaya mwishowe aliungua meno), badala ya kusema: *'Abaraga mumanye mbu nimweingisia mu evima vya okhukhola ovudamba mulafwa* (Vijana mjue kuwa mkijiingiza kwenye tabia za kufanya ngono kila mara ovyo ovyo mtakufa.)

Ni dhahiri kuwa methali hutumiwa katika Kiswahili na Kimarachi kwenye muktadha wa matibabu hususan wakati wa uhamasishaji na uasaji wa wanajamii lugha husika kuhusu madhara ya tabia au maradhi fulani. Methali husaidia kupunguza makali kwenye lugha na kuifanya lugha hiyo kuwa ya upole ili kuzuia kuwepo aibu au kero kwa hadhira lengwa. Mkakati huu wa

kutumia methali hupitisha ujumbe mrefu kwa njia fupi, yenye busara na kudumisha upole katika jamii lugha husika.

### 4.2.4. Mkakati wa Ujumuishaji

Kulingana na Warren (1992) neno fulani huweza kusemwa au kuandikwa kijumla badala ya neno mahsusi. Watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili hukwepa kutaja moja kwa moja sehemu fulani za mwili hasa zile zinazohusika na maswala ya kingono au utoaji wa haja kubwa na haja ndogo mwilini na badala yake kutumia neno la kijumla *'sehemu ya siri*, au *'sehemu nyeti'*. Pia, watumiaji wa Kimarachi hutumia neno la kijumla *imberi* badala ya kutaja sehemu ya siri husika. Kwa mfano, mwanamume anaweza kumwambia muuguzi katika Kimarachi kuwa *imberi yange iri nende obufwimbe* (mbele yangu ina uvimbe) badala ya kusema kuwa *imbolo yange iri nende obufwimbe* (mboo yangu ina uvimbe). Aghalabu madaktari, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji na wanajamii husika hutumia mkakati huu wa kujumuisha ili kujiepusha na kuzua aibu au kero iwapo wangeitaja sehemu yenyewe husika moja kwa moja.

Kwa mfano, mgonjwa anayetumia Kiswahili husema kuwa *'nimeumizwa sehemu yangu ya siri au sehemu yangu nyeti'* badala ya kusema kuwa *'nimeumizwa au nimekatwa mboo yangu.'* Katika Kimarachi, mgonjwa huweza kusema: *'Imberi yange yaumiye'* (Mbele yangu imeumia) badala ya kusema kuwa '*Imbolo yange yaumiye'* (Mboo yangu imeumia).

### 4.2.5. Mkakati wa Kuunda Majina Mapya

Tumetambua katika utafiti huu kuwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi huunda baadhi ya tasfida hasa zile zinazorejelea sehemu za ziri mwilini kwa kupata nomino kutokana na kazi za sehemu fulani za siri mwilini. Mkakati huu ni sawa na ule wa uundaji wa majina mapya ambao ulipendekezwa na Warren (1992). Nomino huundwa kutokana na kazi inayofanywa na sehemu

ya siri inayohusika mwilini. Mkakati huu huwasaidia watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi kutaja sehemu husika kwa njia ambayo inaonyesha heshima au upole.

Nomino zinazoundwa kutokana na mkakati huu husaidia kupunguza kiasi cha aibu au kero katika muktadha wa matibabu hasa zinapotumiwa na wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, waasaji na wanajamii lugha husika kwa jumla. Pia, huchangia katika kudhibiti utamaduni wa jamii lugha, ambapo kila jamii lugha hujibiidisha kudumisha upole katika lugha.

**Mifano: KISWAHILI**

**Jedwali la 17A**

| **Sehemu** | | **Kazi yake** | **Tasfida** |
|---|---|---|---|
| i | Mkundu | Kunya | Kinyeo |
| ii | Matako | Kuketi | Makalio |

**KIMARACHI**

**Jedwali la 17B**

| **Isehemu** | | **Ikasi yayo** | **Injira ya heshima** |
|---|---|---|---|
| i | Munie (Mkundu) | Khunia (Kunya) | Siniero (Kinyeo) |
| ii | Madakho (Matako) | Khwikhala (Kuketi) | Mekhaliro (Makalio) |

Kutokana na matokeo ya uchunguzi wetu, tumetambua kuwa maneno *mkundu* katika Kiswahili na *munie* katika Kimarachi hayapaswi kutajwa mbele ya watu kwani huleta aibu na kero. Kwa

hivyo, nomino inayoundwa kutokana na kazi ambayo sehemu hii hufanya hutumiwa ili kuonyesha upole fulani katika lugha. Hii ndiyo sababu neno *mkundu* hurejelewa kwa tasfida *kinyeo* katika Kiswahili na neno *munie* (mkundu) kurejelewa pia kwa tasfida *siniero* (kinyeo) katika Kimarachi ili kuonyesha upole. Meneno *matako* katika Kiswahili na *madakho* (matako) katika Kimarachi pia hurejelea kwa tasfida *makalio* na *mekhaliro* (makalio) mtawalia ili kuonyesha heshima.

### 4.2.6. Mkakati wa Kutumia Sitiari

Sitiari ni mbinu katika lugha inayohusisha ulinganisho wa moja kwa moja baina ya watu au vitu viwili. Yaani, kitu kimoja huitwa kingine hasa ambapo sifa ya kitu hicho inafanana na kile kitu kingine. Mkakati huu pia ulipendekezwa na Warren (1992) kama njia ya kuibulia tasfida katika jamii lugha husika. Matumizi ya sitiari husaidia kudumisha upole katika lugha kwa sababu watu wenye tabia fulani hasi hawatajwi moja kwa moja kwa majina ya kawaida yanayorejelea tabia hizo. Pia, sehemu fulani za mwili hususan zile za siri huweza kutajwa kwa kutumia sitiari katika Kiswahili na Kimarachi. Mifano:

**KISWAHILI**

*Jamvi la wageni:* Mwanamke malaya

Jamvi ni kifaa kifananacho na mkeka ambacho watu huweza kulalia au kukalia. Jamvi la wageni hasa hutumiwa na mgeni yeyote anayekuja kukalia au kulalia. Kwa hivyo, mwanamke malaya au kahaba hufanananishwa na jamvi la wageni kutokana na tabia yake ya kukubali kufanya mapenzi au kulala na mtu yeyote yule anayemjia.

**KIMARACHI**

i. *Makina* (Mawe): Matiti ya mwanamke yaliyosimama kifuani

ii. *Ichapati* (Chapati): Matiti ya mwanamke yaliyolala kifuani

*Makina* (mawe) hutumiwa na baadhi ya watumiaji wa Kimarachi hasa vijana kurejelea matiti ya mwanamke. Hii hutokana na hali kuwa matiti ya mwanamke hasa yale yaliyosimama kifuani yanaelekeana na mkao wa mawe fulani ambayo huwa na muundo duara au bapa. Pia, neno *ichapati* (chapati) hutumiwa na vijana wanaozungumza Kimarachi kurejelea matiti ya mwanamke yaliyolala kifuani.

Sababu kuu ya kutumia maneno haya ya kiistiari ni kupunguza aibu na kero inayoweza kutokea kwa walengwa hasa kwenye vikao vya uhamasishaji au uasaji kwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi kuhusu afya yao. Ni dhahiri kuwa nahau *jamvi la wageni* hutumika kama tasfida katika Kiswahili lakini haijulikani kama tasfida ya kurejelea mwanamke kahaba katika lugha ya Kimarachi. Watumiaji wa Kimarachi huona tu kama maneno ya kawaida. Kwa upande mwingine, neno *mawe* ambalo hutumiwa kama tasfida *(makina)* katika Kiamarachi halitambuliki kama tasfida katika Kiswahili. Hii hutokea kwa sababu kila jamii lugha huwa na sheria maalum zinazowaongoza watumiaji wa lugha husika kuunda tasfida (Hymes, 1974).

### 4.2.7. Mkakati wa Kutumia Istilahi Zinazohusiana ya Matibabu

Baadhi ya wauguzi au madaktari hulazimishwa kutumia istilahi kwenye taaluma ya matibabu katika Kiswahili ambazo wagonjwa wengi hawafahamu maana yake nzito. Allan na Burridge (1991) wanautambua mkakati huu kama njia ya kuundia tasfida kwenye muktadha wa matibabu.

Sababu ya kutumia istihali kama hizi huwa kumfanya mgonjwa aelewe tu kuwa anapewa tiba au dawa fulani kama njia ya kumtibu kusudi maumivu yake yapungue au yaishe mwilini. Mifano:

**Kiswahili**: *Nusu kaputi*

Nusu kaputi ni dawa ambayo mgonjwa hupewa hospitalini wakati wa upasuaji kumfanya apoteze fahamu ili asihisi uchungu anapofanyiwa upasuaji huo. Muuguzi au daktari hukwepa kumweleza mgonjwa kuwa atampa dawa ya kumfanya apoteze fahamu kwa sababu kauli kama hii huweza kumtishia mgonjwa na kumwongezea maumivu zaidi au hata akashtuka sana. Zaidi ya hayo, mgonjwa huyo atakuwa na wasiwasi kuwa huenda akafa. Kwa hivyo, istilahi *nusu kaputi* inayotumiwa kwenye taaluma ya matibabu hususan katika kitengo cha upasuaji hutumiwa katika Kiswahili ili kuondoa tishio kwa mgonjwa husika.

### 4.2.8. Mkakati wa Kutumia Nyimbo

Tulipata katika utafiti wetu kuwa baadhi ya wahamasishaji au waasaji katika lugha ya Kimarachi hutunga nyimbo wanazotumia kupitisha ujumbe fulani kwa hadhira lengwa kwa njia ya upole. Nyimbo hizi aghalabu huimbwa kwenye vikao vya uhamasishaji au uasaji kama njia mojawapo ya kuwajuza au kuwatahadharisha wanajamii kuhusu tabia fulani zinazoweza kuwatumbukiza kwenye magonjwa hatari kama vile ukimwi. Nyairo (2005) anasema kuwa nyimbo au muziki huwa na athari fulani kwa maisha ya Wakenya wenye umri tofauti tofauti.

Nyimbo hizi hutumiwa kutokana na sababu kuwa ujumbe wake si wa kulazimisha na haulengi mtu mahususi au kundi fulani la watu. Isitoshe, hadhira huweza kuimba kwa pamoja kama burudani lakini ujumbe fulani ukawafikia kwa njia hii wakiwa wamefurahishwa na mahadhi ya wimbo husika. Mifano:

**<u>Wimbo 1</u>**

**Kimarachi**

*Abaraga mube chonjo, mube chonjo ×2*

*Daktari wa obulwaye buhongo abulao,*

*Malesi kobukimwi kabulao.*

*Abaraga muletsira ×2*

*Daktari wobukimu abulao,*

*Malesi ka bukimu kabulao*

**Tafsiri (Kiswahili)**

*Vijana muwe chonjo, muwe chonjo ×2*

*Daktari wa ugonjwa mkubwa hayuko*

*Tiba ya ukimwi haipo*

*Vijana mtaendesha×2*

*Daktari wa ukimwi hayupo*

*Tiba ya ukimwi haipo×2*

**<u>Wimbo 2</u>**

**Kimarachi**

*Basiani na bakhana mwelinde,*

*Bulwaye bukhongo bwetsere bumala abandu×2*

**Tafsiri (Kiswahili)**

*Wavulana na wasichana mjilinde,*

*Ugonjwa mkubwa umekuja unamaliza watu×2*

Wimbo wa kwanza na ule wa pili ni baadhi ya nyimbo ambazo huimbwa katika Kimarachi hasa katika vikao vya uhamasishaji na uasaji kuhusu ukimwi ili kupitisha ujumbe kwa wanajamii kwa lengo la kuzuia uenezaji wa ukimwi.

Baadhi ya wahamasishaji na waasaji katika Kimarachi hutumia mkakati huu ili kuihusisha hadhira lengwa katika mazungumzo yao kusudi ujumbe uwafikie kwa njia ya burudani na upole. Isitoshe, watumiaji wa Kimarachi wanapoelewa nyimbo kama hizi huendelea kuziimba au kuwaimbia wengine hali ambayo huwakumbusha jambo muhimu kuhusu uzuiaji wa ugonjwa hatari wa ukimwi.

**Mfano wa wimbo katika Kiswahili**:

*Watu wengi bado wanajiuliza juu ya ugonjwa huu,*
*Unaomaliza watu katika dunia hii.*
*Waganga wamejitahidi hawajapata madawa*
*Mungu tusaidie, tunakulilia ×2*
*(Mtunzi: Alfred Osonga)*

Wimbo huu unapoimbwa au kuchezwa huwa na ujumbe wa kutahadharisha hadhira husika kuhusu ugonjwa wa ukimwi kwa njia ya upole. Hali hii huwafanya wahusika kuchukua hatua za kujiepusha na tabia zinazoweza kuwatumbukiza kwenye janga la ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Maneno *'unaomaliza watu'* yametumiwa katika wimbo huu badala ya kusema

*'unaowaua watu'* ili kupunguza tishio fulani kwa hadhira. Hii ni kwa sababu neno *kumaliza* hueweza kumaanisha mtu kukonda tu au kuishiwa na nguvu.

### 4.2.9. Kubadilisha Mpangilio wa Sauti au Silabi katika Neno

Sauti au silabi za maneno huweza kubadilishwa ili kupata neno lenye muundo tofauti na muundo wa maneno katika lugha husika kwa lengo la kupata tasfida. Mkakati wa kubadilisha mpangilio wa sauti na silabi katika neno ulipendekezwa na Warren (1992). Mkakati huu pia unaitwa kuunda upya (Allan na Burridge, 1991). Baadhi ya vijana tuliowahoji katika lugha ya Kimarachi hususan wale walio na umri wa miaka 18 hadi 35 walisema kuwa wao huweza kubadilisha mpangilio wa sauti au silabi hasa wanapozungumza na wenzao katika vikao vya kuhamasishana au kuasana kuhusu tabia fulani zinazoweza kusababisha uenezaji wa maradhi ya ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa kama vile kaswende na kisonono. Wao hufanya hivyo ili kuficha makali ya maneno fulani hasa yanayorejelea sehemu za siri mwilini au vitendo vya kufanya ngono.

Mpangilio wa silabi unapobadilishwa katika neno, maana ya neno hilo hupotea na kuifanya lugha wanayozungumza kuonekana kama lugha ngeni kwa watumiaji wengine wa Kimarachi wakiwemo watoto na wazee. Kwa kufanya hivi, huwa wametumia lugha kwa njia ya upole lakini ujumbe kuhusu matibabu umeeleweka miongoni mwao kama kundi la vijana. Tulipata mifano ifuatayo katika lugha ya Kimarachi:

**Jedwali la 18 A**

| (Lira) Neno | | Neno lililobadilishwa sauti au silabi |
|---|---|---|
| i | Imbolo (Mboo) | Lomboi |
| ii | Maneke (Makende) | Kenema |
| iii | Lwena (Kuma) | Nalwe |
| iv | Tsimbere (Matiti) | Rembetsi |
| v | Madakho (Matako) | Khodama |
| vi | Vukimu (Ukimwi) | Mukivu |

Baadhi ya vijana pia hutumia mkakati huu katika Kiswahili ifuatavyo:

**Jedwali la 19**

| Neno | | Neno lililobadilishwa sauti au silabi |
|---|---|---|
| i | Ukimwi | Mwikiu |
| ii | Kunya | Nyaku |
| iii | Kuhara | Rahaku |
| iv | Kaswende | Ndesweka |

### 4.2.10. Mkakati wa Kutosema

Huu ni mojawapo ya mikakati mitano iliyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) kama njia ya kudumisha upole miongoni mwa watumiaji lugha husika. Baadhi ya watumiaji lugha za

Kiswahili na Kimarachi huweza kukosa kusema au kuzungumza kuhusu sehemu fulani za siri mwilini, magonjwa, vitendo vya aibu, hali za watu na takamwili mbalimbali hadharani kama njia ya kujiepusha na kuzua aibu, kuwaudhi au kuwakera wenzao.

Ingawa mkakati huu huonekana kama tasfida, unaweza kuzuia shughuli za matibabu kwa wanajamii kwani waathiriwa hawataeleweka na wauguzi au watoa ushauri nasaha. Zaidi ya hayo, wahamasishaji na waasaji hawataweza kutimiza kazi zao kikamilifu wasipotaja masiala fulani hasa yale yanayoambatana na uenezaji wa magonjwa fulani miongoni mwa binadamu.

Kwa mfano, watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi huogopa kutaja ugonjwa wa ukimwi na saratani kiholela kutokana na dhana kuwa watu wengi wanaogunduliwa kuwa na ugonjwa huo huchukuliwa kama wafu katika jamii lugha zao. Alembi (2002) anaeleza kuwa watu wanaojulikana kuwa wanaugua ukimwi katika jamii ya Abanyore hutengwa na wenzao na hata kuonwa kama wafu ambao wanatembea.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wanajamii lugha hujiepusha na kuzungumzia vitendo vya mwanamume au mwanamke kufanya mapenzi nje ya ndoa au kukataa kusema hata ikiwa sehemu zao za uzazi zina matatizo kwa kuhofia kuwa huenda wenzao wakawacheka au kuwakejeli kwa kutokuzingatia mbeko.

### 4.2.11. Mkakati wa Kutumia Ishara za Mikono

Kulingana na mahojiano tuliyofanya na baadhi ya wazee katika jamii lugha ya Wamarachi, tulibaini kuwa watu wengine hupendelea kutumia ishara za mikono kurejelea au kuashiria hasa sehemu fulani za siri mwilini.  Wao hufanya hivyo kwa sababu ya kuogopa kutaja jina la sehemu yenyewe kulingana na aibu au kero watakayozua kwa wasikilizaji wao. Huu ni mkakati ambao

tuligundua kutokana na utafiti wetu kuwa hutumika sana na Wamarachi katika muktadha wa matibabu hasa tiba na ushauri nasaha.

Pia, baadhi ya wauguzi walieleza kuwa kunao wagonjwa ambao huashiria mahali sehemu fulani ya siri ipo badala ya kuitaja kwa jina lake. Hii ni kwa sababu wanaofanya hivyo huona kwamba watazua aibu au kumkera muuguzi iwapo watataja sehemu hiyo ya siri moja kwa moja hasa ikiwa muuguzi huyo ni wa jinsia tofauti au anamshinda mhusika kwa umri.

### 4.2.12. Mkakati wa Kubadilisha Kategoria ya Neno

Mkakati huu ulipendekezwa na Warren (1992) kama njia mojawapo za kuundia tasfida. Neno fulani huenda likabadilishwa na kuchukua kategoria nyingine kwa lengo la kuficha makali yake. Hali hii hutokea sana katika kutaja nomino za sehemu za siri kwenye mwili wa binadamu. Kwa mfano, badala ya mgonjwa kusema *'mboo yangu ina kidonda'* katika Kiswahili yeye huelekea kusema *'kule kuna kidonda'* ambapo neno *kule* ni kiwakilishi cha neno *mboo.* Watumiaji wa Kimarachi pia huweza kubadilisha kategoria ya neno fulani ili kuonyesha upole. Kwa mfano, mgonjwa wa kike anapomwambia daktari kuwa *'alya vinjakala'* (pale pananiwasha) badala ya kusema kuwa *'tsimbere tsinjakala'* (matiti yananiwasha) huficha aibu na kuonyesha upole.

### 4.2.13. Mkakati wa Kuibua Maana Mpya za Maneno

Warren (2009) pia alipendekeza kuwa tasfida huweza kuibuliwa kwa kubuni maana kwenye maneno fulani ambayo tayari yapo. Kutokana na mkakati huu, neno fulani ambalo hutumiwa na wanajamii lugha husika huweza kutanuliwa kimaana ili kupata tasfida za kutajia matendo au mambo mbali mbali ambayo huzua aibu na kero yanapotajwa moja kwa moja. Tumetambua katika utafiti wetu kuwa maneno fulani katika Kiswahili na Kimarachi hutanuliwa kimaana ili kuunda tasfida za kutumia katika muktadha wa matibabu. Mifano:

**Kiswahili:** *Kuungua*

Maana asilia ya neno *kuungua* ni *kuchomeka*. Kwa mfano, nyumba inaposhika moto huungua. Chakula pia huweza kuungua motoni ikiwa chungu hakitaepuliwa kwa wakati ufaao. Mtu anapoungua aghalabu huhisi uchungu na hata kuwa na mabaka mwilini. Neno *kuungua* hutumiwa kama tasfida ya kurejelea ugonjwa wa kisonono au kaswende kwa sababu ugonjwa huo husababisha uchungu au mwasho mkali kwenye mwili wa mgonjwa ambao humfanya ahisi kuwa anachomeka. Pia, huweza kuacha vidonda mwilini.  Kwa msingi huu, neno kuungua hupata maana mpya.

**Kimarachi:** Khufubula

Maana asilia ya neno *khufubula* katika Kimarachi ni kutoa ugali kwenye sufuria baada ya kuiva hasa kwa kugeuza sufuria na kuufanya au kuulazimisha ugali huo kuanguka kwenye sahani. Neno hilo hutumiwa kama tasfida kurejelea hali ya mwanamke kutoa mimba kimaksudi kutokana na hali kuwa mwanamke husika hutumia mbinu mbalimbali kulazimisha mtoto kutoka tumboni. Kwa hivyo, neno khufubula hupata maana hiyo mpya.

### 4.2.14. Mkakati wa Kutumia Kinaya

Kwa mujibu wa Warren (1992), mkakati huu huhusisha kuita kitu fulani kibaya au kinachowachukiza watu kwa kutumia kinyume chake. Pia, kitu fulani kibaya huweza kuitwa kwa kutumia kitu kingine kinachokaribiana nacho ambacho ni kizuri mbele ya watu. Hii ni kwa sababu kitu hicho kizuri hakizui aibu, kero au chukizo mbele ya watu. Kwa mfano, mtumiaji wa Kiswahili huweza kusema mbele ya muuguzi kuwa *'mimi huhisi maumivu ninapotoa haja kubwa kwenye afisi ndogo*' badala ya kusema kuwa *'mimi huhisi uchungu ninapokwenda kunya chooni*. Vile vile, baadhi ya watumiaji wa Kimarachi pia husema kuwa *'ndolanga obutsuni ninzia*

*okhurusia obunyaka mu iofisi yefwe'* (mimi huhisi maumivu nikienda kutoa kinyesi kwenye ofisi yetu) badala ya kusema kuwa *'ndolanga obutsuni ninzia okhunia mu ichoo'* (mimi huhisi maumivu nikienda kunya chooni). Mkakati huu aghalabu hutumiwa na wanauwili lugha na wanawingi lugha katika jamii lugha ya Waswahili na Wamarachi kwa sababu wao wamesoma na wana uwezo wa kubuni tasfida kutoka kwenye lugha ya Kiingereza au Kiswahili na kuzitumbukiza katika lugha yao kama vile Kimarachi.

Neno *choo* katika Kiswahili linarejelewa kiheshima kwa neno linalomaanisha chumba kizuri, safi na kinachopendeza cha kufanyia kazi ambacho huitwa *ofisi. Pia,* neno *iofisi yefwe* (ofisi yetu) katika Kimarachi hutumiwa badala ya neno la kawaida *ichoo* ili kuonyesha upole katika lugha. Maneno hayo ya upole *ofisi* katika Kiswahili na *iofisi yefwe* (ofisi yetu) katika Kimarachi hutumiwa katika muktadha wa matibabu ili kuficha aibu. Ofisi ni mahali ambapo watu hufanya kazi aghalabu kila siku na hukaa mle kwa muda mrefu kwani mazingira yake safi huruhusu wahusika kufanya hivyo. Basi, inakuwa kinaya jina hili linapotumiwa kurejelea choo ambapo ni vigumu mtu kukaa ndani kwa muda mrefu sana bila kuathirika kwa namna fulani.

## 4.3. Hitimisho

Kuna mikakati mbalimbali iliyopendekezwa na Warren (1992) ambayo wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na Kimarachi hutumia ili kuunda tasfida za matibabu. Hata hivyo, imebainika katika utafiti huu kuwa kuna mikakati mingine zaidi kama vile matumizi ya nyimbo na ishara za mikono ambayo wazungumzaji wa Kiswahili na Kimarachi hutumia kuundia tasfida kando na ile iliyopendekezwa na Warren (1992) na ile ya Nichol (2011). Mikakati hii ya uibuaji wa tasfida huweza kufanana au kutofautiana katika jamii lugha moja na nyingine. Mkakati wa kutumia

maelezo marefu na ule wa kutumia lugha fiche hasa nahau na methali ndiyo hutumiwa sana katika uibuaji wa tasfida nyingi miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi. Hii ni kwa sababau tasfida zinazobuniwa kutokana na mikakati hiyo huonyesha kiasi kikubwa cha upole katika lugha. Zaidi ya hayo, mkakati wa kutumia maelezo marefu na lugha fiche huwa rahisi kutuniwa na hujenga ubunifu katika lugha.

Kutokana na utafiti huu, tumegundua pia kuwa mikakati inayotumiwa katika uundaji wa tasfida hasa katika Kimarachi aghalabu hutegemea umri wa wahusika. Kuna mikakati ambayo hutumiwa sana na vijana wa makamu kuundia tasfida. Kwa mfano, mkakati wa kubadilisha mpangilio wa sauti na silabi katika maneno ili kupata maneno ambayo hueleweka miongoni mwao pekee. Maneno hayo hueleweka tu miongoni mwa hao vijana pekee ingawa huonwa kama tasfida wakati wanahamasishana au kuasana kuhusu ugonjwa hatari kama vile ukimwi. Mfano ni neno *mukivu* ambalo hutokana na neno *vukimu* (ukimwi). Kwa upande mwingine, wazee hutumia sana mkakati wa maana fiche kuundia tasfida kwa sababu wao wana uelewa mkubwa wa nahau na methali zinazopatikana katika utamaduni wa Kimarachi. Isitoshe, mkakati wa kutumia kinaya na istilahi za kimatibabu mara nyingi hutumiwa na wanauwili lugha au wanawingi lugha ambao wana elimu ya kiwango cha juu kidogo au juu zaidi. Picha hii inaonyesha kuwa swala la elimu huathiri matumizi ya mikakati fulani ya kuibulia tasfida za matibabu katika jamii lugha ya Waswahili na Wamarachi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO

## 5.1. Utangulizi

Baada ya kuchanganua data tuliyopata katika utafiti wetu, sura hii inalenga kuonyesha muhtasari wa matokeo kwa kurejelea madhumuni ya utafiti huu, changamoto zilizoshuhudiwa na kutoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada ambayo tumeshughulikia.

## 5.2. Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu umeongozwa na madhumuni haya makuu:

i. Kubainisha tasfida ambazo zinapatikana kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

ii. Kutambua iwapo kuna mfanano au tofauti zozote za tasfida zinazotumiwa kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

iii. Kuchunguza mikakati inayotumiwa kuibua tasfida za muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa kunazo tasfida nyingi zinazotumiwa kutajia magonjwa mbalimbali, takamwili, vitendo vya kutoa takamwili, vitendo vya kufanya ngono, sehemu za siri mwilini, kifo, kazi za watu na hali za watu katika muktadha wa matibabu hasa tukizingatia tiba ushauri nasaha, uhamasishaji na uasaji. Hata hivyo, ilibainika kuwa *kitendo cha ngono* na *kifo* huwa na tasfida nyingi sana ambazo hutumiwa katika Kiswahili na Kimarachi.

Pia, vitendo vya kutoa taka mwilini kama vile *kunya, kuhara, kukojoa, kutoa manii* na *msichana kuona damu* huwa na tasfida mbalimbali za kuvitajia kwenye muktadha wa matibabu katika lugha hizi tafitiwa. Hali hii hutokana na juhudi za kila mwanajamii kutaka kudumisha usafi katika lugha, kuficha aibu, kuonyesha heshima mbele ya watu, kumpa mgonjwa anayetibiwa matumaini hata ikiwa amezidiwa sana na ugonjwa na kudumisha amani miongoni mwa wanajamii. Kulingana na Hymes (1974) kila jamii huwa na sheria ambazo huongoza watumiaji lugha husika kuzungumza lugha yenye heshima.

Kitendo cha kufanya ngono kina tasfida nyingi za kukirejelea kwa sababu mada kuhusu ngono huonekana kuwa ya siri kubwa na kaikosi kujajidiliwa na wanajamii, hivyo kusababisha uibuaji wa tasfida nyingi na hata mpya (Giddens, 1992). Watumiaji wa Kiswahili na Kimarachi hutumia tasfida katika muktadha wa matibabu kutajia kitendo cha ngono ili kukwepa aibu au kuwakera wengine.

Tasfida nyingi zinazotumiwa kwenye muktadha wa matibabu katika Kiswahili na Kimarachi zinafanana pakubwa. Kwa mfano, tasfida zinazotumiwa kutajia baadhi ya magonjwa, takamwili, vitendo vya kutoa taka mwilini, sehemu za siri mwilini, kitendo cha kufanya ngono, kutoa mimba, kufanya mapenzi nje ya ndoa, kifo, hali za watu, mwanamke aliye na mimba na kitendo cha mwanamke kuzaa zinafanana pakubwa. Sababu ya tasfida hizi kuelekeana pakubwa ni kuwa lugha hizi mbili; Kiswahili na Kimarachi ni za aina ya nasaba ya Kibantu.

Tumetambua pia kuwa tasfida zinazotumiwa hasa katika Kimarachi hutegemea maswala mbalimbali kama vile viwango vya elimu, jinsia, makazi ya wanajamii hasa ikiwa mjini au mashambani, umri na lugha ambazo wanajamii husika wanazifahamu. Zaidi ya hayo, mikakati inayotumiwa kuibulia tasfida pia hutegemea kwa kiasi fulani umri wa wahusika na viwango

vyao vya elimu. Kwa mfano, watumiaji wa Kimarachi ambao ni wanauwili lugha au wanawingi lugha huwa na uwezo mkubwa wa kuibua tasfida nyingi kwa kutumia mikakati mbalimbali ikilinganishwa na wale ambao ni wanaumoja lugha.

Utafiti wetu ulibaini kuwa mikakati mbalimbali hutumiwa kuibua tasfida katika Kiswahili na Kimarachi. Tuliweza kubaini mikakati kumi na minne ambayo hutumiwa katika uundaji wa tasfida katika lugha hizi tafitiwa. Mkakati wa kutumia maelezo marefu kurejelea neno fulani na ule wa kutumia maneno yenye maana fiche kama vile nahau na methali ndio hutumika sana kuibua tasfida katika Kiswahili na Kimarachi. Hii ni kwa sababu mikakati hii huwa rahisi kutumiwa katika kuunda tasfida au kuwasilisha maneno fulani kwa njia ya heshima au upole.

## 5.3. Changamoto

Utafiti huu umekumbwa na changamoto mbalimbali. Changamoto nyingi zilitokea nyanjani wakati wa kukusanya data katika lugha ya Kimarachi. Watu wengi wanaozungumza lugha ya Kimarachi hawakuweza kujibu au kuandika majibu yao katika lugha ya Kimarachi wakidai kuwa huwawia vigumu kusoma na hata kuandika katika lugha hiyo. Pia, watafitiwa wengine waliopatikana walikataa kujaza hojaji zetu za utafiti wakidai kuwa lugha iliyokuwemo ni chafu hasa maneno yanayorejelea takamwili, vitendo vya kutoa takamwili, maswala ya ngono na sehemu za siri mwilini. Hata hivyo, baadhi ya watafitiwa walikubali kujaza hojaji baada ya kuelezwa na mtafiti kwa uwazi zaidi madhumuni na umuhimu wa utafiti huu.

Zaidi ya hayo, watafitiwa wengine hawakujaza sehemu zote ilivyohitajika katika hojaji kwa sababu hawafahamu tasfida zinazotumiwa kutajia mambo husika. Hata wachache walipoteza hojaji walizopewa ambapo ilimbidi mtafiti mwenyewe kuwauliza maswali moja kwa moja na kunakili majibu yao. Mahojiano yaliyofanywa yaliendelea vizuri isipokuwa wazee wachache

ambao walidai kuwa baadhi ya maswali tuliyowauliza yalihusisha lugha chafu ambayo haifai kutumiwa ovyo ovyo kulingana na mila, desturi na itikadi za watumiaji wa lugha ya Kimarachi.

Muda niliokuwa nao wa kukusanya data kuhusu lugha ya Kimarachi nyanjani na ile ya Kiswahili kwa kusoma vitabu tofauti vilivyoandikwa katika Kiswahili sanifu ulikuwa mchache. Hata hivyo, nilijitahidi niwezavyo ili kupata data ambayo nimeorodhesha na kuichanganua katika utafiti huu.

## 5.4. Mapendekezo

Tumetambua katika utafiti wetu kwamba baadhi ya wanajamii lugha hasa wale wanaotumia lugha ya Kimarachi hawafahamu tasfida za kutumia hasa kutajia magonjwa fulani, sehemu za siri na vitendo fulani kama vile vya kutoa takamwili katika muktadha wa matibabu. Jambo hili huwafanya wengine wao kutosema shida au hali zinazowakumba kiafya mbele ya muuguzi au mtoa ushauri nasaha kwa sababu ya kuficha aibu. Kwa hivyo, machifu wa jamii lugha hii pamoja na wazee wa baraza wanaweza kuchukua hatua ya kuandaa vikao vichache kwa mwaka ili kuwafunza wanajamii hususan vijana tasfida ambazo wanapaswa kutumia katika muktadha wa matibabu na hata miktadha mingine ya matumizi ya lugha katika jamii.

Utafiti huu umehusu ulinganishi na ulinganuzi wa tasfida za matibabu katika Kiswahili na Kimarachi kwa kuongozwa na nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ya Dell Hymes (1974) na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Tunapendekeza kuwa utafiti mwingine unaweza kufanywa ili kubaini tasfida zaidi zinazotumiwa katika muktadha wa matibabu hasa kwa kurejelea vifaa vinavyotumiwa katika matibabu na sehemu maalum kwenye mazingira ya matibabu hususan hospitalini. Utafiti wetu umehusu tasfida za muktadha wa matibabu lakini haujazungumzia aina za tasfida zinazotumiwa katika muktadha wa matibabu katika Kiswahili na

Kimarachi, swala ambalo linaweza kuangaziwa na watafiti wengine. Pia, uchunguzi unaweza kufanywa ili kubaini tasfida zinazotumiwa kwenye sherehe za kupasha tohara, mazungumzo ya vijana, mazishini, sherehe za arusi, nyimbo za Kimarachi, semi za Kimarachi na vikao vya kupeleka posa katika Kimarachi kwa kutumia nadharia ya Brown na Levinson au nadharia nyingine ya upole.

## MAREJELEO


Alembi, E. (2002). *The Construction of the Abanyole Perceptions on Death Through Oral Funeral Poetry*. Datacom Helsinki.

Allan, K na Burridge, K. (1991). *Euphemisms and Dysphemism: Language used as Shield And Weapon*. Newyork. Oxford University Press.

Allan, K na Burridge, K. (2006). *Forbiden Words: Taboo and the Censoring of Language*. Cambridge, UK; Newyork: Cambridge University Press.

Andodo, M.A. (2015). *The Kisa Verb Phrase*. International Journal of English and Linguistic Research. Volume 3.

Angogo, K. R (1983). *Unity in diversity; Alinguistic survey of the Abaluhya of Western Kenya.* Wien, Afro-publishers.

Brown, P na Levinson, S, (1987). *Politeness. Some Universal in Language Usage.* Cambridge. Cambrige University Press.

Buliba, A, Njogu, K na Mwihaki, A (2006). *Isimu jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Chiragdin, S na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi. Oxford Publishers Press.

Fromkin, Victoria et al. (1990). *An Introduction to Language*, Second Australian Edition. Routledge.

Giddens, A. (1992). *The Transformation of Intimacy: Sexuality, love and eroticism in modern Society*. Cambridge. Polity Press.

Goffman, E, (1976). *Interaction Ritual. Essays on Face to Face Behaviour*. Newyork. Anchor Books.

Guthrie M (1970). *Comparative Bantu; An introductionto thé comparative linguistics And pre-history of the Bantu Languages.* Vol. 3. Farnborough: Gregg International

Publishers.

Gumaa, A and Shi, A. (2012). *Softboiled speech: A contrastive Analysis of Death Euphemisims In Egyptian Arabia and Chinese.* International research Journal: Global Journals Inc. (USA).

Gura, A. (2005). *Coitus in the Symbolic Language of Slavic Culture*. ???

Grice, H.P. (1975). *Logic and Conversation. Syntax anD Semantics*. vol.3. Eds. P. Cole and JL. Morgan. Newyork. Academic Press.

Habwe J, na Karanja P. (2004). *Misingi ya Sarufi*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Harry, H. (1954). *Language in Culture*. Chicago. The University of Chicago Press.

Herbert, A. (2016) *The Role of Euphemisms in Healthcare Communication.* Journal of Healthcare. Volume 1. No. 2.14.

Hickey, R. (2012). *The Handbook of Language Contact*. London. Wiley-Blackwell Publishers.

Hymes, D. (1964). *A language, Culture and Society*. New York. Harper and Row Publishers.

Hymes, D. (1972). *Models of the interaction of language and social life*. In J. Gumperz & D.

Hymes, D. (1974). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Iribemwangi, P na Mukhwana A, (2011). *Isimujamii.* Nairobi. Focus Publishers.

Khanfar, A. (2002). *Euphemism in Arabic: Typology and Formation.* Journal of the College of Arts. University of Basrah. No. (61) 2012.

Leech, G.N. (1974). *Semantics*.  Harmondsworth. Middlesex, England.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics; An Introduction*. Cambridge. Cambridge University

Press.

Mashiri, P. et al (2012). *Ethical Foundatiions of HIV/AIDS Shona Vocabularies*. University of Zimbabwe.

Momanyi, C. (2004). *Urban Disparities in HIV/Aids Infection; the bugged Towns of Kenya*. In: C. Momanyi et al. (eds.). pp. 102-105.

Mugenda, O na Mugenda, A. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative* Approaches. Nairobi. Acts Press.

Ndalu, A na King'ei, K.G. (1988). *Kamusi ya Semi za Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Limited.

Nguti, M. (2013). *Ulinganishi wa Matumizi ya Tasfida za Muktadha wa Nyumbani katika Lugha ya Kikamba na Kiswahili*. Unpublished MA Thesis. University of Nairobi.

Nichol, M. (2011). *7 Types of Euphemisms.* Retrieved from http://www.dailywritingtips. Co/7-types-of-euphemisms.

Njoroge, R na Mukhwana, A. (2015). *Euphemism on Body Effluvia in Kikuyu*. International Journal of Humanities and Social Sciences and Education. Volume 2.

Njoroge, R.N. (2014). *Euphemisms for Taboo Words in Kikuyu.* Unpublished MA Thesis. University of Nairobi.

Nyairo, J. 2005. *"Zilizopendwa": Kayamba Afrika's use of cover versions, remix and sampling In the (re) membering of Kenya*. Africa Studies 64. 1:29-54.

Omosa, F.N. (2015). *Tasfida kama Mkakati wa Upole: Uwiano wa Tasfida za Kiswahili na Ekegusii.* Unpublished MA Thesis. University of Nairobi.

Rawson, H. (1995). "*A dictionary of Euphemism and Other Doublespeak*". Retrieved from http//www.thrfcc.ora/euphemism17822.html//

Roohul-Amini, M. (1989). *Outline of Culture*. Tehran: Atar Press.

Saussure, F. de. (1974). *Course in General Linguistics*. tr. Wade Baskin, London: Fontana.

Tengku na Sepideh (2012). *Language and Culture.* Internatonal Journal on Humanities and Sciences. Vol. 2.

TUKI (2006). *English Swahili Dictionary*. ($3^{rd}$ edition). Dar-es-Saalam. TUKI.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*University of Dar-es- Salaam and Oxford University Press.

Wambua, R.S. (2009). *Variation in Dialectical use of and Attitudes towards Taboo words and Euphemism in Kikamba*. Unpublished MA Thesis. University of Nairobi.

Wamitila, K.W. (2000). *Kamusi ya Misemo na Nahau*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Watts, R. J. (2003). *Politeness.* Cambridge: Cambridge University Press.

Whiteley, W.H. (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: IKHOJAJI (KIMARACHI)

Esie ndi mwanafunzi mu Univasti ya Nairobi wa someranga idigrii ya masters mu Luswairi. Iriwo ipicha yechesia mbu vadaktari, vanaafya, valwaye nende vanajamii mu jumla vakosanga makhuwa ka ovupole kabekhonyera khwelesia ebindu bilondokhana nende obusirishi. Khusaba mbu ojaze ikhojaji ino shinga olwa vinyikhana na majibu kao kalarukhonya khukamilisia ikasi ino. Khusaba mbu olandika tawe elira lyao khu likaratasi lino.

### Sehemu A

Chagua lijibu lala mu isehemu ya (a), (b), (c) nende (d) halafu ochore isako khu lijibu lya ochaguwe.

**1. (a) Miaka**

i. 18-30 ii. 31-40

iii. 41-50 iv. 51 - Zaidi

**(b) Wesisatsa/ Wesikhasi**

i. Wesisatsa ii. Wesikhasi

**(c) Siako sya masomo**

ii. Primari ii. Sekondari

iii. Ikoleji iv. Univasti

**(d) Avundu wa omenyanga**

i. Mulukongo/Muvileji ii. Mutauni

**(e) Ikasi** …………………………………………………………………………….

## Sehemu B

Jaza makalusio kao/majibu kao mu inafasi ya oberesibwe. (Ihali ya obusishirishi ilondokhana nende obusirishi bwa musivitali, khukansola mundu/ mulwaye, khwechesia nende khukerera abandu khulondokhana nende afya.)

**2.** (a) Yandika malyaye kano shinga lwa kalangungwa mu injira ya heshima au irarisia tawe mu ihali ya obusirishi.

| **Vulwaye** | | **Injira ya okhuvulanga mu vupole/heshima** |
|---|---|---|
| i. | Vukimu | |
| ii. | Bulwaye budiranga imberi ya omundu khulondokhana nende khukhola mapenzi ovyo ovyo (Kaswende) | |
| iii. | Tsingakha | |
| iv. | Busumwa | |
| v. | Kansa | |
| vi. | Khunyalala | |
| vii. | Gonoria | |
| viii. | Bulwaye bwa esirifu | |
| ix. | Bulyaye bwa munie khufwimba alafu mabanga khudatsa (Bawasiri) | |
| x. | Bulwaye bwa omwoyo | |
| xi. | Bulwaye bwa ipresha | |

**Maelezo:** Gonoria *(Gonorrhoea),* Kaswende *(Syphilis),* Bawasiri *(Haemorrhoids),* Bulwaye bwa esirifu *(Tuberculosis),* Bulwaye bwa ipresha *(High blood pressure)*

(a) Khubera sina mera kawakhandika ako kekhonyerwanga khulanga malwaye ako?

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**3.** Bikhole bino bilangungwa birye mu injira ya heshima, irarisia tawe au khurera aibu mu ihali ya obusirishi?

| | | |
|---|---|---|
| i. | Khuba isindano | |
| ii. | Khwibusia mukhasi | |
| iii. | Khwara mulwaye | |
| iv. | Khukheba | |

**4.** (a) Yandika mera kekhonyerwanga khulanga bikhole bino mu injira yechesia heshima au vupole mu ihali ya obusirishi.

i. Khwibula

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

ii. Khwinyala

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

iii. Khunia

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

iv. Khunyalala

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

v. Mukhana khurusia omwana

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………....

vi. Khukhola mapenzi

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

vii. Khusala

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

viii. Khwinyamba

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

ix. Mukhana khulola mavanga

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………...

x. Khurusia spamu

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

xi. Musatsa khukhola mapenzi nende musatsa wasie

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

xii. Mukhasi khukhola mapenzi nende mukhasi wasie

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

xiii. Khuva nende mupango kwa kando

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(b) Khubera sina mera akawakhandika ako kekhonyerwanga?

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**5.** (a) Tsisehemu tsino tsia mubiri tsilangungwa tsirie mu injira yechesia heshima mu ihali ya obusirishi?

| **Isehemu** | **Lira liechesia heshima au vupole** |
|---|---|
| i. Imbolo | |
| ii. Lwena | |
| iii. Munie | |
| iv. Madakho | |
| v. Tsimbere | |
| vi. Maneke | |
| vii. Vwoya | |

(b) Khubera sina mera akawakhandika ako kekhonyerwanga?

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**6.** (a) Mera sina kekhonyerwangwa mu injira ya heshima khulanga buchafu buno burula mumubiri kwa omundu mu ihali ya obusirishi?

i. Mafwi ………………………………………………………………………………………

ii. Manyi ………………………………………………………………………………………

iii. Mavanga ……………………………………………………………………………………

iv. Spamu ……………………………………………………………………………………...

v. Mafiria ……………………………………………………………………………………...

vi. Lulehe ……………………………………………………………………………………

vii. Masasi ……………………………………………………………………………………...

viii. Mamira ……………………………………………………………………………………..

ix. Mare ……………………………………………………………………………………….

(b) Khubera sina mera akawakhandika ako kekhonyerwanga?

………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………....

**7.** Abandu bano balangungwa barie mu injira yechesia vupole au heshima mu ihali ya obusirishi?

| | | |
|---|---|---|
| i | Mulalu | |
| ii | Mudamba | |
| iii | Mundu ung'aire sana | |
| iv | Mukhasi uli inda | |
| v | Mundu mulema | |
| vi | Mundu wivusianga vakhasi | |

| | | |
|---|---|---|
| vii | Musatsa kose mukhasi ukholanga mapenzi rwanyi wa indoa yae | |
| viii | Musatsa ukholanga mapenzi nende musatsa wasie | |
| x | Mukhasi ukholanga mapenzi nende mukhasi wasie | |

(b) Khubera sina mera akawakhandika ako kekhonyerwanga?

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

## Sehemu C

**8.** Tsinjira sina tsiekhonyerwanga khunyola mera kechesia heshima ka okhulanga ebikhole, obuchafu au ebindu bya aibu imberi wa abandu? Rusiakho mifano kya omanyire.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

**ORIO MUNO**

## KIAMBATISHO B: <u>HOJAJI</u> (KISWAHILI)

Mimi ni mwanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo ninasomea shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Ipo picha inayojitokeza kuwa wauguzi, watoa ushauri nasaha, wahamasishaji, wagonjwa na wanajamii kwa jumla hukosa tasfida za kutumia hasa katika kueleza maswala ya kimatibabu. Naomba ujaze hojaji hii ambapo majibu yako yatakuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kazi hii. Nakuomba kuwa usiandike jina lako kwenye karatasi hii.

### Sehemu A

Chagua kipengele kimoja pekee kinachokuhusu katika (a), (b), (c) na (d) kwa kuchorea mviringo.

**1. (a) Miaka**

i. 18-30 ii. 31-40

iii. 41-50 iv. 51 - Zaidi

**(b) Jinsia**

i. Kiume ii. Kike

**(c) Kiwango cha masomo**

i. Shule ya msingi ii. Shule ya upili

iii. Chuo anuwai iv. Chuo kikuu

**(d) Eneo la makazi**

i. Mashambani ii. Mjini

**(e) Kazi**………………………………………………………………………………………

### Sehemu B

Jaza majibu yako katika nafasi ulizopewa. (Muktadha wa matibabu unahusisha tiba, ushauri nasaha, uhamasishaji na uasaji wa watu katika jamii.)

**2.** (a) Andika magonjwa haya namna yanavyoitwa kwa lugha ya heshima au upole katika ktadha wa matibabu.

| **Ugonjwa** | | **Namna ya kutaja kwa upole** |
|---|---|---|
| i. | Ukimwi | |
| ii. | Kaswende/Tego | |
| iii. | Upele | |
| iv. | Mba | |
| v. | Kansa | |
| vi. | Kuharisha | |
| vii. | Kisonono | |
| viii. | Kifua kikuu | |
| ix. | Bawasiri | |
| x. | Ugonjwa wa moyo | |
| xi. | Shinikizo la damu | |

**Maelezo:** Kisonono *(Gonorrhoea)*, Kaswende/Tego *(Syphilis)*, Bawasiri *(Haemorrhoids)*, Kifua kikuu *(Tuberculosis)*, Shinikizo la damu *(High blood pressure)*, mba *(skin disease)*

(b) Kwa nini majina hayo ambayo umetaja hutumiwa kurejelea magonjwa hayo.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………...

**3.** Vitendo hivi hurejelewa vipi kwa njia ya heshima, isiyotisha na kuleta aibu katika muktadha wa matibabu?

| | | |
|---|---|---|
| i. | Kudunga shindano | |
| ii. | Kuzalisha mwanamke | |
| iii. | Kufanya upasuaji kwa mgonjwa | |
| iv. | Kupasha tohara | |

**4.** (a) Andika majina yanayotumiwa kurejelea vitendo hivi kwa njia ya heshima au upole katika muktadha wa matibabu.

i. Kuzaa

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………….......

ii. Kukojoa

…………………………………………………………………………………………

iii. Kunia/Kunya

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

iv. Kuhara

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

v. Kutoa mimba

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

vi. Kujamiiana

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

vii. Kutapika

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

viii. Kushuta

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

ix. Msichana kuona damu

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

x. Kutoa manii

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

xi. Mwanamume kufanya mapenzi na mwanamume mwenzake

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

xii. Mwanamke kufanya mapenzi na mwanamke mwenzake

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

xiii. Kuwa na tendo la ndoa nje ya ndoa

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………....

(b) Kwa nini majina hayo hutumiwa?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**5.** (a)Sehemu hizi za mwili huitwaje kwa njia ya heshima hasa katika muktadha wa matibabu?

| **Sehemu** | **Jina linaloonyesha heshima** |
|---|---|
| i. Mboro | |
| ii. Kuma | |
| iii. Mkundu | |

| | |
|---|---|
| iv. Matako | |
| v. Matiti | |
| vi. Makende | |
| vii. Nywele zinazomea kwenye sehemu za siri<br>(Mavuzi) | |

(b) Kwa nini majina hayo ambayo umetaja hutumiwa?

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**6.** (a) Majina gani hutumiwa kwa njia ya upole kurejelea uchafu huu unaotoka kwenye mwili wa binadamu katika muktadha wa matibabu?

ii. Mafi ……………………………………………………………………………………...

iii. Mkojo ……………………………………………………………………………………

iv. Damu……………………………………………………………………………………..

v. Manii ……………………………………………………………………………………

vi. Usaha……………………………………………………………………………………

vii. Udenda ……………………………………………………………………………..

viii. Matapishi …………………………………………………………………………...

ix. Kamasi……………………………………………………………………………..

x. Mate…………………………………………………………………………………...

(b) Kwa nini majina hayo ambayo umetaja hutumiwa?

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**7.** (a) Watu hawa huitwaje kwa njia ya heshima au upole katika muktadha wa matibabu?

| | | |
|---|---|---|
| i. | Mwendawazimu | |
| ii. | Malaya | |
| iii. | Mtu aliyekonda sana | |
| iv. | Mwanamke aliye na mimba | |
| v. | Mtu mlemavu | |
| vi. | Mtu anayewazalisha wanawake | |
| vii. | Mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwenzake | |
| viii. | Mwanamke anayefanya mapenzi na mwanamke mwenzake | |
| x. | Mtu aliye na tendo la ndoa nje ya ndoa | |

(b) Kwa nini majina hayo ambayo umetaja hutumiwa?

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………...

## Sehemu C

**8.** Je, ni mikakati ipi inayotumiwa kubuni majina ya heshima ya kutajia vitendo, uchafu au hali fulani za aibu mbele ya watu? Toa mifano unayojua.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

.................................................................................................................

**ASANTE SANA**